# TASWIRA YA JAMII KATIKA RIWAYA ZA *YASINYA* NA *MWANASIASA*

**NA**

**KIMWEA JAMES GICHOBI**

**C50/72325/2014**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI YA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**IDARA YA KISWAHILI**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2019**

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote.

**KIMWEA JAMES GICHOBI** **Sahihi.............................................**

**(Mtahiniwa)** **Tarehe............................................**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi — Idara ya Kiswahili.

**PROF.MWENDA MBATIAH** **Sahihi.............................................**

**(Msimamizi)** **Tarehe.............................................**

**Bw. GITONGA JOSEPHAT JOHN** **Sahihi....................................**

**(Msimamizi)** **Tarehe.....................................**

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wavyele wangu, Selina Wanja Karingi na Marehemu Daniel Karingi Mwaniki kwa kunileta ulimwenguni huu, wakanilea na kunielimisha. Waama, mwangwi wa kauli ya mwenda zake baba kuhusu elimu bado unapenya masikioni mwangu. Kwa lugha ya Kingereza, marehemu alikariri kila uchao kwa aila yake kuwa*little knowledge is dangerous.* Tafsiri yake ni kwamba, elimu haba ni hatari. Katika ujana wangu, nilitafakari maneno hayo na kuapa kwamba sikuwa na budi kujiepusha na hatari ambayo huenda ingetokana na elimu haba. Falsafa ya marehemu baba ilinishawishi hadi nikajisajili katika kozi ya Shahada ya Uzamili. Mchango wa mama mzazi nao umenifaa sana. Katu, sikosi kukumbuka namna alivyonitia shime nilipokumbana na vizingiti katika usomi wangu.

## SHUKRANI

Ningetaka kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mungu Muumba kwa kunipa siha na uwezo wa kiuchumi nikamilishe kozi hii. Ninawapongeza pia wasimamizi wangu, Profesa Mwenda Mbatiah na Bwana Gitonga Josephat John kwa kunielekeza vyema katika shughuli nzima ya utafiti wangu. Ninautambua pia ushauri wa Bwana Sanja Leonard Leo katika hatua za mwanzo za kazi hii. Bila wao, naona ingekuwa muhali kukamilisha utafiti wangu.

Sikosi kuwashukuru wahadhiri wengine wa Chuo Kikuu cha Nairobi ambao wamenifunza na kunipa maarifa mengi ambayo pia yamekuwa muhimu katika utafiti huu. Wahadhiri hawa ni: Mwenyekiti wa idara ya Kiswahili na mratibu wa kozi ya Shahada ya Uzamili Profesa Iribe Mwangi, Profesa John Habwe, Profesa Rayya Timammy, Profesa Kineene Wa Mutiso, Daktari Evans Mbuthia, Daktari Amiri Swaleh, Daktari Prisca Jerono, Daktari Zaja Omboga na Daktari Jefwa Mweri.

Fauka ya hao niliotaja, ningetaka pia kuwapongeza wanafunzi ambao tulisoma pamoja darasani. Hawa ni: Lokidor Ekadeli Edward, Sarah Mueni Kivuva, Kiptum Jeruto Tecla, Cathreen Mungania, John Mugo, Godfrey Makori, Munyasya Florence Muthio, Patrick Oyinda, Virginia Wairimu Gaithuma, Maurice Lavaya, Muasya Victor Mumo, Gwako Bosibori Jackline, Winnie Awuor Oduor, Obila Alice Akinyi, Alivitsa Eunice, Braicy Inziani Endovu, Dorcas Jerotich Suter, Lonyce Mwakio, Njagi Lilly Murugi, Seraphine Kemuma Orucho na Risper Kinanga. Nilifaidika pakubwa kutokana na mijadala tuliyokuwa nayo na mawasilisho ya mada kutoka taaluma mbalimbali. Sitasahau jinsi tulivyotiana moyo wakati tulipokumbwa na hali za kutatanisha.

Shukrani zingine ziwaendee wote katika aila yangu ambao hawakukosa kunitia moyo katika usomi wangu.Ni muhali kuusahau msaada wa vitabu na ushauri niliopata kutoka kwa dadangu Elizabeth Wawira Karingi.Kwa walioipiga chapa kazi hii, nasema heko! Bila mchango wenu, ukamilifu wake haungepatikana.

Idadi ya waliotoa mchango wa kufanikisha tasnifu hii ni kubwa kuliko niliowataja. Madhali sitaweza kutaja kila mmoja wao, naomba wote wazipokee shukrani kutoka kwa kilindi cha moyo wangu. Ni matumaini yangu kwamba walionipa msaada wataendelea kuwafaidi wasomi wengine. Wanapotekeleza shughuli hiyo adhimu aushini, naomba:

Mola na uwajalie,

Mema uwazindishie,

Nao wakuinamie,

Amina waitikie.

## ORODHA YA VIFUPISHO

**BSKT** Bible Societies of Kenya and Tanzania

**CUP** Cambridge University Press

**TUKI** Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

## IKISIRI

Kwa namna ya kulinganisha na kulinganua, tasnifu hii imechunguza taswira ya jamii katika riwaya ya *Yasinya* (2014) ya Leonard Sanja Leo na *Mwanasiasa* (2014) ya Swale Mdoe. Tatizo la utafiti wetu limekuwa kuhakiki maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka katika riwaya hizo kwa msingi wa nadharia ya u-Marx wa kirasimi. Uchunguzi wetu katika tafiti za awali kuhusu uhakiki wa maudhui katika riwaya umeonyesha kwamba maudhui hayo — japo ndiyo yanayosisitizwa katika nadharia inayohusika — hayajashughulikiwa katika riwaya teule. Lengo letu la kwanza limekuwa kuhakiki maudhui, kutathmini uhalisia wake na kuonyesha kiasi cha kuhusiana kwa maudhui katika *Yasinya* na *Mwanasiasa* na suala la mgawanyiko wa jamii kitabaka. Lengo la pili limekuwa kubainisha jinsi fani kwa jumla ilivyotumiwa kuwasilisha maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka katika riwaya teule.Kazi yenyewe ina sura nne.Sura ya kwanza ina utangulizi, tatizo la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, umuhimu wa utafiti, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia, haipothesia na mbinu za utafiti. Katika sura ya pili, tumehakiki maudhui, tukatathmini uhalisia wake na kuonyesha kiasi cha kuhusiana kwa maudhui hayo na suala la mgawanyiko wa jamii kitabaka. Sura ya tatu imebainisha jinsi fani — kwa jumla — ilivyotumiwa kuwasilisha maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka katika riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa.* Sura ya nne ina hitimisho la utafiti ambapo tumetoa maelezo ya kina kuhusiana na malengo ya utafiti. Aidha, tumechunguza ufaafu wa nadharia ya u-Marx wa kirasimi na changamoto za utafiti. Mwisho kabisa, tumetoa pendekezo kuhusu utafiti wa baadaye, tukaweka muhtasari wa hitimisho na orodha ya marejeleo.Kwa ufupi, matokeo ya utafiiti huu yamekuwa kwamba maudhui makuu ya mgawanyiko wa jamii kitabaka ni umaskini na utajiri. Maudhui hayo yamewasilishwa kiuhalisia japo kuna ukwepaji wa uhalisia kwa viwango tofauti katika riwaya teule. Ni kupitia kwake ambapo matabaka makuu katika jamii yamesawiriwa. Tabaka la matajiri ni la watawala, ukoo na washirika wao huku la maskini likiwa la watawaliwa. Kwa hivyo, matabaka makuu katika jamii ya sasa hayakusawiriwa kama Marx alivyoyaeleza.Hivi ni kutokana na mfumo wa kiuchumi, ulio ubepari uchwara, unaoendelezwa katika jamii zinazowakilishwa na riwaya tulizozihakiki na ambao ndio pia unaotawala mataifa ya Kiafrika kwa sasa. Katika mfumo huo, matabaka aliyoyazungumzia Marx (mabwanyenye na wafanyikazi) na yaliyokuwa na dhima ya kuzua mivutano ili kuiwezesha jamii kuendelea na kufikia ukamilifu wa kinjozi kupitia ngazi za kiuchumi: ujima, utumwa, umwinyi, ubepari, ujamaa na kisha ukomunisti hayapo. Kwa mujibu wa riwaya teule, mivutano iliyopo katika jamii ni baina ya tabaka tawala na tabaka tawaliwa. Hata hivyo, nafasi ya mivutano hiyo kuleta maendeleo chanya ya jamii ni finyu mno hasa katika riwaya ya *Yasinya*.

## YALIYOMO

**UNGAMO** .................................................................................................................. **ii**
**TABARUKU** .............................................................................................................. **iii**
**SHUKRANI** ............................................................................................................... **iv**
**ORODHA YA VIFUPISHO** .......................................................................................... **vi**
**IKISIRI** ..................................................................................................................... **vii**
**YALIYOMO** .............................................................................................................. **viii**

**SURA YA KWANZA** .................................................................................................... **1**
1.0 Utangulizi ................................................................................................................ 1
1.1 Tatizo la utafiti ........................................................................................................ 3
1.2 Maswali ya utafiti .................................................................................................... 4
1.3 Malengo ya utafiti .................................................................................................... 4
1.4 Umuhimu wa utafiti ................................................................................................. 4
1.5 Upeo na mipaka ....................................................................................................... 5
1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada ................................................................................... 6
1.7 Misingi ya nadharia ................................................................................................. 12
1.8 Haipothesia ............................................................................................................. 16
1.9 Mbinu za utafiti ....................................................................................................... 16
  1.9.1 Uteuzi wa sampuli ........................................................................................... 16
  1.9.2 Ukusanyaji wa data ......................................................................................... 17
  1.9.3 Uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti ........................... 18
  1.9.4 Usahihi wa utafiti ............................................................................................ 18
  1.9.5 Hitimisho ......................................................................................................... 18

**SURA YA PILI** ........................................................................................................... **19**
**MAUDHUI YA MGAWANYIKO WA JAMII KITABAKA KATIKA RIWAYA ZA *YASINYA NA MWANASIASA*** ........................................................................................ **19**
2.0 Utangulizi ................................................................................................................ 19
2.1 Umaskini na utajiri .................................................................................................. 19
2.2 Nafasi ya dini katika mfumo wa kitabaka ................................................................ 37

2.3 Ubaguzi na mchakato wa kutafuta usawa katika jamii iliyogawika kitabaka ............ 43
2.4 Hitimisho........................................................................................................ 53

**SURA YA TATU ........................................................................................... 60**
**FANI NA UWASILISHAJI WA MAUDHUI YA MGAWANYIKO WA JAMII KITABAKA KATIKA RIWAYA ZA *YASINYA* NA *MWANASIASA*. ..................... 60**
3.0 Utangulizi........................................................................................................ 60
3.1 Uchambuzi wa fani kwa jumla ...................................................................... 61
3.2 Hitimisho........................................................................................................ 85

**SURA YA NNE ................................................................................................ 87**
**HITIMISHO ..................................................................................................... 87**
4.0 Utangulizi........................................................................................................ 87
4.1 Maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka katika *Yasinya* na *Mwanasiasa*............ 87
4.2 Fani na uwasilishaji wa maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka........................ 93
4.3 Ufaafu wa nadharia husika na changamoto za utafiti ............................................... 94
4.4 Pendekezo kwa watafiti wa baadaye.......................................................................... 97
4.5 Muhtasari wa hitimisho............................................................................................ 97

**MAREJELEO ................................................................................................... 99**

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Mada ya utafiti wetu inahusiana na uhakiki wa riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa*. Riwaya ya *Mwanasiasa* inahusu utawala mbaya na jinsi watawaliwa hasa wanaokaa Bondeni ya viamboni wanavyojinasua kutokana na utawala huu unaowakandamiza. Kwa kiwango cha juu, riwaya hii inasawiri maisha ya wanajamii kiuyakinifu. Mfano mzuri wa usawiri wa jamii jinsi hii unaonekana kupitia kwa Mwarupia — mhusika wa kimaendeleo. Yeye anatumiwa kama kipaza-sauti cha mtunzi kupulizia uhai kwa wachochole wa Bondeni ya viamboni. Katika riwaya hii, maisha ya Wanabonde na matatizo waliyopitia yameelezwa kihistoria. Historia hii inafahamika hata kupitia majina ya makazi katika Bondeni ya viamboni kwa wachochole na Bondeni Mpya kwa matajiri. Kama tunavyojulishwa na msimulizi, majina haya yalitokana na sababu au jambo fulani lililowahi kutendeka katika enzi zilizopita.Kwa miaka mingi, Wanabonde walikabiliwa na ukata lakini hawakuzozana. Japo Bondeni ilikuwa na makabila mengi, Wanabonde waliishi kwa amani kama watu wa kabila moja la walalahoi. Hali ya sasa ya wanaonyanyaswa inatokana na kosa la Wanabonde ambao kwa muda mrefu, walikuwa wakiwachagua viongozi wasiofaa kila msimu wa uchaguzi. Viongozi hawa walitorokea mijini mara baada ya kuchaguliwa huku wakionekana tu wakati wa kutaka kuchaguliwa tena.

Kutokana na uongozi mbaya wa Bwana Mkubwa, Jamii ya Wanabonde imegawika katika matabaka mawili: tabaka linalowakilishwa na matajiri au mamwinyi wanaokaa Bondeni Mpya na tabaka linalowakilishwa na wachochole wanaokaa Bondeni ya viamboni. Kwa muda mrefu, tabaka la walalahoi limekuwa gizani likinyanyaswa hadi pale ambapo linapozinduliwa na hivyo basi kuanza harakati zinazolenga kuboresha hali yao ya maisha. Hata hivyo, Bwana Mkubwa na wanasiasa wa mrengo wake hawasitishi dhuluma kwa Wanabonde wachochole na hawako tayari kuachilia uongozi wa Bondeni.

Utawala wa Bwana Mkubwa unadumisha utabaka katika jamii kupitia vyombo kandamizi vya dola kama vile polisi na magereza  na vyombo vya ki-itikadi vya dola hasa asasi za sheria na siasa. Hali hii inazua mivutano na mwamko wa mabadiliko unaotanda Bondeni. Mwarupia anawaongoza Wanabonde katika maandamano yanayozua makabiliano ya silaha na kusababisha umwagikaji wa damu. Hatimaye Wanabonde wanafanikiwa kupindua utawala wa Bwana Mkubwa ambaye anatoroka kisiri hadi nchi jirani. Waliokuwa na vyeo katika utawala wake pamoja na matajiri waliowadhulumu wanabonde pia wanatoroka na hawakuonekana tena

Bondeni. Mashamba yaliyoibwa na matajiri yanawarudia Wanabonde waliokuwa maskini. Mwarupia anaunda utawala mpya wa Bondeni — utawala uliozingatia utawala wa watu na usawa wa Wanabonde wote bila kubaguliwa katika msingi wa kikabila — utawala uliohakikisha kuwa kila mtu alikula jasho lake.

Riwaya ya *Yasinya* inahusu masuala yanayozitatiza na kuzidunisha nchi nyingi barani Afrika na kuzifanya zikose mshikamano, ustawi na maendeleo. Suala la kisiasa limetiliwa mkazo sana ambapo tamaa na ubinafsi hususan kwa viongozi ni mambo ambayo yamechangia pakubwa kuunda matabaka katika jamii ya Mabonde.Kama ilivyo katika riwaya ya *Mwanasiasa*, maisha ya wanajamii wa Mabonde katika riwaya ya *Yasinya* yameelezwa kihistoria. Kwa siku nyingi, hasa katika ukoloni mkongwe, watu wa Mabonde waliishi chini ya ubaguzi na chuki. Kwa miaka mingi baada ya uhuru, Mabonde haijaendelea kutokana na tamaa na ubinafsi hususan wa viongozi na washirika wao. MA (mhusika wa kihistoria anayepatikana katika kisasili cha jamii ya Mabonde) anashangaa kugundua kwamba hata baada ya miaka hamsini na zaidi ya kupata uhuru, bado kulikuwa na maradhi, ujinga, umaskini na uzembe wa kutoungana ili juhudi za kuvuta pamoja zifaulu. MA anaiita hali hii ya kutoendelea utasa huku akiona kwamba ni jukumu la kizazi kipya kuleta mabadiliko chanya katika jamii.

Masaibu mengi wanayopitia Wamabonde (katika *Yasinya*) yanatokana na uongozi mbaya wa Kifuja hasa baada ya kusadiki na kufuata ushauri mbaya kutoka kwa kizazi cha kina Mayowe. Kizazi hiki kinaendeleza ukoloni mamboleo. Ni kizazi kinachotilia utabaka mbolea kwa kumpa Kifuja ushauri unaopotosha. Aidha, kizazi hiki kinaiga mapisi ya kizazi cha MA ambayo kwa muda mrefu uliopita yaliongozwa na miko, kanuni na desturi zilizoendeleza tamaa, ubinafsi na utabaka. Katika hali hii, kizazi hiki kinashindwa kutekeleza wajibu wake wa kuleta umoja, udugu na utangamano wa watu.

Viongozi wa jamii ya Wamabonde wanashindwa kuweka mikakati ya kuiendeleza jamii. Badala yake, wanawahadaa watawaliwa. Baada ya kupata uhuru, tumaini kwa kizazi kipya kuleta demokrasia barani Afrika halipo maadamu kizazi hiki kimeiga ukoloni mkongwe na kuendeleza dhuluma kwa wanajamii barani Afrika.MA anasema kwamba nyoyo za kizazi kipya zimejaa ubinafsi, uchoyo na ulafi. Aidha, MA anasema kuwa hata sasa, anasikia kilio cha wanawe kama nyakati za Chebaskwony (anayewakilisha ukoloni mkongwe). Hali hii inasababisha kutamauka kwa jamii ya Wamabonde.

Viongozi na washirika wao wanajitokeza kama tabaka la matajiri. Viongozi hawa wanawadhulumu watawaliwa na kujiendeleza kwa njia zisizo za haki. Kutokana na hali hii, kunajitokeza Wamabonde wachache, hasa vijana, wanaopinga utabaka na dhuluma kwa wanajamii. Vita dhidi ya ulaghai, ubaguzi, ulanguzi wa dawa za kulevya na unyanyasaji wa Wamabonde inaungwa mkono na vijana wengine kutoka familia zilizo katika tabaka la matajiri. Wao wanawakilisha kisasi kipya ambacho kinaonekana kuwa na nafasi kubwa katika kutetea haki na kuondoa tofauti za kibinadamu zinazounda matabaka miongoni mwa wanajamii.

Asisi na wengine walio na maono sawa na yake wanaunda mashirika na kuanzisha miradi kwa lengo la kuwapa afueni Wamabonde wasiobahatika, wanaolaghaiwa na kunyanyaswa kutokana na uongozi mbaya wa Kifuja. Aidha, mashirika na miradi hii inawasaidia wanaoathirika kutokana na uraibu wa kutumia dawa za kulevya zinazouzwa na walio mamlakani kama Kifuja, kwa ushirikiano wa mjukuu wake (Huni) na Mayowe.Kutokana na juhudi za kina Asisi na Kijasiri kuleta mabadiliko chanya ya Wamabonde, Chifu Kifuja anaona tisho katika uongozi wake. Juhudi hizi pia ni tisho kwa shughuli haramu anazoendeleza na washirika wake ili kujitajirisha. Kwa sababu hii, kunazuka migogoro baina ya kiongozi huyu na wapinzani wake. Ili kuzima upinzani na kuendeleza maslahi yake, Chifu Kifujaanawatia hofu wale wote waliokwenda kinyume na matarajio yake. Katika hali ya vuta nikuvute baina ya utawala na upinzani, utawala dhalimu unaanguka katika hali isiyotarajiwa. Chifu mpya anachukua hatamu za kutawala Mabonde. Mabadiliko katika utawala yanaashiriwa na Chifu mpya kupitia kuachiliwa kutoka jela kwa Kijasiri, mmojawapo wa wapinzani sugu wa Chifu Kifuja na wafuasi wake.

### 1.1 Tatizo la utafiti

Tatizo letu ni kuhakiki maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka katika riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa*kwa msingi wa nadharia ya u-Marx wa kirasimi. Uchunguzi wetu katika tafiti za awali kuhusu uhakiki wa maudhui katika riwaya umeonyesha kwamba maudhui hayo —japo ndiyo yanayosisitizwa katika nadharia inayohusika — hayajashughulikiwa katika riwaya teule.Riwaya ya *Mwanasiasa* ni ya kisiasa. Kwa mujibu wa Wamitila (2003:182), riwaya ya aina hii ina msuko unaowahusu wanasiasa na maisha yao. Ni aina ya riwaya inayodhamiria kuyafichua mambo yanayotendeka kinyume na picha inayoonekana waziwazi. Katika riwaya ya aina hii, mwandishi hufichua uozo, ufisadi na unafiki uliojikita katika utekelezaji wa sera za uongozi.  Riwaya ya *Yasinya* ni ya kisosholojia/kijamii. Kuhusu riwaya ya aina hii, Wamitila (k.h.j) anasema kwamba ni ile inayosawiri maisha ya kawaida ya jamii kwa kuchunguza

matatizo yake; yawe ya kifamilia, kitabaka, kiuchumi, kisiasa au hata kiutamaduni. Kutokana na maelezo hayo, riwaya hizi zimejikita pakubwa katika masuala ya kihalisia.

Katika uhakiki, uhalisia huangazia masuala ya kipindi maalum kihistoria yanayoshughulikiwa na mwandishi fulani katika kazi yake. Kwa sababu hii, tumezihakiki riwaya teule kwa pamoja maadamu ni za wakati mmoja kihistoria. Aidha, zinaendeleza dhamira zinazohusiana huku zikijikita katika masuala sawia ya kisiasa na kiuchumi na ambayo ni kiungo cha mihimili ya nadharia ya u-Marx wa kirasimi. Matumizi yake kwa pamoja yamekuwa kiwakilishi cha jamii ya sasa au sampuli tosha ya kufanikisha malengo yetu. Tumezihakiki kwa pamoja na tukaweza kukadiria kwa kulinganisha na kulinganua mawanda au kiasi cha kuhusiana kwa maudhui na suala la mgawanyiko wa jamii kitabaka. Kadhalika, tumezihakiki kwa pamoja, tukalinganisha na kulinganua jinsi maudhui hayo yalivyowasilishwa pamoja na viwango vyake vya uhalisia. Kulinganisha na kulinganua kwa riwaya hizi kumewezesha uhakiki wetu kuwa na dayolojia ambapo fasihi moja hujibizana na nyingine na kuzifanya tungo teule zifahamike zaidi.

### 1.2 Maswali ya utafiti

1. Ni kwa kiasi gani maudhui ya *Yasinya* na *Mwanasiasa* yanavyohusiana na suala la mgawanyiko wa jamii kitabaka?
2. Maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka yamewasilishwaje?

### 1.3 Malengo ya utafiti

1. Kuhakiki maudhui, kutathmini uhalisia wake na kuonyesha kiasi cha kuhusiana kwa maudhui katika *Yasinya* na *Mwanasiasa* na suala la mgawanyiko wa jamii kitabaka.
2. Kubainisha jinsi fani kwa jumla ilivyotumiwa kuwasilisha maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka katika riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa*.

### 1.4 Umuhimu wa utafiti

Uhakiki wetu umefaulu kuzifasiri tungo zinazohusika katika misingi ya nadharia maalum na kuchangia katika uelewekaji wake. Yaani, mpokezi wa kazi hii ataelekezwa katika usomaji wa riwaya teule na hivyo basi kufaidika kutokana na thamani za kiumbuji na kimaana za riwaya hizo. Aidha, utafiti huu ni mchango unaoendeleza mawanda ya kiuhakiki kwa kutumia nadharia ya u-Marx wa kirasimi.Umeongeza marejeleo katika fasihi ya Kiswahili na hivyo basi, utafanikisha ufundishaji na uelewekaji wa somo la uhakiki katika mtalaa wa fasihi. Katika kurejelewa kwake, utafiti wetu utakuwa msingi wa uhakiki wa baadaye kuhusu riwaya teule

madhali hakuna fasiri ya kazi ya kifasihi inayoweza kusemwa kuwa ni ya mwisho.Nadharia teule (u-Marx wa kirasimi) imekuwa muhimu katika utafiti wetu kwa kuwa inaangazia masuala ya kisiasa, kiuchumi na kitabaka ambayo kwa muda mrefu, yamechukua sehemu kubwa ya maudhui katika fasihi ya kihalisia. Aidha, hakuna nadharia nyingine inayoisawiri jamii kitabaka katika msingi wa kiuchumi-jamii kama ambavyo imeshughulikiwa katika nadharia hii.

**1.5 Upeo na mipaka**

Upeo wa utafiti wetu umekuwa kuhakiki maudhui na fani katika riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa*. Japo kuna maudhui mengi katika riwaya teule na namna anuwai za kuyashughulikia, maudhui ambayo tumehakiki ni ya mgawanyiko wa jamii kitabaka na yaliyojikita katika uhalisia. Maudhui hayo yana nguzo zake katika vipengee na dhana za kimsingi za nadharia ya u-Marxkama inavyoonyeshwa katika misingi ya nadharia. Kutokana na mabadiliko mengi ambayo u-Marx umepitia, uhakiki wa ki-Marx una mikabala mingi ya kihakiki chini ya kichwa kimoja (cha u-Marx). Kimsingi, utafiti wetu umeongozwa na nadharia ya u-Marx wa kirasimi. Haya ni mawazo asili ya Karl Marx (1818-1883) na Friedrich Engels (1820-1895) kabla ya muendelezo wa u-Marx.

Tumeiteua nadharia hii kwa kuwa ndiyo inayosheheni mawazo ya kina, jumuishi na asili ya Karl Marx na Friedrich Engels kuhusu mfumo wa kitabaka na ubepari ambayo bado hayajawahi kukanushwa na yeyote. Aidha, nadharia hii ni kielelezo cha hali halisi ya jamii na zana muhimu ya kujihami dhidi ya mazingira makali yaliyo na msingi wake katika utabaka. Nadharia zilizotokana na muendelezo wa u-Marx zilichota mawazo kutoka kwa nadharia ya u-Marx wa kirasimi. Hivi ni kumaanisha kwamba muendelezo wa nadharia ya u-Marx haukujumuisha mawazo yote ya Marx na Engels. Kwa hivyo, matumizi ya nadharia badala katika utafiti wetu hayangefaa kuliko nadharia ya u-Marx wa kirasimi katika kuitoa taswira kamili ya jamii kuhusu mgawanyiko wake kitabaka.

Mbali na maudhui ambayo tumehakiki, tumeonyesha jinsi uhalisia umejitokeza katika jamii. Bila kupotosha malengo yetu, tumetoa mifano inayohusisha mandhari na wahusika ili kuhimili uchambuzi wa maudhui katika riwaya teule. Tumethibitisha uhalisia wa maudhui hayo kwa kujikita katika jamii pana ya kisasa kama inavyowakilishwa katika riwaya ambazo tayari tumezihakiki.Kadhalika, tumechunguza fani lakini kwa ujumla.Katika kufanya hivyo, tumeonyesha jinsi tawi hili la fasihi (fani) lilivyotumiwa kuwasilisha maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka. Kipindi cha sasa kinachorejelewa katika utafiti huu ni miaka kadha baada ya

uhuru ambapo wanajamiikatika riwaya husika wanajitawala wenyewe. Hii ni miaka takribani hamsini baada ya kupata uhuru.

**1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada**

Kwa mujibu wa Mbatiah (2016:53), tabaka ni kundi la watu katika jamii inayotawaliwa na mfumo wa kiuchumi unaowagawa watu katika misingi ya uwezo wao wa kumiliki rasilimali. Mfumo wa kitabaka ni utaratibu wa kuwaweka watu katika matabaka mahususi kama vile mabwanyenye na wafanyikazi katika mfumo wa kibepari. Mawazo haya yanalingana na mawazo ya Wamitila (2003: 210) anapolieleza tabaka kama kundi la watu walio na sifa sawa za kiuchumi.

Kulingana na Marx (1998) katika kitabu kiitwacho *The Communist Manifesto*, matabaka sita yafuatayo ndiyo yaliyopatikana katika jamii za kibepari: Tabaka la mabwanyenye, la wafanyakazi, la kati katika jamii, la waliotengwa katika jamii, la makabaila na pia la wakulima.Tabaka lamabwanyenye lilikuwa la watu waliomiliki mbinu zote za uzalishaji mali.Yaani,liliundwa na waliodhibiti siasa na uchumi katika tawala za kibepari zilizoibuka baada ya kuporomoka kwa ukabaila (umwinyi) uliohusu utawala wa kifalme huko ulaya. Kwa ufupi, tabaka la kibwanyenye ni tabaka lililojenga na kuendelea kuudhibiti ubepari. Haya yanaelezwa na Mbatiah (2016:94) katika urejelezi wake wa Arnold Kettle (1967:28). Tabaka la wafanyakazi lilikuwa la watu ambao hawakuwa na mbinu za kuzalisha mali bali waliuza nguvu zao ili waishi. Lilikuwa tabaka la wale walioajiriwa na mabwanyenye katika mfumo wa kibepari. Tabaka la kati katika jamii liliundwa na watu walioajiriwa kazi na ambao waliweza kununua nguvukazi kidogo. Hawa walijumuisha wamilisi wa biashara ndogondogo na wenyeji wa mashamba ya kupangisha. U-Marx ulitabiri kwamba mwishowe, maendeleo katika uvumbuzi wa namna ya kuzalisha mali yangeliharibu tabaka hili na kuwazusha waliomo kutoka tabaka la kati hadi katika tabaka la wafanyikazi (wauza nguvukazi). Tabaka la waliotengwa katika jamii lilijumuisha wahalifu, ombaomba na makahaba — watu ambao hawakuwa na nafasi yoyote katika uchumi wa nchi. Hawa ni watu wasio na uhuru wa kimawazo na kwa hivyo hushawishiwa na kila mzabuni au anayewajaribu.Tabaka la makabaila lilikuwa la matajiri waliokuwa na nguvu za kisiasa na ambao walimiliki majumba na ardhi za kupangisha kwa faida zao binafsi au za watu wachache. Hili ni tabaka muhimu kihistoria. Tabaka la wakulima liliundwa na watu waliotapakaa na ambao walikosa uwezo wa kupanga na kuleta mabadiliko ya kijamii na kiuchumi. Wengi wao hatimaye huingia katika tabaka la wafanyikazi wanaouza nguvukazi huku wengine wakiishia kuwa makabaila.U-Marx ulitabiri kwamba katika maendeleo ya jamii kiuchumi, mfumo wa kitabaka

utabadilika na kuyafanya matabaka kuwa mawili tu na yanayokinzana — maskini na matajiri (tafsiri yetu).

Akishughulikia suala la riwaya na uhalisia, Mbatiah (2016:95) anasema kwamba mazingira ya kihistoria ambamo utanzu huu ulichimbuka huko Ulaya yalikuwa kuporomoka kwa ukabaila na kuinuka kwa ubepari. Fasihi iliyotawala wakati wa ukabaila ilikuwa ya kiramsia — fasihi iliyokwepa uhalisia wa maisha. Fasihi hii ilizua picha ya ulimwengu wa kinjozi uliojaa vituko vya mashujaa waliotenda miujiza ya kila aina. Ni fasihi iliyoandikiwa makabaila waliodhibiti mfumo wa kifalme ili kuwaburudisha wasisumbuliwe na matatizo yaliyowakabili maskini. Mbali na hayo, fasihi hii ilikusudia kuwapumbaza maskini ili waendelee kulitumikia tabaka tawala bila kulalamika.Katika karne ya 18, kuliibuka tabaka la kibwanyenye. Tabaka hili liliiona fasihi ya kiramsia na mfumo wa ukabaila kama vikwazo vilivyolizuia kupata uhuru kamili hususan katika kujenga jamii ambapo mtu binafsi aliweza kushughulikia maslahi yake bila vizuizi. Kwa hivyo, fasihi ya kiramsia haikuwapa mabwanyenye nafasi ya kujiendeleza kibinafsi. Kwa mabwanyenye, fasihi ya kiuhalisia iliwafaa sana katika kuendeleza matamanio yao. Hivi ni kwa sababu fasihi hii iliweza kuonyesha tajiriba za watu katika shughuli zao za kila siku. Aidha, fasihi ya kiuhalisia ililifaa tabaka la mabwanyenye katika kuelezea mwonoulimwengu wake ulioegemea ubinafsi, ubiashara na usokidini.Mbatiah anaendelea kusema kwamba biashara ya watumwa ndiyo iliyoweka msingi wa ubepari. Hivi ni kwa sababu biashara hii ilitoa nguvukazi yenye gharama ya chini na hivyo basi kuwawezesha wawekezaji kupanua biashara na tasnia zao.Akieleza kuhusu mfumo wa kiuchumi uliodumishwa Zanzibar na Waarabu, msomi huyu anasema kwamba mfumo huo ulikuwa wa kikabaila (kimwinyi). Utawala ulikuwa wa kifalme ambapo ukoo wa kifalme ulimiliki ardhi na watumwa. Kwa kiasi kidogo, kulikuwa na ubepari uliotokana na athari za wafanyibiashara wa Kihindi na Kizungu. Matabaka yaliyokuwamo wakati huo yalikuwa ya aina tatu.

a. Tabaka tawala la makabaila wa Kiarabu.
b. Tabaka la wafanyibiashara wa Kihindi na Kizungu.
c. Tabaka la Waafrika maskini waliokuwa wengi.

Mawazo haya yanatuonyesha hila zilizotumiwa na makabaila ili kuendelea kuwanyanyasa maskini na kudumisha matabaka katika jamii. Aidha, tunaona jinsi tabaka la kibwanyenye lilivyoitumia fasihi ya kiuhalisia kujenga jamii iliyoendeleza ubinafsi ambao huchangia pakubwa katika kuendeleza matabaka. Mawazo haya yamekuwa muhimu katika utafiti wetu maadamu yanadhihirisha mahusiano ya utabaka na fasihi ya kiuhalisia. Kihistoria, yametupa msingi wa

mfumo wa utabaka. Ni mawazo yaliyomo katika kitabu kiitwacho *Riwaya ya Kiswahili: Chimbuko na Maendeleo Yake* (2016) kinachoangazia kuzaliwa, kukua na kukomaa kwa riwaya ya Kiswahili katika msingi wa nadharia ya Sosholojia ya Fasihi na kwa hivyo hayafanani na utafiti wetu.

Kwa mujibu wa Njogu na Wafula (2013:63), wanauhalisia huitazama fasihi kama kioo cha jamii. Hivi ni kumaanisha kuwa fasihi huitoa picha ya jamii bila kuidunisha wala kuipiga chuku. Katika fasihi, mwandishi husawiri masuala ya wakati fulani yanayoikumba jamii inayoandikiwa. Maelezo haya yanaonyesha jinsi waandishi wa fasihi wanavyozingatia uhalisia katika tungo zao. Ni mawazo ambayo yametusaidia kuchunguza maudhui yanayoisawiri jamii kitabaka kwa msingi wa uhalisia katika riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa*. Haya ni mawazo yaliyomo katika kitabu kiitwacho *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi* (2013) kinachoshughulikia nadharia mbalimbali za uhakiki wa fasihi na hivyo basi ni tofauti kabisa na utafiti wetu.

Katika kitabu chake, *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar* (1997), Njogu ametumia nadharia ya u-Marx kutafiti kuhusu maudhui ya mapinduzi. Riwaya anazozihakiki ni pamoja na *Dunia Mti Mkavu* (1980), *Nyota ya Rehema* (1976), *Utengano* (1980), *Asali Chungu* (1980), *Kiu* (1972), *Kasri ya Mwinyi Fuad* (1978) na *Kuli* (1979). Amechunguza mfumo wa kiuchumi na jinsi ulivyosababisha kutokea kwa mapinduzi wakati huo. Masuala mengine aliyoshughulikia ni jamii na muundo wa uzalishaji mali, ukoloni Visiwani, muundo wa jamii, elimu na nafasi za kazi, pupa, mikinzano ya kitabaka na mapinduzi ya kijamii, urazini wa kitabaka, asasi za kiutawala na usawiri wa mapinduzi. Njogu anasema kuwa mivutano ya kijamii, kiuchumi na kisiasa ndiyo iliyokuwa kichocheo cha mapinduzi ya Visiwani Zanzibar ya 1964 yaliyoondolea mbali utawala wa Kisultani. Kwa mfano, kulikuwa na mivutano mikubwa ya kitabaka baina ya matajiri na maskini. Mivutano hii ilidhihirika kupitia kwa migomo na kukaidi amri kwa tabaka la chini pamoja na pupa ya mali na mwili. Kwa kuwa mawazo ya Marx ni msingi wa nadharia ambayo tumetumia, utafiti wa Njogu umetuongezea maarifa kuhusu mtazamo wa Marx, uelewa wa kina wa nadharia teule pamoja na jinsi ya kuitumia katika utafiti wetu. Aidha, utafiti huu umetufaa katika kuchunguza maudhui na jinsi yanavyoisawiri jamii kitabaka na kihalisia katika riwaya ambazo tumezihakiki. Hata hivyo, mwelekeo wa Njogu katika utafiti wake, riwaya alizotumia kukusanyia data yake pamoja na kipindi cha historia kinachohusiana na utafiti wake ni mambo yanayofanya utafiti wake uwe tofauti kabisa na wetu.

Kwa kutumia nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi (UHU), Njoroge, (2014) amefanya utafiti juu ya viongozi kama visababishi vya mabadiliko katika riwaya za Mwenda Mbatiah. Riwaya

anazochunguza ni *Vipanya Vya Maabara* (2007) na *Majira ya Tufani* (2012). Katika kazi hii, makundi mbalimbali na jinsi yanavyojitokeza kama vipanya vya maabara yanajadiliwa. Makundi haya ya vipanya vya maabara yanatumiwa na viongozi katika kufanya majaribio yao huku yakitupiliwa mbali na kuangamia baada ya majaribio. Mbali na hayo, Njoroge anaeleza kuhusu viongozi na mchango wao. Aina tofauti za uongozi na sifa zake pia yamejadiliwa. Maudhui mengine yanayoshughulikiwa katika utafiti huu ni ufisadi, ubarakala, ukoloni mambo leo, ukabila na udhalimu.

Akirejelea Were (1983) Njoroge anaeleza kwamba viongozi wa Afrika huru wamekuwa wakipuuza umuhimu na ufaafu wa maadili ya umma katika matendo yao. Katika hali hii, jamaa zao, marafiki na kabila lao kawaida hupewa nyadhifa za juu katika uongozi na vilevile mishahara mikubwa pasipo kujali ustahili.Kuhusu utabaka, tabaka la chini ndilo linalojitokeza kama kundi la vipanya vya maabara. Mfano mzuri ni pale ambapo viongozi wanawatumia vijana katika uuzaji wa dawa za kulevya ili kujinufaisha kiuchumi. Utabaka pia unajitokeza katika mataifa yaliyoendelea na yanayoendelea ambapo mataifa yaliyoendelea hulazimisha mataifa yanayoendelea kufuata sera za kiuchumi zilizobuniwa na mashirika pacha ya Benki ya Dunia na Mfuko wa Kifedha wa Kimataifa. Sera za mashirika haya zinazojulikana kama mpango wa kubadilisha muundo wa kiuchumi ndizo zinazochangia mfumo wa kitabaka wa kimataifa hivi kwamba kuna mataifa maskini na mataifa tajiri. Lengo la mashirika haya na sera zake ni kupata namna ya kuyadhibiti kiuchumi mataifa maskini. Njoroge anasema kwamba ni jambo linaloshuhudiwa katika jamii kwamba wale wa tabaka la juu huweza kutambuliwa na huwa na uwezo mkubwa wa kudumisha ubaguzi, uonevu na ukandamizaji kupitia mikakati tofauti ya ubishi. Kwa sababu hii, matakwa ya wenye uwezo katika jamii aghalabu hudumu.Utafiti wa Njoroge umekuwa muhimu kwetu katika kuchunguza jinsi masuala ya tamaa ya mali, ubinafsi na uongozi mbaya yamechangia katika kuwako kwa matabaka katika jamii kwenye riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa*. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti kabisa na wetu kwa misingi ya mada, nadharia na hata mwelekeo.

Kwa kutumia nadharia ya Umitindo, Nyutu (2016), amechunguza mtindo katika kazi za kubuni za Leonard Sanja. Kimsingi, ameshughulikia tamathali za usemi katika tungo anuwai za nathari. Kazi hizi ni riwaya ya *Yasinya* (2014), tamthilia ya *Zinguo la Mzuka* (2011), na hadithi fupi mbili: "Mimba Ingali Mimba" katika *Mimba Ingali Mimba na Hadithi nyingine* (2006), na "Mwavyaji wa Roho" katika *Mwavyaji wa Roho na Hadithi nyingine* (2011). Katika mtindo, ameshughulikia: majazi, jazanda, istiari, ndoto, kinaya na maswali ya balagha. Katika hitimisho

lake, Nyutu amependekeza utafiti zaidi ufanywe katika tamathali zaidi za usemi hususan taswira, taharuki, kisengere nyuma, kisengere mbele, takriri, kejeli, chuku, sadfa, tashihisi na tashbihi. Aidha, amependekeza nadharia tofauti zitumiwe kutafiti kuhusu wahusika, usimulizi, ploti na mandhari. Katika utafiti wetu, tumeyachukua mapendekezo haya kwa kutumia nadharia badala ya u-Marx wa kirasimi ijapokuwa kwa kujikita katika fani kwa jumla. Bali na kuelekezwa jinsi hiyo, utafiti wa Nyutu umetufaa katika uelewa zaidi wa riwaya ya *Yasinya*. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti na wetu kinadharia na hata katika mkondo au mwelekeo wake. Hauhusiani na *Mwanasiasa* — riwaya mojawapo ambayo tumehakiki, wala haujikiti katika maudhui yanayoisawiri jamii kitabaka na kihalisia kama utafiti wetu ulivyo.

Katika tasnifu yake ya uzamili, Rono (2013) amehakiki maudhui na fani katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* (2012) ya Ken Walibora. Nadharia alizotumia ni umuundo na uhalisia wa kijamaa. Katika fani, Rono ameshughulikia wahusika. Baadhi ya maudhui aliyochunguza ni uozo wa viongozi, utabaka, ulitima, nafasi ya mwanamke, utu, ukosefu wa haki, tamaa na umuhimu wa mabadiliko miongoni mwa mengine. Rono anadhihirisha kwamba masuala ya utabaka yanayojitokeza katika nchi ya Tomoko inayoangaziwa katika *Kidagaa Kimemwozea* yana msingi wake katika ukoloni mamboleo. Miongoni mwa masuala haya ni ukosefu wa haki hasa kwa wanyonge, ukatili, upendeleo, unyang'anyi, na umasikini.Katika riwaya anayoihakiki, mhusika aitwaye Mtemi Nasaba Bora anajitokeza kama kiongozi anayewakilisha tabaka la juu la matajiri. Aliishi katika kasri. Alikuwa na mashamba na watumishi. Hata hivyo, Mtemi aliwabagua na kuwanyanyasa watu wa tabaka la chini wanaosawiriwa kupitia makazi duni, ukosefu wa mavazi na chakula bora. Japo Mtemi alikuwa katika hali nzuri ya kiuchumi, tamaa yake iliyokithiri ilimfanya awanyang'anye watu ardhi yao kikatili ili ajinufaishe kibinafsi. Alipanga mauaji ili kufanikisha unyang'anyi wa ardhi. Katika nchi ya Tomoko, mauaji yalihalalishwa kwa kutegemea mtendaji alikuwa nani na mtendwa alikuwa nani. Huu ni uovu unaodhihirisha kuweko kwa matabaka katika jamii. Utafiti wa Rono umetufaa katika kuchunguza masuala sawa na haya katika riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa*. Hata hivyo, Rono amechunguza maudhui katika ujumla wake tofauti na utafiti wetu ambao umechunguza maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka. Aidha, asili ya data yake si sawa na yetu. Kwa jumla utafiti wake ni tofauti kabisa na wetu.

Katika misingi ya nadharia za uhalisia na elimumitindo, Muthoni (2014) amehakiki maudhui na mtindo katika riwaya ya *Tikitimaji*. Anaeleza kuwa kama ilivyo kwa Wanatikitimaji, udhalimu na unyanyasaji umekithiri katika ulimwengu wa tatu. Utafiti wake unadhihirisha kwamba

changamoto zinazowakabili Wanatikitimaji ni za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Baadhi ya masuala anayoshughulikia ni uharibifu na uchafuzi wa mazingira, udhalimu, miundo msingi mibovu kutokana na uongozi mbaya na umaskini. Akieleza tofauti za kiuchumi miongoni mwa Wanatikitimaji, Muthoni anataja kwamba kwa muda mrefu, jamii imejengeka katika msingi wa kitabaka unaodhihirisha matabaka mawili: matajiri na maskini. Kulingana naye, hali hii inaendelea kuonekana katika mataifa mengi ulimwenguni. Kuhusu dhuluma, Muthoni anasema kwamba wanyonge wanadhulumiwa na vyombo vya dola hasa askari. Dhuluma hizi zinalenga kuwanyamazisha wanyonge ili kuzima harakati zao za kutaka kujikomboa. Kwa sababu ya uhusiano wa baadhi ya maudhui katika riwaya ya *Tikitimaji* na riwaya teule ambazo tumehakiki, tunaona kwamba kazi ya Muthoni imetufaa katika kuhakiki maudhui yanayofanana. Pia, imetuwezeshakuonyesha jinsi maudhui hayo yanavyoisawiri jamii kihalisia. Hata hivyo, utafiti wake ni tofauti kabisa na wetu hasa kwa kuzingatia mada, nadharia na asili ya data yake.

Kamunde (1983) ameshughulikia kilio cha wanyonge katika riwaya za Said Ahmed Mohamed. Ameonyesha 'unyonge' wa kiuchumi uliopo katika tabaka la chini na 'unyonge' wa tabia katika tabaka la juu kama unavyojitokeza katika *Utengano* (1980), *Asali Chungu* (1978) na *Dunia Mti Mkavu* (1980). Amefanya hivyo kwa kuchunguza jinsi wahusika wanavyodhihirisha 'unyonge' wao. Katika kazi hii, imebainika kwamba watu wa tabaka la chini wamedhalilishwa kupitia masuala ya kijamii pamoja na mifumo ya kisiasa na kiuchumi. Utafiti huu umekuwa muhimu kwetu hasa katika kuchunguza jinsi tofauti za kitabaka zinavyodhihirika katika riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa.*Kazi ya Kamunde imetufaa pia katika kuchunguza suala la udhalimu na jinsi unavyoendelezwa na tabaka tawala dhidi ya tabaka tawaliwa. Hata hivyo, asili ya data na mwelekeo wa utafiti huu ni tofautu kabisa na wetu.

Huku akitumia nadharia za Semiotiki na Dhima na Kazi, Bibiana (2014) amechunguza masuala ya kisiasa katika riwaya za Shaaban Robert. Riwaya alizochunguza ni *Kusadikika* (1951) na *Kufikirik*a (1967). Masuala aliyoshughulikia ni uongozi mbaya na mzuri, utii wa sheria, kujifunza mambo kutoka jamii nyingine, masuala ya kijinsia, amani, umoja na mshikamano. Bibiana anasema kwamba masuala ya kisiasa aliyoshughulikia ndiyo yaliyotawala majukwaa ya siasa katika nchi zote za Afrika, ikiwemo Tanzania. Katika utafiti wake, Bibiana anasisitiza umuhimu wa siasa katika maendeleo ya jamii. Akimrejelea Omary (2011), Bibiana anasema kwamba umuhimu huu ni kuamua aina ya mfumo wa maisha utakaofuatwa na wanajamii ambapo siasa huamua utoaji wa sera, mipango, bajeti, maamuzi kuhusu miradi ya maendeleo na utekelezwaji wake. Kwa hivyo, siasa ina mchango mkubwa katika kuyaongoza masuala ya

kiuchumi, kiutamaduni na kijamii.Kwa maoni yake, masuala ya kisiasa anayoyaeleza Shaaban Robert yana umuhimu mkubwa katika maendeleo ya mataifa machanga kama ilivyo Tanzania.Mbali na masuala ya kisiasa, Bibiana amechunguza mbinu za kisanaa zilizotumiwa na Shaaban Robert katika kuwasilisha masuala hayo katika riwaya teule. Mbinu alizochunguza ni matumizi ya methali, tashbihi, kejeli, mandhari na wahusika bapa.Utafiti wake umetufaa katika kuchunguza jinsi masuala ya kisiasa yanavyoathiri uchumi na maendeleo ya jamii na kuunda matabaka katika msingi wa kiuchumi. Mbinu za kisanaa zilizotumiwa kuwasilisha masuala ya kisiasa zimekuwa muhimu kwetu katika ubainishaji wa masuala ya kisiasa na jinsi yanavyoathiri uchumi wa jamii katika riwaya ambazo tumezihakiki. Katika mwanga huu, tumeweza kuelewa namna ya kuhusisha masuala ya kisiasa na kuweko kwa matabaka katika jamii. Hata hivyo, utafiti wa Bibiana ni tofauti sana na wetu maadamu umejikita katika kipindi cha zamani sana kihistoria. Aidha, mada yake, mwelekeo wa utafiti wake, riwaya na nadharia anazotumia ni tofauti kabisa na utafiti wetu.

Lomatoro (2014) ameshughulikia viwango vya uhalisi na ubunifu katika riwaya teule za Kiswahili. Riwaya alizochunguza ni *Kusadikika* (1951) ya Shaaban Robert, *Cheche za Moto* (2008) ya John Habwe na *Kaburi bila Msalaba* (1969) ya Peter Kariithi. Katika utafiti wake, Lomatoro ametumia nadharia ya uhalisia kuchunguza mbinu zilizotumiwa na waandishi kusawiri uhalisia na ubunifu katika riwaya za Kiswahili. Baadhi ya masuala ambayo kwayo uhalisia unajitokeza katika utafiti wake ni pamoja na mandhari, ukosefu wa uhuru, ukosefu wa maendeleo, mbinu za usafiri, uwepo wa vibanda, ufisadi, matumizi mabaya ya mamlaka, ukosefu wa dawa, umaskini n.k. Masuala ya ubunifu anayotaja ni kama vile sifa za ushujaa, wahusika wa kiajabu na miujiza. Utafiti huu umetufaa katika kuteua maudhui yanayoisawiri jamii kihalisia. Hivi ni kwa sababu uhalisia na ubunifu aghalabu huingiliana katika utunzi wa kazi za kifasihi. Hata hivyo, utafiti wa Lomatoro ni tofauti kabisa na wetu maadamu haujikiti katika kuchunguza maudhui au fani katika muktadha wa jamii iliyogawika kitabaka. Kadhalika, mwelekeo wa utafiti wake kinadharia ni tofauti na mwelekeo wa utafiti wetu.

### 1.7 Misingi ya nadharia

Utafiti wetu umeongozwa na nadharia ya u-Marx wa kirasimi au u-Marx mkongwe. Hii ni nadharia inayorejelea mawazo ya kiuchumi, kifalsafa na kijamii ya Karl Marx (1818-1883) na Friedrich Engels (1820-1895) yaliyoibuka na kujadiliwa kabla ya muendelezo wa u-Marx. Katika uasisi wake (u-Marx wa kirasimi), Karl Marx aliathiriwa pakubwa na mawazo ya Hegel katika dhana yake ya upembuzi.

Katika upembuzi, Hegel alizungumzia michakato mitatu ya kimawazo ambayo kwayo migongano hutokea. Michakato hii ni *tasnifu*, *tabaini* na *usanisi*. Kulingana naye, migongano hutokea katika kiwango cha kimawazo. Maoni ya Marx kuhusu upembuzi wa Hegel ni kwamba unapotosha. Yeye (Marx) alionelea kwamba migongano haitokei katika kiwango cha mawazo bali hutokea katika jamii. Ni Kutokana na mtazamo huu wa Marx ambapo aliamua kuiweka nadharia yake katika msingi wa muundo wa kijamii wa utabaka hususan utabaka wa kiuchumi-jamii.

Kulingana na Marx, historia ya maisha ya binadamu ni ya harakati za kitabaka. Harakati hizi husababishwa na tendo la kwanza la historia ya binadamu ambalo ni kutafuta njia ya kuyakidhi mahitaji ya kimsingi. Kama walivyosema Marx na Engels katika *The German Ideology*, mahitaji haya ya kimsingi ya binadamu ni kula na kunywa, kupata malazi na mavazi na mambo mengine. Ili kuyapata, binadamu hujiunga pamoja kwa lengo la kuimarisha ubora na wepesi wa kuizalisha mali ya kukidhi mahitaji hayo. Wanapoungana, binadamu hugawa majukumu au kazi. Ugawaji huu wa majukumu au kazi ndio msingi wa kuundwa kwa matabaka katika jamii. Hali hii inapoendelea, kunazuka mfumo wa ubepari. Katika mfumo huu, mali humilikiwa na idadi ndogo ya watu (Wamitila, 2002:183).Marx alieleza kwamba kile kinachotawala maudhui ya historia ya binadamu ni migongano na mivutano ya kitabaka iliyoletwa na hali ya kiuchumi na kisiasa. Migongano hii ndiyo iliyozaa hali mpya za kijamii na kusababisha jamii kuendelea kutoka enzi ya ujima, kisha umwinyi, ubepari na hatimaye ujamaa.

Misingi ya nadharia ya u-Marx wa kirasimi ni hali yakinifu katika maisha ya binadamu au uhalisi unaoonekana. Kwa mfano, nadharia hii ina msisitizo mkubwa kwenye msingi wa hali yakinifu ya mazingira ya kuishi kuliko mawazo katika maisha ya binadamu. Akimrejelea Baxandall, Njogu (1997:13) anasema kwamba uyakinifu humtarajia msanii auwasilishe uhalisia wa maisha katika hali yake ya kimaendeleo na kimapinduzi kikweli na kwa kuzingatia historia. Masuala ya kijamii yanayohusishwa na nadharia hii ni kama vile historia, uchumi, siasa, utamaduni, itikadi na mapinduzi. Kwa kiasi kikubwa, sifa za kikorombwezo (siasa, sheria, maadili, utamaduni, falsafa, itikadi, dini n.k.) hutegemea jinsi mali inavyozalishwa na kusambazwa (msingi). Haya yanafafanuliwa na mawazo ya Marx ambapo Njogu (1997:11) anasema kuwa hali za watu kijamii na hata kisiasa hazielekezwi na urazini wao bali ni mfumo wa uzalishaji mali katika hali halisi ya maisha. Hata hivyo, mabadiliko ya sifa za kikorombwezo kama vile mageuzi katika muundo wa kiutawala au kisiasa huweza kuuathiri msingi.

Mfumo wa ubepari unapoendelea, uzalishaji mali huongezeka huku tofauti za matabaka zikiimarika. Kuimarika huku kwa tofauti za matabaka hutokana na kufaidika kwa baadhi ya watu kwa njia zisizo za haki. Njia kama hizi ni unyonyaji wa wafanyikazi. Katika hali hii, ubepari kama njia ya uzalishaji mali hujitengenezea njia za kujiharibu wenyewe. Aidha, ubepari unaweza kuharibiwa kutokana na juhudi za wafanyakazi au tabaka la chini linalodhulimiwa.

Dhana za kimsingi za u-Marx wa kirasimi ni mkengeuko, itikadi na ubidhaaishaji (Wamitila 2002:183-185). Kuhusu itikadi, Wamitila anasema kwamba matamanio na matakwa ya matabaka yaliyopo katika jamii na hasa tabaka lenye nguvu yanaakisiwa katika itikadi iliyopo katika jamii, jinsi na miundo ya mawazo ambayo aghalabu huwa imeshika kwa nguvu na huwapo kila mahali kiasi cha kuwa huenda wanajamii wasiitambue kwa haraka. Kudadisi, kukosoa, kushutumu na kulaumu batili iliyopo katika itikadi ya kibwanyenye inayoimarisha ubepari ni muhimu katika kuangamiza mfumo wa ubepari. Dhana ya ubidhaaishaji hurejelea hali ambapo katika ubepari, watu katika tabaka la juu hununua na kumiliki vitu ambavyo labda hawavihitaji. Aidha, watu katika tabaka la chini hudhalilishwa na kutumiwa kama bidhaa hivi kwamba umuhimu wao huonekana tu katika uzalishaji mali.

Kabla ya kuweko kwa mwamko mpya katika jamii, kutakuweko na mkengeuko. Terry Eagleton (2005:18) alieleza dhana ya mkengeuko kama hali ambapo wanadamu hushindwa kutambua kuwa wao ndio waumbaji wa ulimwengu wanamoishi. Yaani, wanavyoishi ni matokeo ya wanavyowaza na wanavyotenda. Kabla ya mwamko, tabaka linalodhulumiwa huwa katika hali ya mkengeuko. Huwa halijajitambua na kujua kuwa linadhulumiwa. Hali hii inaweza kudhihirika kupitia lugha ya tabaka hili. Lugha hii huwa ni ya unyonge, mkengeuko na kukata tamaa. Ni lugha inayotokana na kushindwa kutambua kuwa jinsi hali ilivyo hutokana na mawazo na matendo yao. Jamii inapopata mwamko mpya, tabaka linalodhulumiwa hujitambua, watu huwa tayari kuleta mabadiliko na kupingana na dhuluma. Lugha zao hubadilika na kuwa si lugha za kiunyonge bali ni lugha za watu walio na nguvu. Wao huanza kuona kuwa wana uwezo wa kubadilisha hali yao ya kiunyoge na dhuluma kutoka kwa mabwanyenye.

Uhakiki uliojikita katika u-Marx wa kirasimi una mwelekeo mkubwa wa kutilia mkazo kwenye dhamira na maudhui. Huu ni mkabala unaoiangalia fasihi kwa kuihusisha na mazingira yake ya kihistoria pamoja na shughuli nyingine za kibinadamu. Kwa hivyo, u-Marx wa kirasimi unapinga mtazamo wa kuibagua na kuitenga fasihi na mazingira yanayoizaa. Kwa ufupi, utafiti wetu utaongozwa na mihimili ifuatayo ya nadharia ya u-Marx wa kirasimi.

1. Historia ya maisha ya binadamu ni ya harakati za kitabaka zinazosababishwa na tendo la kwanza la historia ya binadamu ambalo ni kutafuta njia ya kuyakidhi mahitaji ya kimsingi. Tumetumia mhimili huu kuchunguza jinsi harakati za kukidhi mahitaji ya kimsingi zinavyodhihirisha mgawanyiko wa jamii kitabaka.
2. Ugawanaji wa majukumu au kazi ndio msingi wa kuundwa kwa matabaka katika jamii na hatimaye kuzuka kwa mfumo wa ubepari. Mhimili huu umetuelekeza katika kuchunguza jinsi nafasi za kisiasa na uongozi zinavyochangia katika kuundwa kwa matabaka katika jamii.
3. Maudhui ya historia ya binadamu hutawaliwa na migongano na mivutano ya kitabaka iliyoletwa na hali ya kiuchumi na kisiasa. Tumeongozwa na mhimili huu kuchunguza jinsi hali tofauti za kiuchumi na kisiasa za wanajamii zinavyoibua migongano ya kitabaka na hatimaye maudhui yanayotokana na mivutano hii.
4. U-Marx wa kirasimi hutilia mkazo dhamira na maudhui na huihusisha fasihi na mazingira yake ya kihistoria pamoja na shughuli nyingine za kibinadamu. Utafiti wetu umeweka msisitizo kwenye maudhui ijapokuwa tumeshughulikia fani kwa jumla katika kuchunguza jinsi ilivyotumiwa kuwasilisha maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka.Maisha ya binadamu huelezewa zaidi kama uhalisi unaoonekana kama vile mazingira ya kuishi kuliko mawazo. Aidha, uhalisia huu huwasilishwa katika hali yake ya kimaendeleo na kimapinduzi kikweli na kwa kuzingatia historia. Mawazo haya yamekuwa muhimu kwetu katika kuchunguza uhalisia wa maudhui ambayo tumeyahakiki. Tumethibitisha uhalisia wa maudhui hayo kwa kujikita katika mawazo asili ya uhalisia (uhalisia wa kirasimi) ambao hasa ni uhalisia kabla ya muendelezo wa nadharia ya uhalisia. Kwa vile kuna mikondo mingi ya uhalisia, sisi tumejikita katika uhalisia kama mbinu ya kuhakiki inayozingatia hali halisi ya wahusika na lugha wanayotumia. Hali halisi ya kiuchumi na kisiasa ya wahusika ndiyo inayoibua matendo yao na kujenga maudhui halisi. Aidha, mkondo huu umetuwezesha kuchunguza jinsi fani ilivyotumika kuwasilisha maudhui ambayo tumeyachambua.
5. Masuala ya kijamii yanayohusishwa na nadharia hii ni kama vile historia, uchumi, siasa, sheria, utamaduni, maadili, itikadi, dini, falsafa na mapinduzi. Tumetumia mhimili huu kuchunguza namna masuala hayayanavyoathiriwa na msingi na jinsiyalivyoendeleza maudhui na kudhihirisha kiasi cha kuhusiana kwake na mgawanyiko wa jamii kitabaka.
6. Dhana za kimsingi za u-Marx wa kirasimi ni mkengeuko, itikadi na ubidhaaishaji. Dhana ya mkengeuko imetuwezesha kuchunguza namna mawazo potovu ya wanajamii

yamechangia katika kuendeleza na kudhibiti mgawanyiko wa jamii kitabaka. Mwamko wa jamii ambao umefuata mkengeuko umetuwezesha kuchunguza jinsi watu wa tabaka moja wanavyoweka juhudi za pamoja ili kujihami dhidi ya nguvu za tabaka jingine. Kwa kufanya hivyo, tumedhihirisha harakati za tabaka linalodhulumiwa ambazo zimelenga kuleta mapinduzi ambayo yamehusisha mageuzi katika muundo wa kiutawala unaolikandamiza tabaka tawaliwa. Dhana ya itikadi imetuwezesha kutathmini imani za wanajamii ambazo zimehalalisha utabaka huku ubidhaaishaji ukituwezesha kuchunguza jinsi tabaka tawaliwa limetumiwa kama bidhaa katika mazingira ya kuwatumikia matajiri.

### 1.8 Haipothesia

Zifuatazo ni haipothesia ambazo zimeongoza utafiti wetu.

1. Maudhui katika *Yasinya* na *Mwanasiasa* ni ya kihalisia na yanahusiana pakubwa na suala la mgawanyiko wa jamii kitabaka.
2. Fani imetumiwa kihalisia na kwa usahihi kuwasilisha maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka katika riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa.*

### 1.9 Mbinu za utafiti

#### 1.9.1 Uteuzi wa sampuli

Utafiti wetu umekuwa wa maktabani. Sampuli lengwa imekuwa riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa.* Huku akiwarejelea Newman na wenzake (2006:22) Bibiana (2014) anaeleza sampuli lengwa kama aina ya sampuli ambayo mtafiti huiteua akiwa na imani kwamba itampatia data itakayowezesha kukamilisha malengo ya utafiti wake. Uteuzi wa sampuli lengwa umefanywa kimakusudi na kama tulivyoamini, riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa* zimetupatia data ambayo imetufaa na ya kutosha katika utafiti wetu. Tumeziteua riwaya hizi kwa kusoma maandishi yaliyomo kwenye sehemu ya nyuma ya majalada ya riwaya mbalimbali. Maandishi hayo yamekuwa muhimu kwetu katika kutudokezea masuala yanayojadiliwa katika riwaya husika.Uteuzi wa kimakusudi unafanyika wakati elementi kutoka kwa sampuli zinateuliwa kupitia uamuzi wa mtafiti. Mtafiti huamini kuwa anaweza kupata sampuli wakilishi kwa kutumia uamuzi wa busara ambao utaokoa wakati na kupunguza gharama (Upekuzi wa mtandao: tafsiri yetu). Ni kutokana na imani hii ambapo tuliziteua riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa* na kwa kweli, zimetupatia majibu ya maswali yetu ya utafiti.

### 1.9.2 Ukusanyaji wa data

Data msingi imetokana na usomaji wa riwaya teule. Tumekusanya data hii kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa fani na maudhui. Kwa mujibu wa Mutea (2015:154-156), uchambuzi wa kimaudhui hutumiwa kudhihirisha maudhui na thamani za riwaya na hadithi fupi. Mbinu hii huwezesha kushughulikia kazi za aina nyingi, haina gharama kubwa na ni muhimu kwa kurekodi mabadiliko ya kiwakati. Kadhalika, mbinu hii inafaa katika kuchunguza maudhui ya kisiasa na kiuchumi maadamu inatumiwa kudhihirisha falsafa ya viongozi wakuu wa kitaifa pamoja na kuchunguza mbinu za propaganda zinazotumiwa na vyombo vya propaganda katika jaribio la kuathiri umma. Uchambuzi wa kimaudhui huwa wa kimaelezo au kiufafanuzi. Kwa hivyo, unaeleza tu yaliyomo na huenda usionyeshe maana ya matokeo ya utafiti. Hivi ni kusema kwamba uchambuzi huu hulijibu swali “nini?” na wala sio “kwa nini?” (tafsiri yetu).Kuhusu suala hili, Bibiana akimrejelea John (1997) anasema kwamba uchambuzi wa kimaelezo ni mbinu ya uchambuzi wa data ambayo humruhusu mtafiti kusikiliza au kusoma shairi, kisha kuelewa maudhui, falsafa, mtazamo, na kadhalika. Mbinu hii pia huhusisha uchambuzi wa lugha iliyotumika. Mbali na hayo, uchambuzi wa kimaelezo huruhusu utolewaji wa maelezo ya kina juu ya data zilizokusanywa na mtafiti kwa namna ambayo inawezesha kujibu swali au maswali ya utafiti husika.

Kufuatana na maelezo hayo, tumezisoma riwaya teule na kuchunguza maudhui na fani (kwa jumla) iliyotumiwa na waandishi husika. Katika usomaji huu, tumenukuu katika shajara, sehemu ambazo zimehusiana na malengo yetu ya utafiti. Aidha, tumekusanya data msingi kwa kujadiliana na wataalamu wa fasihi. Kwa kufanya hivyo, tumeweza kupata maoni na mielekeo yao mbalimbali kuhusu masuala ya utabaka na uhalisia katika muktadha wa kiuchumi-jamii.

Kwa kuzingatia maadili yote yanayohusiana na utafiti wa maktaba, tumekusanya data isiyo msingi katika maktaba za Chuo Kikuu cha Nairobi na vyuo vingine ambapo data hii imeweza kupatikana. Ili kupata data hii, tumesoma tasnifu, maandishi yanayoendeleza nadharia tunayotumia na miongozo iliyoandikwa na waandishi mbalimbali kuhusu masuala ya utabaka na uhalisia. Tumepekua mtandao, tukasoma majarida ya kiusomi, vitabu na makala yanayohusiana na utafiti wetu. Katika usomaji huu, tumenukuu mistari na aya ambazo tumeona kwamba zimetufaa katika utafiti wetu. Aidha, tumeyatafsiri maandishi muhimu kutoka lugha ya Kingereza hadi katika lugha ya Kiswahili. Maandishi kuhusu nadharia ya u-Marx wa kirasimi yamekuwa mwongozo muhimu katika kazi yetu. Kwa jumla, usomaji ambao tumeufanya umetuwezesha kuzichunguza riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa* kulingana na nadharia teule.

### 1.9.3 Uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti

Baada ya kuchanganua data tuliyoipata kwa kuzingatia maswali ya utafiti, malengo yake, haipothesia na nadharia ya u-Marx wa kirasimi, tumeyawasilisha matokeo ya utafiti wetu kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo. Huku tukilinganisha na kulinganua, tumetoa maelezo ya kina kuhusu maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka na jinsi fani kwa jumla ilivyotumiwa kuyawasilisha. Pamoja na maelezo hayo, tumedhihirisha jinsi uhalisia unavyojitokeza katika maudhui tuliyochanganua kwa kujikita katika jamii pana ya kisasa kama inavyowakilishwa katika riwaya teule.

### 1.9.4 Usahihi wa utafiti

Usahihi wa utafiti wa kitaaluma na kisayansi hutegemea mbinu na taratibu za utafiti zilizokubalika. Mbinu na taratibu hizi ndizo zinazowezeshamatokeo ya utafiti kuwa ya kuaminika. Utafiti wetu umeongozwa na mbinu zilizokubalika katika utafiti wa kitaaluma. Mbinu mojawapo ni uteuzi wa sampuli lengwa kimakusudi. Aidha, tumetumia mbinu ya uchambuzi wa kimaudhui na mbinu ya kimaelezo. Pamoja na kuongozwa na nadharia ya u-Marx wa kirasimi, tumetumia mbinu hizi katika kukusanya data, kuichambua na kuwasilisha matokeo ya utafiti wetu. Mbali na kutumia mbinu hizi, mtafiti na wasimamizi wa utafiti wamehakikisha usahihi wa utafiti huu kwa kujadili ufaafu wa nadharia husika pamoja na mbinu za ukusanyaji wa data, uchambuzi wake na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti.

### 1.9.5 Hitimisho

Masuala ambayo tumeshughulikia katika sura hii ni yale ya kitangulizi cha utafiti, ya kimsingi na ndiyo yanayoelekeza utafiti wetu. Masuala hayo ni usuli wa mada, tatizo la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, umuhimu wa utafiti, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia, haipothesia na mbinu za utafiti.

# SURA YA PILI

# MAUDHUI YA MGAWANYIKO WA JAMII KITABAKA KATIKA RIWAYA ZA *YASINYA NA MWANASIASA*

## 2.0 Utangulizi

Katika sura hii, tunachunguza maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka katika riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa* huku tukijikita katika nadharia ya u-Marx wa Kirasimi. Kwa mujibu wa mihimili ya nadharia hii, maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka yamejikita sana katika masuala ya kiuchumi na kisiasa. Mbali na kuchunguza maudhui, tunatathmini uhalisia wake kwa kujikita katika uhalisia kama mbinu ya kuhakiki inayozingatia hali halisi ya wahusika na lugha wanayotumia. Katika kufanya hivyo, tumetumia vigezo vinavyobainishwa na nadharia inayohusika kama vile uhalisi unaoonekana (mandhari ya mahali) na unaodhihirisha hali tofauti za kiuchumi za wanajamii. Vigezo vingine ambavyo tumetumia ni wahusika, matendo yao na matukio ya matendo hayo. Maelezo ya uhalisia yameoanishwa pamoja na ya maudhui kwa namna ya kulinganisha na kulinganua riwaya teule.

## 2.1 Umaskini na utajiri

Riwaya ya *Yasinya* inadhamiria kuonyesha jinsi tamaa ya mali na ubinafsi wa watu wachache katika jamii umechangia katika kuzikosesha mshikamano na maendeleo nchi nyingi barani Afrika. Walio katika mstari wa mbele kuyaendeleza maovu haya ni walio mamlakani pamoja na washirika wao. Zaidi ya hayo, riwaya hii inadhihirisha kwamba matatizo ya jamii hususan barani Afrika yana kiini chake katika historia ya jamii hizo. Historia hiyo inaonyesha kwamba, japo nchi hizo zilipata uhuru wa kujitawala kutoka kwa wakoloni, uhuru huo haukuleta maendeleo na ukomavu wa kisiasa na kiuchumi. Bado zinaitwa nchi changa. Katika *Yasinya*, matabaka mawili yanadhihirika: tabaka la maskini wanaotawaliwa na la matajiri walio mamlakani, ukoo na washirika wao. Maovu ya unyonyaji na ukandamizaji yaliyotendwa na wakoloni kwa Mwafrika yanaendelezwa na walioshika hatamu baada ya kuondoka kwa wakoloni. Katika hali hii, riwaya ya *Yasinya* inaonyesha wazi kwamba kwa sasa, nchi za Kiafrika zimekumbwa na ukoloni mamboleo.

Kadhalika, riwaya hii inalenga kuonyesha jinsi jamii barani Afrika zilivyotamauka kutokana na masaibu yanayozikumba. Inataka kudhihirisha kwamba tumaini kwa kizazi cha sasa kilichotarajiwa kuzikomboa jamii kutokana na athari za kikoloni halipo tena baada ya kizazi hiki

kuiga mienendo ya ukoloni mkongwe. Wanaokerwa na uongozi uliopo katika nchi za Kiafrika hawana uwezo wa kutosha kuzikomboa nchi zao kutokana na ushawishi mkubwa wa kisiasa na kiuchumi wa tabaka la matajiri linalojumuisha walio mamlakani. Hata hivyo, riwaya ya *Yasinya* inalenga kuonyesha kwamba si lazima mapinduzi yasababishwe na makabiliano ya kivita katika jamii inayodhulumiwa. Mtazamo wa u-Marx wa kirasimi kuhusu suala hii ni kwamba jamii haiwezi kuendelea bila mivutano ya kitabaka. Kwa hivyo, tungetarajia kuona maandamano na pengine mapinduzi kwa kuwa mahusiano ya matabaka ni ya mkinzano kutokana na matamanio ya kila tabaka huku nadharia za ki-Marx zikipaswa kuhusishwa na kuandamana pamoja dhidi ya mfumo wa kibepari kama anavyosema Wamitila (2002:184). Tamaa iliyokithiri ya mali inaonekana kama mbegu ya kujiangamiza kwa uongozi mbaya na hata ubepari. Hatima ya waliokuwa na tamaa ya mali katika riwaya hii ni vifo ambavyo havikutarajiwa.

Riwaya ya *Mwanasiasa* inakusudia kuyasawiri matatizo ya kisiasa na kiuchumi yanayozikumba nchi nyingi katika karne ya ishirini na moja. Matatizo hayo yanatokana na utawala mbaya unaoendelezwa na viongozi wasiowajibikia majukumu yao huku wakiyajali maslahi yao tu. Riwaya hii inadhihirisha kwamba, japo nchi nyingi za Kiafrika zimekuwa huru, uhuru huo haujakamilika kwani mahitaji yote ya wanajamii yanadhibitiwa na wengine. Kama ilivyo katika riwaya ya *Yasinya*, jamii katika riwaya ya *Mwanasiasa* imegawika katika matabaka mawili: wachochole na wakwasi. Ukosefu wa mahitaji ya kimsingi kwa maskini unazua hali ya kutamauka kwa wanajamii wengi. Aidha, riwaya hii inalenga kuonyesha udhaifu wa jamii katika kuchagua viongozi wao. Inaeleza kwamba kwa muda mrefu, wanajamii wamekuwa wakiwachagua viongozi walewale kila msimu wa kupiga kura japo viongozi hao hawakutekeleza majukumu waliyopewa. Badala yake, waliyapuuza na kuwapa waliowachagua ahadi za uongo.

Dhamira nyingine inayoendelezwa katika riwaya ya *Mwanasiasa* nikuwa hali ilivyo katika jamii inachangiwa na imani, mitazamo na matendo ya wanajamii wenyewe na kwamba wana uwezo wa kujikomboa kutokana na matatizo yanayowakumba hususan ya kiutawala. Jamii ina uwezo wa kupinga dhuluma, kupigania haki na usawa na hivyo basi kuangamiza matabaka yaliyomo katika jamii. Aidha, riwaya hii inalenga kuonyesha jinsi umaskini unavyoweza kumfanya binadamu amwabudu binadamu mwenzake. Haya yanajitokeza tunapotazama mahusiano baina ya Bwana Mkubwa na watawaliwa. Watawaliwa walinyenyekea kwa Bwana Mkubwa huku wakimwita majina yanayostahili kuitwa Mungu.

Maudhui ya umaskini na utajiri ni miongoni mwa maudhui tunayochunguza. Ingawa haya ni masuala mawili tofauti, kimantiki, hayawezi kutenganishwa. Kwa hivyo, tunayachanganua kwa

pamoja kwa minajili ya kulinganisha na kulinganua. Katika riwaya ya *Yasinya*, maudhui haya yanadhihirika kupitia wahusika mbalimbali na umilisi wao wa rasillimali muhimu za kujiendeleza kiuchumi. Umilisi na utumiaji wa ardhi ni mojawapo ya njia kuu za uzalishaji mali katika mfumo wa ubepari. Tukichunguza umilisi wa rasilimali hii, tunapata kwamba kulikuwa na maskwota hususan katika maeneo ya Kibisuswa, huku watu wengine wakimiliki mashamba makubwa. Kwa mfano, tunaarifiwa kuhusu 'mheshimiwa' katika uwanja wa Jamhuri palipokuwa na maombi ya umma. Kiongozi huyu aliyekuwa karibu na Asisi aliwaza juu ya shamba lake la mibuni huko Mlimani na lile la chai huko karibu na Matunda (uk.32). Mbali na kiongozi huyu, tunaelezwa kuhusu Chifu Kifuja aliyekuwa na mashamba matatu yenye thamani kubwa. Shamba moja liliitwa LT 120 kutoka Nyakua Area lenye thamani ya shilingi milioni themanini. La pili liliitwa LT 133 kutoka Laghai Area na lenye thamani ya shilingi milioni mia tatu sitini. La tatu liliitwa LT 146 kutoka Lenu Area na lenye thamani ya shilingi milioni sabini (uk.63). Umilisi wa ardhi jinsi hii ni suala linaloudhi na kutamausha wasiokuwa na uwezo wa kiuchumi au kisiasa katika jamii nyingi hasa barani Afrika. Hata tunaposafiri kutoka sehemu moja ya nchi kwenda nyingine, hatukosi kupitia ardhi kubwa isiyostawishwa au iliyostawishwa ambayo aghalabu huwa ni ya mtu au watu fulani maarufu kisiasa au kiuchumi. Vilevile, ni uhalisia kwamba hatukosi kupitia vijiji ambamo watu wanaishi kama maskwota kwa msongamano mkubwa.

Mbali na kumiliki mashamba makubwa, Chifu Kifuja alikuwa amewekeza katika Wahote Banking Corp kwa kununua robo tatu ya hisa katika shirika hilo. Kama ardhi, umilisi wa mashirika kama haya na wachache katika uzalishaji mali huwa na nafasi kubwa ya kudhibiti mfumo wa ubepari na kuendeleza matabaka katika jamii. Ubinafsi huu wa Chifu Kifuja unamaanisha kwamba ni robo moja tu ya hisa inayobaki kwa wengine.Tetesi zilisema kuwa Kifuja aliwahi kununua mabasi yaliyoabiri katika mji mkuu ingawa usafiri ulionyesha jina la mpwa wake, Albin Kifuja huku mkurugenzi wa pili akiwa Mayowe (uk.64). Kwa kuwahusisha mpwaye na Mayowe (rafikiye na mfanyibiashara mwenza), ni maoni yetu kwamba Chifu Kifuja alikuwa akiuficha upendeleo na ukiritimba wake. Kama inavyoelezwa katika u-Marx wa kirasimi, hali hii inaonyesha jinsi mali katika Mabonde inavyomilikiwa na idadi ndogo ya watu katika mfumo wa ubepari. Mashamba ya Kifuja yamo katika maeneo ambayo yamepewa majina ya kimajazi yanayoashiria unyanyasaji wa tabaka la wanyonge kama unavyoendelezwa na walio mamlakani. Kwa hivyo, hatuoni kama unyakuzi wa ardhi uliendelezwa katika maeneo ambayo majina yao halisi ni hayo yaliyotajwa. Majina haya (Nyakua Area, Laghai Area na Lenu Area) ni kejeli ya wenye nguvu kwa wanyonge na yanaeleza namna ambayo kwayo mashamba hayo yalimilikiwa — kwa njia zisizokuwa za haki. Japo umilisi kama huu ni tatizo ambalo tunaweza

kujitambulisha nalo katika jamii ya sasa, matumizi ya majazi ni mbinu ya ubunifu ambayo inaweza kuikosesha fasihi sifa ya mwigo wa mazingira halisi katika jamii.

Kwa upande mwingine, Chebaskwony (Chifu aliyemtangulia Kifuja) alikuwa tajiri mkubwa hivi kwamba hata kifo alikiogopa kutokana na utajiri wake. Tunaarifiwa kwamba aliendesha mradi wa maji uliomletea pesa si haba. Aidha, alimiliki majosho mengi. Japo Chebaskwony alikuwa na biashara hizi nyingi na kwamba aliwahi kumiliki Mabonde kwa miaka mingi, tamaa ya mali ilimfanya auze hata sukumawiki, mahindi choma na mbuzi sokoni katika minada mbalimbali (uk.61). Yaani, Chebaskwony alikuwa mmojawapo wa wachache waliomiliki njia kuu za uzalishaji mali huku pia akijishughulisha na biashara zilizofanywa na kina yahe. Tetesi zilisema kwamba alikuwa na nyumba za kukodisha katika mataifa ya kigeni. Pia, ilisemekana kwamba yeye na Kifuja walikuwa na biashara tele zilizowaletea pesa nyingi. Tajiri mwingine alikuwa Dkt Balaa. Yeye pamoja na Kifuja, Mayowe na Angusha, walimiliki Shirika la Maba ambalo ndilo lililokuwa shirika kubwa sana la bima nchini. Aidha, alikuwa na maduka kochokocho ya kuuza dawa pamoja na kiliniki kemkem. Mhusika huyu amesawiriwa kiuhalisia maadamu umilisi wa kiliniki na maduka ya kuuza dawa ni jambo la kawaida kwa madaktari katika enzi hizi hivi kwamba hata wagonjwa wanapokosa huduma za kiafya katika vituo vya kiafya vya serikali hujikuta mara kwa mara wameelekezwa kwenye kiliniki na maduka kama haya ya watu binafsi.

Fauka ya hayo, maudhui ya umaskini na utajiri yanadhihirika kupitia nafasi za elimu shuleni. Katika riwaya ya *Yasinya*, tunaelezwa kwamba eneo alikoishi Asisi (mwakilishi wa tabaka la maskini) lilikuwa na idadi kubwa ya watoto lakini shule zilikuwa chache sana. Zile zilizokuwapo zilikuwa na wanafunzi wengi mno huku walimu wakiwa wachache. Hali hii inaonyesha wazi kwamba eneo hili la walalahoi lilitengwa katika maendeleo ya kielimu. Hii ndiyo hali iliyomfanya Chifu Kifuja kusajili mwanawe kusomea uchoraji katika chuo kilichokuwa karibu na mtaa wa wakwasi (uk.48).

Katika Mabonde, nafasi za elimu katika shule za umma ni za wale wasiojiweza kiuchumi. Walio na uwezo wa kiuchumi hupeleka watoto wao katika shule za kibinafsi. Hii ndiyo hali halisi katika jamii nyingi. Tunaona tofauti hizi za kiuchumi baina ya matabaka tunapochunguza yaliyojiri kwa Kijasiri alipokwenda kumtafutia mwanawe Tumaini nafasi ya kuanza masomo katika shule ya msingi. Kwanza, Kijasiri alitafuta nafasi katika shule ya Msigulu — shule ya umma au iliyomilikiwa na serikali. Kulikuwa na vitu vichache ambavyo Kijasiri alihitajika kununua ili mwanawe apate nafasi katika shule hii. Mojawapo ya vitu hivi ni sare kamili ya shule. Hata hivyo, elimu katika Mabonde ilikuwa ya bure. Ijapokuwa ilikuwa lazima kwa

wanafunzi kuwa na sare ya shule, Kijasiri aliwaona watoto ambao hawakuwa nayo. Hedimasta wa shule hiyo alimwambia Kijasiri kuwa watoto hao walitoka Magengeni na kwamba wazazi wao hawakuwa na uwezo. Ni wazi kwamba hedimasta alitambua kuwa waliotoka Magengeni hawakuwa na uwezo mkubwa wa kiuchumi. Waliwakilisha tabaka la chini katika jamii ya Wamabonde.

Baada ya kunyimwa nafasi katika shule ya umma, Kijasiri alienda kubahatisha katika shule ya kibinafsi iliyokuwa jirani na shule ya Msigulu. Mara tu alipofika katika lango la shule, bawabu alimuuliza Kijasiri iwapo angeweza kulipa karo ya shule hiyo. Aliendelea kusema kwamba watoto waliosomea shule hiyo walipelekwa humo na kuchukuliwa kwa magari. Hakukuwa na waliotembea. Maneno ya bawabu huyo yanaonyesha wazi kwamba alitambua kuweko kwa matabaka ya walalahoi na walalaheri katika jamii. Alitambua pia kwamba kuna shule za waliojimudu na wasiojimudu kiuchumi. Bila shaka, bawabu aliutambua uwezo wa chini wa Kijasiri kiuchumi. Alipofika mapokezini, Kijasiri alipewa fomu iliyoonyesha karo ya shule hiyo ya kibinafsi. Alishangaa kwamba karo ya muhula mmoja, ambayo angemlipia bintiye katika shule hiyo, ilikuwa sawa na karo yake aliyolipa kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne (uk.112-114). Tunaposoma yaliyojiri kwa mhusika huyu, tunahisi kutamauka kwake kutokana na hali yake duni kiuchumi.

Riwaya ya *Yasinya* inatueleza kuhusu familia ya Kikwasi iliyokuwa ya matajiri. Katika familia hii, kulikuwa na mtoto (mwana wa Kikwasi) aliyeitwa Anao. Tunafahamishwa kwamba japo alitoka katika tabaka la matajiri, Anao aliishi maisha ya kawaida (kama tu maskini) — akawa amejitenga na tabaka lake la walalaheri. Kujitenga huku ni dhahiri maadamu marafiki zake wote waliishi Umachocholeni (kwa tabaka la maskini). Utotoni mwake, Anao alitangamana na hao marafiki bila kuona tofauti kati yake na wao. Msimulizi anamtaja Anao kama mtu aliyekuwa ishara ya tumaini kwa maskini. Kudhihirisha sifa hii, tunafahamishwa kwamba Anao hakukubali kutengwa na wanadamu wenzake na wala hakuyaunga mkono maonevu yoyote kwa binadamu. Hulka yake ya kutotaka kutengwa na binadamu wenzake (hususan maskini) pia inasisitizwa na maamuzi yake kukataa kusomea katika shule ya kibinafsi iliyokuwa karibu na nyumbani kwao na badala yake akapendelea kusomea shule ya Kinani Belsa walikosomea watoto kutoka familia maskini. Kama tuonaovyo katika jamii, watoto wengi kutoka familia zenye uwezo wa kiuchumi hupelekwa shuleni na pia huchukuliwa humo kwa magari ya kifahari. Alipokuwa anajiunga na shule, Anao alizikataa starehe hizi. Badala yake aliamua kuelekea shuleni kwa mguu huku akiwa ameshikwa mkono na yaya. Alipofika darasa la kwanza, Anao aliukataa msaada huu wa yaya na

wala hakukubali mtu yeyote kumpeleka. Badala yake, alikimbia kutoka nyumbani na kusimama njiani ambapo alijiunga na watoto wenzake wakatembea hadi shuleni pamoja.

Tukirejelea wanavyosema Marx na Engels katika Wamitila (2002:183) kwamba kitu cha kimsingi katika maisha ya binadamu ni kula, kunywa, kupata malazi, mavazi na mambo mengine, ni muhimu kuangazia vyakula vilivyoliwa na kubainisha matabaka mbalimbali. Kulingana na uwezo wao wa kiuchumi, matabaka hutegemea vyakula vya aina zinazotofautiana. Kwa mfano, tabaka la matajiri aghalabu hutegemea mapochopocho na vyakula ambavyo maskini hawawezi kupata maadamu ni vya kununuliwa. Mara nyingi, tabaka la watu maskini hutegemea vyakula ambavyo vimetoka shambani moja kwa moja bila kupitia viwandani. Haya yanaelezwa kupitia kwa wahusika Sifichi kutoka tabaka la maskini na Anao kutoka tabaka la matajiri. Katika*Yasiny*a, Sifichi alichekwa na watu siku ya wazazi ambapo mamaye alimtembelea shuleni na vyakula kama buyu la maziwa, viazi vitamu na *nduma* badala ya asali, siagi, biskuti na *weetabix* (uk.142). Ni wazi kwamba asali, siagi, biskuti na *weetabix* ni vyakula vilivyowatambulisha wanafunzi kutoka familia zenye uwezo wa kiuchumi huku maziwa, viazi vitamu na *nduma* vikiwatambulisha waliotoka katika familia maskini.

Kwa upande mwingine, tunajulishwa kwambafamilia ya Anao ilikuwa na uwezo wa kumlisha kwa vyakula vilivyolingana na tabaka alimotoka lakini kijana huyo (Anao) hakujitambulisha shuleni kwa vyakula vya sampuli hii. Akiwa na Asisi shuleni, walikula muwa na mahindi choma. Katu, hakubeba mkate, siagi, kuku na maziwa — vyakula ambavyo kwa mujibu wa walimu wake, viliwatambulisha watoto kutoka familia za matajiri. Hii ni sifa iliyowashangaza walimu wake.

Kulingana na maelezo ambayo tumetoa kumhusu Anao, ni dhahiri kwamba familia yake ilijua nafasi ya mwanao katika jamii kiuchumi hivi kwamba kiuhalisia, matendo ya wanafamilia yanasukumwa na hali yao ya kiuchumi. Kwa mfano, wazazi wa Anao walielewa fika kwamba mwanao hakustahili kusomea shule ya watu wa kawaida kama Kinani Belsa. Kwa sababu hii, walipendelea kumpeleka katika shule ya kibinafsi. Aidha, walijua kwamba alistahili kupelekwa kwa gari hadi shuleni. Kuweko kwa yaya wa kumsindikiza Anao shuleni ni ishara ya uwezo wa kiuchumi wa familia ya mtoto huyu. Walimu katika shule ya Kinani Belsa walimtarajia Anao kubeba vyakula vya aina fulani kulingana na tabaka alilotoka. Walistaajabishwa na bidii yake na sifa zingine alizoeneza katika mahusiano yake na wenzake. Mbali na bidii, walimu walitambua kwamba Anao alikuwa mtiifu, mwenye heshima na mpole. Mshangao wa walimu wa Anao kuhusu hulka yake unaonyesha kwamba kuna hulka hasi wamezoea kuona ikiwatambulisha

watoto kutoka tabaka lenye nguvu za kiuchumi. Mwenendo huu wa Anao wa kujitenga na tabaka la matajiri huku akijiunga na tabaka la maskini ulimuudhi baba yake (Kikwasi). Kulingana na Kikwasi, “huo ulikuwa ni usaliti, udunishaji na upofu ambao haukumstahili mtu mstaarabu”.

Lugha anayotumia Kikwasi kuhusu tabia ya mwanawe inautambulisha mtazamo wenye kiburi wa walio katika tabaka la juu kiuchumi. Wanajiita wastaarabu kumaanisha kwamba wao ni bora kuliko wanajamii walio maskini. Tunapoyachunguza maneno ya Kikwasi, hatukosi kujiuliza iwapo kuwa tajiri ndiko hasa kuwa mtu mstaarabu. Ni ajabu kwamba mwenendo wa Anao ambao mtu razini atauona kuwa mzuri unawafanya baadhi ya watu walioshikilia imani za kishirikina kuona kwamba Anao hangeweza kujitambua eti kwa sababu alirogwa na kufanywa zuge (uk.81-83).Ni maoni yetu kwamba wanaosema kuwa Anao alirogwa wamo katika tabaka la matajiri. Nafasi za elimu shuleni ni suala linaloendeleza maudhui ya umaskini na utajiri ambapo fasihi inahusishwa na shughuli halisi za kibinadamu na hivyo basi kutotengwa na mazingira yanayoizaa kama inavyostahili katika uhakiki wa ki-Marx. Suala hili linaingiliana vizuri na haipothesia yetu kwamba maudhui katika *Yasinya* na *Mwanasiasa* ni ya kihalisia na yanahusiana pakubwa na mgawanyiko wa jamii kitabaka.

Ili kuusawiri uhalisia katika uhakiki unaoegemea u-Marx wa kirasimi, maisha ya binadamu huelezewa zaidi kama uhalisi unaoonekana kama vile mazingira ya kuishi kuliko mawazo. Katika riwaya tunazozihakiki, maudhui ya umaskini na utajiri pia yanawasilishwa kupitia mazingira ya aina hiyo. Kwa mfano, riwaya ya *Yasinya* inadhihirisha kwamba mazingira wanamoishi wanadamu katika maeneo tofauti ya Mabonde yanaakisi hali halisi ya kuweko kwa matabaka katika jamii. Tabaka la maskini liliishi katika mitaa duni kama vile Kabisuswa, Magengeni, Umachocholeni na Changu Kidogo — mitaa ya mabanda iliyojengwa kwa namna ya kusikitisha. Kwa mfano, mtaa wa Changu Kidogo ulijengwa kwa mabati makuukuu na masalio ya maboksi. Hakukuwa na njia nzuri za kufika makazi haya. Isitoshe, kulikosekana hospitali na shule za kuwafunzia madaktari. Ili kutafuta matibabu, ilibidi wenyeji watembelee zahanati zilizokuwa mbali na ambazo hazikuwafaa sana kwa vile zilikosa dawa. Kulikuwa na maji ya rangi ya kijani na mengine ya rangi ya mchanga. Tunayaelewa haya kama maji yaliyotuama mahali fulani baada ya mvua kunyesha. Hii ni taswira halisi inayopatikana katika sehemu nyingi za nchi mbalimbali. Aghalabu, mabomba yaliyobeba maji taka na kupitia mbele na chini ya nyumba zilizokuwamo katika makazi haya yalivuja na kuongeza uchafu zaidi kwa maji yaliyotegemewa. Tunaarifiwa kwamba wakazi wa maeneo ya maskini wa Mabonde waliyatumia maji haya katika shughuli zote za nyumbani —kuosha mboga, kupika, kunywa na kufua nguo.

Ni jambo lililowakera wakazi wa humu kwamba japo Mabonde ilikuwa na mito yenye maji safi, utawala wa Chifu Kifuja haukuwa umestawisha maeneo walikoishi maskini kwa kuweka maji safi ya mabomba. Kwa kukosa taa za umeme, tunaarifiwa kwamba wakazi wa maeneo haya walipata mwanga kutoka kwa vibatari au masalio ya mihindi iliyowashwa (uk.91). Kadhalika, uchafu mwingi ulioenea kote ni taswira halisi inayotambulisha makazi haya ya walalahoi.

Kwa mujibu wa nadharia ya u-Marx wa kirasimi, ni muhimu kuchunguza shughuli za kibinadamu zilizoendelea katika makazi ya matabaka yaliyomo katika jamii. Katika maeneo walikoishi maskini, kulikuwa na makanisa, waombaji na waganga wengi. Aidha, huku ndiko walikojificha majambazi. Wakazi wa maeneo haya walilaghaiwa na waganga waliotoka Bongo kwa madai ya kuwa na uwezo wa kutibu magonjwa yanayoonekana kuwa sugu kama vile ukimwi, kichaa, uchawi na utasa. Waganga hawa walidai pia kwamba hirizi zao zingewaletea watu bahati, kudhibiti uongozi na mapenzi, kuvutia utajiri, kumwepusha mtu na macho mabaya pamoja na kumpa amani na utulivu wa moyoni. Shughuli za waganga zilizoendelezwa huku kama vile kuvutia utajiri na bahati zinalenga kumhadaa maskini aone uwezo wa kuinuliwa kwake kiuchumi. Makanisha yaliyojengwa mbele ya mabanda yalitumiwa na wakazi maskini kuzinywea pombe za kienyeji na vinywaji vingine ambavyo vingewawezesha kuyasahau matatizo waliyokuwa nayo katika ulimwengu ambao ulionekana kuwachukia maskini. Makazi mengine yanayolisawiri tabaka la maskini ni makao ya watoto machokora kwa pasta alipokimbilia Kijasiri baada ya kukejeliwa na kunyimwa malazi na binamuye pamoja na amiye Amte (uk.117).

Katika kulisawiri tabaka la matajiri, msimulizi anatuchorea picha halisi ya makazi yaliyokuwa katika ujirani wa Kibisuswa, upande wa ng'ambo ya barabara. Taswira hii ni tofauti kabisa na ile inayopatikana katika makazi ya tabaka la maskini. Tunaelezwa kwamba huku kulikuwa na majumba makubwa yenye mapaa ya vigae, kuta za mawe, maji safi ya mabomba, vyoo vya kurashia maji na taa za umeme. Makazi haya yalikuwa mitaa ya kifahari kulikoishi matajiri. Mfano mzuri wa mitaa hii ni Bwanyenye alikoishi Deni. Huku hakukuwa na waganga. Badala yake kulikuwa na hospitali kwenye majumba marefu. Aidha, hakukuwa na makanisa. Badala yake kulikuwa na majumba ya mabenki na magari ya makampuni ya ulinzi (uk.53-54). Ni muhimu kujiuliza hapa sababu ya kukosekana kwa makanisa katika makazi ya walalaheri huku mengi yakipatikana katika makazi ya walalahoi. Jibu la swali hili limo katika maudhui yanayoeleza nafasi ya dini katika mfumo wa kitabaka.

Katika riwaya ya *Mwanasiasa*, sehemu ya Bondeni ya viamboni kuliishi wachochole. Huku kulikuwa na mitaa kama Mwembe legeza, Tuwa Tugawe na Shika Adabu. Ili kuwasilisha maudhui kihalisia, kuna urejelezi wa mandhari kiwakati katika historia ya jamii ambapo Mwembe legeza na Shika Adabu ni majina yanayohusiana na kutamauka kwa Wanabonde na adhabu kali kwa wazinifu na wadokozi wa mali za watu mtawalia. Historia ya mitaa hii haionyeshi maendeleo yoyote ya kiuchumi. Taswira tunayochorewa katika makazi haya ni ya vitongoji duni vilivyokuwa pembeni mwa majumba ya kifahari ya matajiri yaliyojengwa katika ardhi ambayo ilikuwa imenyakuliwa kwa hila kutoka kwa wachochole. Nyumba nyingi zilizokuwa humu zilikuwa na kuta za mbavu za mbwa zilizoshikiliwa kwa michegamo nusura ziporomoke. Kuta hizo zilikuwa na udongo wenye matundu yaliyomwezesha aliyekuwa nje kuona ndani. Aidha, aliyekuwa ndani angeweza kuona kwa urahisi yaliyotendeka nje. Mapaa ya nyumba hizi yaliezekwa makuti au vipande vya mabati ya madebe na mikebe iliyookotwa kwenye vifusi baada ya kutupwa na mabwanyenye walioishi Bondeni mpya. Mabwanyenye walivitupa vifaa hivi baada ya kutumia mafuta yaliyokuwamo.

Mbali na madebe na mikebe, kina yahe wa viamboni waliokota bilauri zilizovunjika, vigae vya sahani za kauri, chupa tupu za vileo ghali na kadhalika. Vifaa hivi vilikuwa muhimu kwao. Hata hivyo, baadhi yao walijikuta wamekatwa na vigae vya chupa vilivyowaambukiza maradhi ya pepopunda. Wengine waliugua vidondandugu. Hakukuwa na hospitali wala zahanati. Kwa sababu hii, maambukizi hayo yalisababisha vifo kutokana na ukosefu wa huduma za matibabu (uk.5). Ilibidi wagonjwa na mama wazito watembee hadi Bondeni mpya kutafuta huduma za kiafya. Aidha, kulikuwa na ukosefu wa maji hivi kwamba akina mama walitembea masafa marefu kuyatafuta. Wakati mwingine, maji taka yaliyochanganyika na kinyesi, yaliyoenea kila mahali na kutoa uvundo uliochukiza; yalitumiwa kuogea, kufulia nguo, kunywesha mifugo, kupikia na hata kunywa. Vyoo humu vilikuwa haba. Aghalabu, wenyeji walikwenda haja pembeni mwa kuta za vijibanda vyao, kwenye vifusi vilivyokuwa kila mahali au kwenye kwekwe zilizoenea. Kwekwe hizo zilikuwa maficho ya mbu hivi kwamba ugonjwa wa malaria ulikuwa tisho kwa maisha yao daima. Barabara nazo zilikuwa mbovu. Hakukuwa na baraste isipokuwa vichochoro na njia ambazo zilikuwa na mwisho wa ghafla (uk. 6). Tunajulishwa kwamba watu wengi walisafiri kwa miguu huku mbinu za uchukuzi zikihusu machela, gari la punda, rukwama au kubebwa mgongoni na mtu.

Baada ya kustawishwa kwa ardhi iliyonyakuliwa na mabwanyenye kutoka kwa wachochole, ungeweza kupotea ulipokuwa ukipita katika viambo vya Shika Adabu kwani ungekutana na

majumba ya kupendeza na vichochoro vilivyokuwepo zamani vikiwa ni baraste kubwa zilizoweza kupitisha motokaa (uk.104-105). Ustawishaji huo ndio ulioibua makazi ya Bondeni Mpya walikoishi matajiri. Huku kulikuwa na mitaa kama Maweni, Kwa Shibu na Mwananyamala. Mabwanyenye walijitenga kutoka kwa wachochole kwa kujenga kuta ndefu zilizowazuia wachochole hata kuchungulia ndani. Kama ilivyo katika mitaa ya viamboni, majina ya mitaa hii yanahusiana na matukio ya kihistoria.Mtaa wa Maweni ni jina lililotokana na kuta za nyumba nyingi zilizojengwa kwa tofali za kuchomwa au kutomelewa kwa mawe ya pwani. Katika mtaa huu, kulikuwa na hospitali kubwa tofauti na viamboni ambako hakukuwa na hata zahanati (uk.32). Mandhari haya yametumika kuonyesha kwamba walioishi humu walikuwa watu wa tabaka la walalaheri.

Mtaa wa Kwa Shibu ni jina lililotokana na tajiri mmoja aliyeitwa Bwana Shibu. Tajiri huyu alimiliki kiunga kikubwa cha mikomamanga, mizabibu na maduka kadha ya kuuza vitu vya rejareja. Alikuwa kabaila. Alimiliki ardhi kubwa alizokodisha ambapo alizitoza kodi walimaji waliopanga. Aliitoa kodi hiyo hiyo kama sadaka kwa wahitaji (uk.13). Watu walitafuta vibarua kwake. Kihistoria, mandhari haya yanatumiwa kuisawiri jamii kitabaka ambapo Bwana Shibu anayehusishwa na jina la mtaa huu aliwakilisha tabaka la mabwanyenye huku aliyewakodisha ardhi na kuwapa vibarua wakiwakilisha tabaka la makabwela. Katika jamii ya sasa inayowakilishwa katika *Mwanasiasa*, mandhari ya mtaa huu pia yanatumiwa kuisawiri jamii kitabaka. Msimulizi anatufahamisha kwamba kulikuwa na maduka makubwa yenye bidhaa mbalimbali. Kulikuwa na mafundi hodari wa kushona kwa cherahani walioishi viamboni kwa wachochole japo wao walivalia midabwada — mavazi yaliyotambulisha tabaka lao (uk.14). Kulikuwa na maseremala waliowatengenezea wakazi vitanda vya samadari ilhali wao walilalia vitanda vya mwakisu au kumba. Aidha, kulikuwa na maduka makubwa makubwa ya masonara, vyakula, majora ya nguo za hariri na kila aina ya vitu vya tunu (uk.13-14). Mandhari haya yanaonyesha jinsi mabwanyenye walioishi humu walivyomiliki njia kuu za kuzalisha mali Bondeni.

Kama ilivyokuwa mitaa ya Maweni na Kwa Shibu, Mwananyamala ulikuwa mtaa wa kifahari. Tunajulishwa kwamba kulikuwa na utulivu mkubwa uliopatikana usiku na mchana. Jina la mtaa huu limo katika mojawapo ya masimulizi ya jamii ya Bondeni ambapo utulivu unaotajwa ndio asili ya jina 'Mwananyamala' kutokana na uchukulio wa wanajamii kwamba, iwapo mwana mchanga angelia humo, angezua bughudha kubwa kwa wakaaji wake ambao msimulizi anawaita 'wenyenchi'— watu waliokuwa na nafasi zao katika jamii. Utulivu huo ulitokana na kuwepo

kwa korija za miti iliyotamalaki kila mahali, baraste pana na zilizotakata. Aidha, kulikuwa na vitalu vya asmini na vilua vilivyonawiri katika kila uso wa nyumba huku vikivutia na kutoa harufu nzuri kwa mabwanyenye. Tofauti na viamboni, mtaa huu ulikuwa na hospitali ya kujifungulia akina mama. Walioishi viamboni walikwenda Mwananyamala kutafuta riziki. Kazi walizozipata ni zile duni: uyaya, uboi au ulinzi kwa ujira mdogo. Waliopata ajira waliyavumilia matusi na masimango kutoka kwa mabwana wenye nyumba au wake zao na watoto (uk. 82). Hawakuwa na budi kuvumilia dhuluma hizo ili wapate riziki. Hivyo ndivyo wanyonge wanavyodhulumiwa katika mfumo wa kitabaka. Umuhimu wao huonekana tu wanapotoa huduma kuwaendeleza mabwana zao kiuchumi. Katika hali hii, wanatumiwa kama bidhaa.

Mgawanyiko wa jamii kitabaka pia unaonekana kupitia kwa makazi ya Bambua na Bwana Mkubwa. Bambua anayewakilisha tabaka la maskini wa Bondeni aliishi kwenye kijumba cha msonge kilichokandikwa kwa udongo mwekundu na kuezekwa kwa nyasi. Kijumba hiki kilikuwa na mlango wa kumba za makuti ya mnazi (uk.4). Mlango huo haukuwa na hata tumbuu (uk.54). Kitanda cha Bambua kilikuwa mkeka. Tofauti kabisa na makazi haya, Bwana Mkubwa (kiongozi na mwakilishi wa tabaka la matajiri), aliishi katika kasri. Kasri hilo lilikuwa na milango iliyotiwa nakshi. Vyumba vyake vilikuwa na mapankaboi yaliyopepea juu ya dari zuri. Aidha, kulikuwa na arshi za dhahabu, vitanda vya samadari na mavono manene yaliyokuwa yakimpa usingizi mwanana huku maelfu ya Wanabonde waliokuwa masikini wakilalia virago. Kulikuwa na masanduku yaliyokuwa yamejaa nguo furifuri kama vile majoho, kanzu za kila aina, makoti na sahari alizokuwa akibadilisha kila uchao huku Wanabonde maskini wakiishia kuvaa midabwada (uk.122).

Ni dhahiri kwamba makazi ya wanajamii yametumika kikamilifu kuelezea tofauti za kitabaka baina ya maskini na matajiri katika mji wa Bondeni — mji uliogawika katika tabaka la Wananchi (maskini walioishi viamboni) na tabaka la Wenyenchi (matajiri walioishi Bondeni mpya)-uk.4. Ingawa kwa kiasi kikubwa majina ya kimajazi yametumiwa kuibuni mitaa ya kifahari na ile ya viamboni, kuna chembechembe za uhalisia kwani tunaweza kutambua mitaa kama hiyo katika jamii za kisasa. Kuna mitaa ya kifahari kunakokaa watu walio na nafasi zao huku pia kukiwa na mitaa duni kunakokaa masikini. Ni mandhari yanayoakisi uhalisi unaoonekana.

Umaskini katika jamii unasawiriwa kupitia namna ya kujikimu maishani kwa tabaka la wachochole. Katika riwaya ya *Yasinya*, tunaarifiwa kwamba tabaka la chini linajikimu maishani kwa kujihusisha na biashara ndogondogo. Chumo la baadhi ya wanajamii lilikuwa kukamua

kangara na kuichemsha usiku. Katika soko la maeneo alikotoka Asisi, biashara duni ziliendelezwa. Kwa mfano, kulikuwa na uuzaji wa uji au chai kwa viazi, kuku na mayai, soksi na viatu, dawa za kienyeji ndani ya chupa au mikebe mbalimbali na uchuuzi wa njugu, vitambaa vya kupenga pua, ugoro na tambuu (uk.50-51). Biashara za aina hii hazikuwa na uwezo mkubwa wa kuwainua wanajamii kiuchumi.

Aisha (rafikiye Kipokeo), alipata kipato chake kwa kupika na kuuza chang'aa. Usiku, alifanya uasherati ama 'biashara ya Sigalame' kama wenyeji walivyozoea kusema. Kutokana na umaskini, Aisha alisikitika kwamba hakuwa na namna nyingine ya kujikimu katika maisha. Kila uchao, aliamkia njaa huku mahitaji yakiwa kochokocho. Alijihurumia kwamba hakuwa afisa. Alisema kwamba maafisa walichota pesa bila kujua zilitoka wapi (uk.45-47). Kwa hivyo, hali ya kiuchumi ya maafisa wanaotajwa hapa ni tofauti na ile ya Aisha. Maafisa wamo katika tabaka la waliojiweza kiuchumi huku Aisha akiwa katika tabaka la wenye uhitaji mkubwa.

Uchanganuzi wa maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka kupitia suala la utajiri na umaskini umefanywa kwa kueleza dhamira za waandishi wa riwaya husika pamoja na masuala mengine yanayojikita katika nadharia ya u-Marx wa kirasimi. Masuala hayo ni kama vile umilisi wa rasilimali muhimu za kujiendeleza kiuchumi. Mfano wa rasilimali hizo ni ardhi, mashirika, na maduka ya kufanyia biashara. Umilisi huo unaonekana ukiibua matabaka katika jamii kwa vile mali inamilikiwa na idadi ndogo ya watu. Aidha, tumechunguza na kueleza kuhusu makaziya watu huku tukiyatambua kama mandhari muhimu ya kuakisi uhalisia unaoonekana. Masuala mengine ambayo tumeshughulikia kwa misingi ya nadharia husika ni nafasi za elimu shuleni, shughuli za kibinadamu na vyakula vya matabaka mbalimbali.

Katika kushughulikia suala la umaskini na utajiri, ni muhimu kuzama zaidi katika kuchunguza jinsi baadhi ya wanajamii wanavyopata utajiri wao huku wengine wakiishia kuwa maskini. Hivi ni kutokana na yanayosemwa na waasisi wa nadharia ya u-Marx wa kirasimi kwamba, katika maendeleo ya mfumo wa ubepari na ongezeko la uzalishaji mali, kuna namna ambazo kwazo baadhi ya watu hufaidika kwa njia zisizo za haki na hivyo basi kuimarisha matabaka yaliyomo katika jamii. Njia mojawapo katika riwaya ya *Mwanasiasa* ni kupitia unyonyaji wa wafanyikazi. Katika riwaya hii, tunajulishwa kwamba wanajamii maskini wa Bondeni waliwafanyia kazi matajiri huku wakipewa ujira mdogo. Isitoshe, ilikuwa vigumu kwa wafanyikazi hao kuipata mishahara hiyo duni kwa vile waajiri walilipa kwa kujilazimisha (uk.82). Huo ni ujanja au upunjaji na ndivyo inavyokuwa katika mfumo wa ubepari ambapo mfanyikazi hulipwa ujira ulio mdogo ili kuwezesha kupatikana kwa faida kubwa katika uwekezaji wa mabepari. Aidha, waajiri

hawakujali utu na masaibu yaliyowakumba wafanyikazi wao. Kwa mfano, tunaelezwa kuhusu Mwakinago aliyekuwa mwashi na hodari kwenye uchimbaji wa mashimo na vyoo. Mhusika huyu alianguka na kuvunjika uti wa mgongo alipokuwa akifanya kazi kwa tajiri mmoja katika mtaa wa kifahari wa Kwa Shibu. Mwajiri wake alihakikisha kwamba Mwakinago hakulipwa fidia. Mwakinago alipomshtaki mwajiri wake, kesi ilicheleweshwa.

Kucheleweshwa kwa kesi hapa kunaonyesha jinsi mfumo wa ubepari unavyotumia mahakama kulinda mali ya matajiri wanaomiliki njia kuu za uzalishaji mali. Baada ya kulazwa hospitalini kwa muda mrefu, Mwakinago alihitajika kulipa deni kubwa la hospitali. Mwajiri wake hakumsaidia katika ulipaji wa deni hilo. Baadaye, Mwakinago alikufa lakini mwajiri wake hakuhudhuria matanga wala kutoa mchango wa fedha kwa matayarisho ya mazishi (uk.84-85). Kama u-Marx wa kirasimi unavyoeleza katika dhana ya ubidhaaishaji, umuhimu wa watumishi hao kwa mabwanyenye unaonekana wakati wanapowazalishia mali tu. Tuliyoyaeleza kuhusu Mwakinago ni mfano wa ubidhaaishaji ambapo wafanyikazi wanatumika kama bidhaa.

Kutokana na pupa ya mali ya mabwanyenye katika riwaya ya *Mwanasiasa*, wanabiashara walafi wa tabaka la matajiri walijiendeleza kwa njia zisizo za haki kwa kuhodhi bidhaa muhimu kwa lengo la kusababisha upungufu usiokuwepo ili wapate nafasi ya kuongeza bei (uk.84). Aidha, wafanyibiashara walioweza kuuza bidhaa kwa wingi ndani na hata ughaibuni, walinunua bidhaa mbalimbali kutoka kwa wakulima wa Bondeni kwa bei hafifu na kuziuza bidhaa zizo hizo kwa bei ambayo wachochole wengi hawangeweza kuimudu. Katika hali hii, wanaotoa nguvukazi (Wanabonde maskini) wanazidi kudidimia kiuchumi huku mahitaji yao yote yakiwa yamedhibitiwa na tabaka la mabwanyenye (uk.83).

Kwa mujibu wa u-Marx wa kirasimi, umilisi na utumiaji wa ardhi ni mojawapo ya njia kuu za uzalishaji mali katika mfumo wa kibepari. Katika riwaya ya *Mwanasiasa*, unyakuzi wa ardhi ni njia nyingine isiyo haki ambayo kwayo baadhi ya wanajamii wanajiendeleza kiuchumi. Katika riwaya hii, tabaka la mabwanyenye na wote waliokuwa na uwezo wa kisiasa, wa jadi au wa kidini walitumia nyadhifa zao kujilimbikizia mali. Walinyakua ardhi kwa kuwafurusha Wanabonde wachochole kutoka ardhi yao na kujenga nyumba kubwa. Maovu hayo yalifanywa bila wenyeji kupewa ilani wala kutafutiwa mahala badala pa kuishi. Nyumba zao nyingi zilivunjwa na wakaishia kuwa maskwota. Kila walipokabiliwa na dhuluma hizi, wakaazi walijaribu kuzipinga lakini hawakufanikiwa madhali askari waliojihami walikuwa chonjo kuzuia purukushani yoyote ambayo ingetokea (uk. 103). Aidha, unyakuzi huu uliwezesha mabwanyenye walioishi katika maeneo ya Bondeni mpya kuwa wamilisi wa mashamba makubwa ya kulima

hivi kwamba hata hawakujua yaliyokuwamo mashamba hayo. Hali kama hiyo inapatikana katika jamii nyingi hususan barani Afrika. Ni hali ambayo imesababisha mivutano ya kitabaka na hivyo basi kuthibitisha yaliyosemwa na Marx kwamba kile kinachotawala maudhui ya historia ya binadamu ni migongano na mivutano hiyo ambayo huletwa na hali za kiuchumi na kisiasa. Mfano mzuri wa mivutano hii ni kwamba njaa inayowakumba Wanabonde wa viamboni inawafanya baadhi yao kuchuma matunda kwenye mashamba ya mabwanyenye walioishi katika maeneo ya Bondeni Mpya. Katika msimu wa matunda, Wanabonde wengi wangeshikwa na kushtakiwa na mabwana shamba kwa kuingia bila ruhusa kwenye mashamba hayo.

Suala la sheria ni miongoni mwa masuala ya kijamii yanayohusishwa na u-Marx wa kirasimi. Katika jamii inayotawaliwa na mfumo wa ubepari, sheria hutumiwa kulinda mali ya tabaka lililo mamlakani na kukandamiza tabaka la walio wanyonge kiuchumi. Katika riwaya ya *Mwanasiasa*, sheria za uvuvi zilitumika kuwanyima haki Wanabonde wachochole. Utawala wa Bwana Mkubwa uliwazuia wachochole kuvua samaki katika maeneo yaliyokuwa na majimakuu au maji ya kina kirefu. Ulifanya hivyo kwa kuyazingira na kuyaweka maji hayo chini ya hifadhi ya dola kwa kisingizio kwamba maeneo hayo ndiyo yaliyozalisha samaki kwa wingi. Walinzi waliwekwa kuhakikisha kwamba samaki hawakuvuliwa kwenye maeneo ambayo hayakuruhusiwa. Akina yahe waliachiwa maji ya kina kifupi yasiyokuwa na samaki. Sababu ya utawala huo kufanya hivyo ilikuwa ni kupunguza idadi ya samaki waliovuliwa maadamu ndio waliokuwa kitoweo kikubwa kwa Wanabonde. Matokeo yalikuwa kwamba samaki waliongezeka na dola kufaidika kwa kuwauza Ughaibuni. Walipokosa samaki katika maeneo waliotengewa, kina yahe waliishia kuiba samaki kwenye maeneo yasiyoruhusiwa. Wakati mwingine, walishirikiana katika wizi huo na walinzi wa majimakuu kwa kugawana samaki waliowavua kinyume cha sheria iliyowekwa (uk.97-98). Kwa kuwa samaki ndio waliokuwa kitoweo kikubwa kwa Wanabonde, basi Wanajamii walipata matatizo ya kukabiliana na njaa. Japo dola la Bwana Mkubwa lilifaidika kwa kuwauza samaki Ughaibuni, halikuboresha maisha ya Wanabonde wachochole kutokana na mauzo hayo. Tabaka la "Wenyenchi" (watawala) likazidi kuimarika kiuchumi huku tabaka la "Wananchi" (watawaliwa) likizidi kudidimia. Hali hii ilizindisha mvutano baina ya matabaka haya huku Walalahoi wakilenga kuung'oa utawala wa Bwana Mkubwa mamlakani.

Katika riwaya ya *Yasinya*, baadhi ya watu wanafaidika kwa njia zisizo za haki kupitia utozwaji kodi na hivyo basi kuimarisha matabaka yaliyomo katika jamii. Katika muktadha wa utafiti wetu, neno kodi linarejelea fedha inayotozwa na serikali (TUKI: 2013). Japo malipo haya ni

muhimu kwa maendeleo ya nchi, ni unyonyaji wa walipa kodi iwapo serikali itaendelea kukusanya kodi bila kutoa huduma. Katika riwaya hii, wanajamii wanatozwa kodi bila kupewa huduma muhimu kama umeme, maji ya mabomba na barabara nzuri. Hali hii inazua mivutano ya kitabaka baina ya tabaka tawala na tabaka tawaliwa. Katika riwaya ya *Mwanasiasa*, tabaka tawala liliwatoza kodi wachuuzi katika biashara zao duni. Mzigo wa ulipaji kodi uliwalemea wachochole wa Bondeni madhali kodi hizo zilikuwa zikizaana kila siku (uk.97). Mwarupia alilalamikia sheria ya kukata kibali cha kuendesha biashara ndogondogo hata kama ilikuwa ya rukwama au uchuuzi. Aliwatahadharisha Wanabonde kwamba endapo wangeendelea kunyamaza, basi wangeambiwa na utawala wa Bwana Mkubwa wakate kibali hata walipotaka kulala na wake zao majumbani mwao (uk. 100).

Pupa ya mali inayosababisha baadhi ya wanajamii kujiendeleza kwa njia zisizo za haki inaonekana pia kupitia ukiritimba na ubinafsi wa tabaka la matajiri. Ukiritimba ni "tabia ya mtu, kampuni, shirika au serikali kujilimbikizia bidhaa, mali au madaraka bila ya kujali wengine". Ubinafsi hurejelea "hali ya mtu kujifikiria na kujipenda yeye mwenyewe" (TUKI: 2013). Ukiritimba na ubinafsi ni ukosefu wa maadili unaodhihirisha mfumo pendelevu wa uzalishaji mali katika jamii. Kama u-Marx wa kirasimi unavyoeleza, mfumo wa aina hii una nafasi kubwa ya kuamua hali za watu kijamii na kisiasa. Katika riwaya ya *Yasinya*, maovu haya yanajitokeza pale ambapo Kifuja pekee — kutokana na nguvu zake za kisiasa na kiuchumi — anapewa fursa ya kubeba abiria katika jiji huku wengine wakizuiliwa (uk.64). Upendeleo huu una uwezo mkubwa wa kuzidisha pengo baina ya matajiri na maskini na hivyo basi kuunda matabaka. Kifuja, aliye katika tabaka la juu la watawala, anajikuta katika mvutano wa kitabaka na wadhulumiwa wanaopinga ukiritimba na ubinafsi.

Kwa mujibu wa nadharia ya u-Marx wa kirasimi, tendo la kwanza la historia ya binadamu ni kutafuta namna ya kuyatosheleza mahitaji ya kimsingi (Wamitila 2002:183). Ili kuyapata mahitaji hayo, binadamu hujiunga pamoja na kugawa majukumu au kazi ili waweze kuizalisha mali kwa haraka. Katika riwaya ya *Yasinya*, maovu ya ukiritimba na ubinafsi yanajitokeza katika ugawanaji wa majukumu au kazi. Chifu Kifuja (Kiongozi wa Mabonde) aligawa majukumu katika bodi ya usimamizi wa hazina ya ustawishaji wa maeneo alikotoka Asisi. Alifanya hivyo kwa upendeleo na ubinafsi — hali ambayo ililenga kukidhi mahitaji yake ya kimsingi na ya wachache aliowapendelea. Hakutaka kuwapa wapinzani wake nafasi ya kuhudumu katika bodi hiyo. Kwa mfano, kwa kumwona Asisi kama mpinzani sugu wa uongozi wake, Kifuja alimtaka Kipokeo ampinge Asisi kwenye uenyekiti wa bodi hiyo. Tunafahamishwa kwamba Kipokeo

aliyependelewa na Chifu Kifuja hakuwa na ujuzi wa mambo ya utunzaji hazina na uratibu. Kifuja hakujali udhaifu huu. Isitoshe, alizigawa nyadhifa zilizobaki kwa mke wake, binamu yake na rafiki yake Shindo (uk. 43-44). Katika wadhifa wa Yusi mkuu, Kifuja alimpendekeza Tumbo. Tunaarifiwa kwamba bila umaarufu na ushawishi wa Kifuja, Tumbo hangefanikiwa kuupata wadhifa huo. Inasemekana kwamba upendeleo huu ulizima azma za wanakijiji wengine waliokuwa wakiitaka kazi hiyo (uk.109). Katika hali hii, Kifuja na anaowapendelea wana nafasi kubwa ya kujiendeleza kiuchumi huku wasiokuwa na ushawishi wowote wa kisiasa wakibaki nyuma kiuchumi. Kipokeoalitambua dosari iliyokuwapo katika utendakazi wa Kifuja na hakukubali kupigania wadhifa uliopendekezwa kwake huku akisema kwamba kufanya hivyo kungekuwa ni ubinafsi ambao ndio chanzo cha vita, ukabila, utengano, ufujaji na ufisadi (uk.46-47).Dosari nyingine ya utendakazi wa Chifu Kifuja inaonekana katika miradi iliyoanzishwa. Badala ya kufanywa miradi ya kuiendeleza jamii nzima kwa usawa katika maeneo alikotoka Asisi, visima vinne vya maji vilichimbwa kwa upendeleo katika mashamba ya watu binafsi. Kimoja kilichimbwa shambani mwake Kupe, kimoja kwa dadake Kifuja, kingine kwa rafikiye Shindo na cha nne kwa wakwe zake Kifuja. Aidha, majosho yalijengwa kwa namna sambamba na visima (uk. 48). Ili kukwepa mivutano baina ya tabaka tawala na tabaka tawaliwa, wanajamii walidanganywa kwamba miradi ilitekelezwa namna hiyo ili kuipa ulinzi madhubuti. Maovu haya yanadhihirisha matabaka yaliyojengwa kwa misingi ya ushawishi wa kiuchumi na kisiasa na yana uwezo mkubwa wa kuyaendeleza matabaka hayo.

Riwaya ya *Yasinya* inaeleza kwamba, tabaka lenye nguvu za kiuchumi linawalaghai wanyonge. Hii ni mbinu mojawapo ambayo kwayo matabaka yanaimarika katika jamii. Tunafahamishwa haya kupitia mhusika aitwaye Kijasiri. Alipokuwa akifuatilia malipo ya marehemu mumewe katika Shirika la Maba — shirika kubwa sana la bima — Kijasiri analaghaiwa. Anaishia kutamauka na kuona kuwa si rahisi kushinda kesi ya bima (uk.101). Shirika hili lilimilikiwa na Kifuja, Mayowe, Dkt Balaa na Angusha. Watu hawa walikuwa matajiri. Walikuwa katika tabaka la juu katika jamii. Shirika hili lilimhangaisha Kijasiri kwa kuyachelewesha malipo ya mumewe. Haya yanakuwa bayana wakati mhazili wa kampuni hii anamtaka Kijasiri atoe hongo ili ahudumiwe (uk.110). Aidha, daktari Balaa anachelewesha kutoa ripoti yake na hivyo basi kusababisha kuahirishwa kwa kesi iliyohusu malipo hayo. Kadhalika, wakili wa Kijasiri anaongeza malipo ya kesi wakati kesi yenyewe imesimama (uk.96). Baada ya kujaribu akashindwa, wakili mpya wa Kijasiri anaishia kumkwepa Kijasiri na kuahirisha kesi mara kwa mara. Ni wazi kwamba shirika la Maba liliendesha ulaghai. Kijasiri anaeleza kwamba mienendo

kama hiyo kwa wateja wa makampuni ya bima ndiyo huwaogofya watu hadi wakakataa kuchukua bima.

Katika *Yasinya*, hedimasta wa shule ya Msigulu anatumia Mchango wa pesa, kupitia wito wa *harambee*, kujaribu kumlaghai Kijasiri. Alimnyima bintiye Kijasiri nafasi ya kusomea katika shule hiyo baada ya Kijasiri kukataa kumtolea mchango wa *harambee*. Kutokana na maelezo ya hedimasta, uhalali wa *harambee* hiyo ulikuwa wa kutiliwa shaka kama ilivyofichuliwa na Kijasiri katika fomu ya *harambee*. Ukweli huu unajitokeza katika mazungumzo yao ambapo hedimasta alimtaka Kijasiri amwandikie hata kama ni elfu au mia tano ya kusaidia kufadhili elimu ya mtoto wa mpwa wake. Hedimasta alidai kwamba mtoto wa mpwa wake alikuwa yatima hivi kwamba yeye ndiye aliyekuwa mlezi wake. Kwa mshangao, Kijasiri alisema kwamba fomu ya kuchangisha pesa za *harambee* ilikuwa imeandikwa jina la mzazi wa mtoto husika. Akichekacheka, hedimasta alichukua fomu hiyo akalifuta jina la mzazi huku akidai kwamba yalikuwa makosa tu (uk.112-113). Kijasiri alinyimwa nafasi shuleni kwa kuambiwa ajaribu kuitafuta baada ya muhula wa pili ingawa ndipo mwaka ulikuwa umeanza na kwamba aliona wazazi wakiondoka na kuwaacha watoto ndani ya shule. Japo *harambee* nchini Kenya hurejelea wito wa kuvuta pamoja kwa nia ya kuiendeleza jamii, wito huu umetumiwa na watu wengi wakiwa na lengo la kujitajirisha kibinafsi. Ni wito ambao umetumiwa sana kuwalaghai watu huku ukichangia pakubwa katika kuendeleza utabaka katika jamii.

Mbali nakuendelezwa kwa ulaghaikatika taasisi za elimu, watu wazima na razini wanawatumia watoto kuendeleza uovu huo katika barabara za mijini. Riwaya ya *Yasinya* inatueleza kwamba barabara hizo zilijaa watoto wachanga waliopewa vileo vya kila aina ili walale na kuonekana kama viumbe ambao wangekufa wakati wowote. Kila mtoto aliyenyweshwa vileo alilindwa na mtu mzima aliyeketi kando yake. Wakati mwingine, mlinzi alitia mabango yaliyowasihi wapita njia kufanya *harambee* ili mtoto atibiwe moyo ama figo. Jioni, mtu mwenye uwezo kiuchumi na aliyehusika katika biashara hii alikwenda kumchukua mtoto huyo pamoja na mlinzi wake. Mtoto angelipwa kwa kupewa chakula duni kama mkate na soda huku mama mzazi akipata malipo ya shilingi mia na hamsini (uk.78-79). Mama na mwanawe wanaishia kubaki katika ulitima huku wanaoendeleza biashara hii wakinawiri kiuchumi. Hali hii inasababishakuimarika kwa matabaka katika jamii. Haya ni matukio ambayo tunashuhudia kila mara katika mazingira yanayoonekana — barabara za miji ya mataifa mengi. Kwa hivyo, ni matukio yanayotendeka katika mandhari halisi. Kama ilivyo katika malengo yetu, tathmini ya uhalisia wa maudhui tunayohakiki kwa mujibu wa uhalisia kama mbinu ya uhakiki inatuonyesha kwamba hali halisi ya umaskini ndiyo

inayowafanya wazazi na watoto wao kujihusisha na matendo ya aina hii na hivyo basi kulisawiri tabaka la waliotengwa katika jamii; la ombaomba. Licha ya hayo, baadhi ya wanajamii wanazidi kujiendeleza kwa njia zisizo za haki kupitia ajira za watoto kutoka tabaka la maskini. Katika riwaya ya *Yasinya*, Kifuja na Mayowe wanamiliki moja kati ya kampuni zilizotangaza kazi katika nchi za nje — ng'ambo ya bahari. Mwandishi anaziita nchi hizi "nchi za maziwa na asali". Jina hili linadhihirisha kwamba mataifa hayo ni bora kiuchumi kuliko mataifa mengine. Huu ni utabaka katika kiwango cha kimataifa. Kazi nyingi zilizotangazwa zilikuwa za hadhi ya chini kama vile udereva, upishi na za nyumbani. Vijana walipelekwa humo kwa ahadi ya kupata ajira lakini wakaishia kurudi na majeraha na ngano za kutisha. Baadhi ya watoto walioajiriwa katika nchi hizi walipigwa na kuchomwa kwa moto na waajiri wao (uk.130). Huu ni unyanyasaji wa walio wanyonge kiuchumi. Ili kuajiriwa, Ilibidi vijana hawa kutoa kiasi fulani cha pesa kwa kampuni zilizotangaza kazi hizi. Kwa kuhofia kuachwa nje, baadhi ya watu waliuza vikata vyao au wakakopa pesa huku wakiweka jamaa zao kwenye madeni. Wengine waliomba mikopo ya benki ili kuwawezesha wapendwa wao kusafiri kulikopatikana kazi hizi. Matokeo yake ni kuwatajirisha waliomiliki makampuni ya aina hii kama vile Kifuja na Mayowe huku jamaa za vijana hao zikiendelea kudidimia kiuchumi na kuongeza pengo baina ya matabaka katika jamii.

Kadhalika, matabaka katika *Yasinya* yanasawiriwa kupitia ndoa ya lazima ya Kipokeo. Kutokana na tamaa ya mali, binti huyu aliozwa kwa lazima (uk.29). Alilazimishwa na ami zake aolewe na kijana wa tajiri mmoja wa hapo karibu na kwao ambaye alikuwa amewapa nafaka magunia matano na shilingi elfu tatu. Ami yake alizitumia pesa hizo kulipa karo ya mwanawe wa kiume (uk.23). Ni wazi kwamba Kipokeo alitoka katika tabaka la wasiojimudu kiuchumi huku kijana aliyemuoa akitoka katika familia ya tabaka la matajiri.Ni uhalisia kwamba ndoa nyingi za lazima zinafanyika katika makabila mengi barani Afrika huku zikiwadhulumu wasichana wachanga kutoka familia maskini.

Kutokana na umaskini uliowakumba Wanabonde katika riwaya ya *Mwanasiasa*, kulizuka uovu wa utekajinyara wa watoto hususan kutoka familia zilizojiweza kiuchumi. Watekajinyara walitekeleza kitendo hiki kwa nia ya kutaka kulipwa kiasi fulani cha pesa ili wamwachilie mateka. Walifanya hivyo kwa kumficha mtoto waliomteka nyara, kisha wakaandika barua na kuitupa wakati wa usiku karibu na kwao ili kuwajulisha wazazi wake wapeleke pesa mahali fulani kwa muda uliowekwa kabla mtoto wao kuachiliwa (uk.107). Ni wazi kwamba waliotekeleza uovu huu walitoka katika tabaka la maskini huku wakilenga tabaka la matajiri.

Mintarafu ya maelezo katika maudhui haya, tunaona uhalisia wa maudhui ukijitokeza kupitia wahusika wanaotenda maovu tuliyotaja kwa namna inayochochewa waziwazi na hali waliyomo. Hali hii inaweza kuwa haja ya kukidhi mahitaji ya kimsingi kutokana na umaskini au uwezo wa nguvu za kiuchumi, kisiasa na kidini. Wahusika hao ni kama vile: waajiri na wafanyibiashara mabwanyenye, wamilisi wa shirika kubwa la bima kama vile Chifu Kifuja pamoja na watoto ombaomba. Aidha, tungo za kihalisia aghalabu hujikita katika muundo wa utanzu wa riwaya unaoelezea mifumo ya kisiasa, kiuchumi na kitamaduni ya ulimwengu. Tumejadili masuala ya aina hii kama vile utozwaji kodi usiofaa, unyanyasaji wa wafanyikazi, ugawanaji wa majukumu kwa upendeleo na mengine yanayojenga maudhui ya kujiendeleza kwa baadhi ya wanajamii kwa njia zisizo za haki. Kwa hivyo, tunayaona masuala haya yakiwa mwigo wa maisha halisi ya jamii.

### 2.2 Nafasi ya dini katika mfumo wa kitabaka

Suala la dini ni miongoni mwa masuala ya kijamii yanayohusishwa na u-Marx wa kirasimi. Kama anavyoeleza Raines (2002), Karl Marx alikuwa na mengi ya kusema kuhusu dini na mchango wake katika kuendeleza matabaka katika jamii. Kulingana naye, binadamu ndiye ameanzisha dini ili kukidhi mahitaji yake. Kupitia asasi hii, tabaka tawala hususan linaloendeleza mfumo wa ubepari, hudhibiti mienendo ya watu na usalama ili kukandamiza na kuwanyonya watawaliwa ambao wamo katika tabaka la chini. Kiitikadi, dini humfunza binadamu kuwa mtiifu kwa tabaka tawala huku ikimsahaulisha ulimwengu wa kweli. Yaani, watu wa tabaka la chini hufunzwa dini ili kuwafanya waisahau hali halisi ya kisiasa na kiuchumi inayowakumba. Katika hali hiyo, dini huiondoa busara ya binadamu na uwezo wake wa kuzalisha mali. Dini basi humnyima binadamu uhuru wa kufanya mambo na kuafikia upeo wa uwezo wake. Hivi ni kwa sababu uwezo wake huwa umewekewa mipaka(tafsiri yetu). Mawazo haya ni bayana tukizingatia jinsi Bibilia inavyofunza waumini wa dini ya ki-Kristo kutii viongozi na utawala uliopo. Tunayapata hayo katika kitabu cha Warumi (13:1) kinachosema kwamba “kila mtu na aitii mamlaka iliyo kuu; kwa maana hakuna mamlaka yasiyotoka kwa Mungu; na yale yaliyopo yameamriwa na Mungu”. Mstari unaofuata wa sura hiyo katika kitabu hicho nao unasema: “hivyo, amwasiye mwenye mamlaka hushindana na agizo la Mungu; nao washindanao watajipatia hukumu”. Kwa hivyo, haijalishi kama mfumo tawala ni mbaya. Muhimu ni kufuata amri ya Mungu — kutii mamlaka. Itakuwa vigumu kwa waumini wa kweli katika dini ya ki-Kristo kwenda kinyume na agizo hili la Mungu na hivyo basi watafuata mafunzo haya yanayoonekana kuwanyima nafasi na ujasiri wa kudadisi, kufichua, kushutumu na kukosoa

uongozi dhalimu kama ule wa kibepari. Kihalisia, walio mamlakani wamekuwa wakitumia mafunzo kama hayo kwa wanaowapinga ili kuhakikisha wamebaki mamlakani hata kama wao ni madhalimu.

Athari nyingine hasi ya dini ni kumkosesha binadamu ujasiri na uwezo wa kufikiri kibinafsi. Kutokana na hali hii, uwezo wa binadamu wa kutekeleza mambo huwa umedhibitiwa na Mungu. Kwa mfano, mafunzo ya Bibilia katika Mathayo (6:26) yanaeleza kuhusu ndege wa angani ambao hawapandi, hawavuni wala hawakusanyi ghalani lakini Baba wa binguni huwalisha. Basi mkristo hastahili kujisumbua kwa mahitaji yake kwani Mungu atamtosheleza. Kadhalika mafunzo katika 1Samuel (2:7) yanaonyesha kwamba uwezo wa kuwa tajiri uko mikononi mwa Mungu kwa kuwa yeye ndiye hutajirisha na hufukarisha. Hivi ni kumaanisha kwamba ni kwa mapenzi na kudura za Mungu kukawa na matabaka ya kiuchumi katika jamii na hatuwezi kumlaumu mtu yeyote kutokana na pengo lililopo baina ya matajiri na maskini. Mafunzo kama hayo huwafanya waumini wa dini ya ki-Kristo kukwama kimawazo wanapokabiliwa na changamoto za kiuchumi. Badala ya kufikiria namna ya kujikwamua, wanaona ni heri wamtegemee Mungu kwa maana yeye ndiye mpaji wa vyote kama ilivyoandikwa katika Wafilipi (4:19) kwamba: "Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu". Wanapofuata mafunzo hayo, waumini hujisalimisha kwa mienendo ya kijamii.

Kutokana na athari hasi za dini kwa binadamu, Marx aliiona asasi hii kama ya kipumbavu kwa kuwa inakana yale yote yanayoheshimiwa katika viumbe kwa kuwageuza au kuwafanya wanyonge au watumwa na pia wakubali hali ilivyo. Aliita dini, njozi ya uongo kwa maskini inayopeana sababu na kisingizio cha kuiwezesha jamii iendelee jinsi ilivyo au bila kubadilika. Hivi ni kwa sababu uhalisia wa kiuchumi huwazuia maskini wanaokandamizwa kupata furaha ya kweli katika maisha huku dini ikiwaeleza kwamba wataipata furaha hiyo katika maisha baada ya kifo. Tukichunguza jinsi dini ya ki-Kristo inavyoweza kuwafanya waumini kuwa wanyonge wa kiuchumi na hatimaye watumwa, tunaona kwamba Bibilia Takatifu inapinga utajiri. Jambo hili linaweza kusababisha wakristo waridhike hata katika hali yao ya umaskini. Kwa mfano, mafunzo ya Yesu Kristo yanaeleza kwamba ni vigumu kwa tajiri kuingia katika ufalme wa binguni. Katika Bibilia, haya yanapatikana katika funzo linalosema kwamba "ni rahisi kwa ngamia kupenya tundu la sindano kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu" (Mathayo 19:23-24). Funzo lingine linalopinga utajiri linapatikana katika Luka (16:13) ambapo tunaambiwa kwamba

“hakuna mtumishi awezaye kutumikia mabwana wawili” na hivyo basi, “hatuwezi kumtumikia Mungu na mali”.

Sifa hasi za utajiri na zinazodhihirisha upumbavu wa asasi ya dini zinaendelea kutolewa katika kitabu cha Mhubiri (1:3) ambapo Mhubiri anakosa kuona thamani ya kufanya kazi au kutia bidii katika maisha. Anauliza: “mtu ana faida gani ya kazi yake yote aifanyayo chini ya jua?” Anasema pia kwamba “mambo yote yamejaa uchovu” (Mhubiri 1:8). Katika maisha yake, Mhubiri anaeleza jinsi alivyonunua watumwa na wajakazi, akawa na wazalia nyumbani mwake, tena akawa na mali nyingi za ng’ombe, kondoo, fedha, dhahabu na tunu za kifalme kupita wote waliomtangulia katika Yerusalemu (Mhubiri 2:7-8). Ingawa alikuwa na utajiri mwingi kiasi hicho, maoni yake ni kwamba “mambo yote ni ubatili (Mhubiri 1:2) na hakuna faida yoyote apatayo mtu kwa kazi yake chini ya jua” (Mhubiri 2:11). Mafunzo ya aina hii yana uwezo wa kumtamausha kila mja na labda, mkristo hataiona haja ya kufanya kazi ili kujiendeleza kiuchumi. Badala yake, atazingatia kutenda wema amfurahishe Mungu wake huku akifuatilia mafunzo ya dini kwamba“wenye haki watairithi nchi; nao watakaa humo milele” (Zaburi 37:29). Kwa mujibu wa imani ya ki-Kristo, tukio hili la kuirithi nchi ndilo litakalowapa waumini wake furaha ya kweli baada ya kifo.

Kwa mtazamo wake Marx, dini huendeleza unafiki maadamu inaweza kutangaza na kuunga mkono kanuni muhimu huku ikiwaunga mkono wakandamizaji. Kwa mfano, mafunzo ya dini ya kuhimiza kutopenda pesa au utajiri yanaweza kusaidia nchi katika kupigana na tamaa ya pesa inayosababisha ufisadi. Hata hivyo, wahubiri wengi wemekwenda kinyume na mafunzo hayo kiasi cha kuwanyanyasa waumini kupitia mafunzo yaliyopotoka ya “kupanda mbegu”. Katika baadhi ya makanisa ya ki-Kristo, mafundisho haya yanaendeleza unafiki wa kidini. Ni mafunzo ambayo yanaonekana kuigeuza asasi ya dini kuwa ya kibiashara. Katika mafunzo hayo, waumini wa dini ya ki-Kristo hushawishiwa kutoa mali yao kwa kanisa ili wabarikiwe kwa namna zote ikiwemo kupata utajiri. Imani wanayotiwa wakristo hawa ni kwamba mtu hawezi kupata baraka zozote pasipo kumtolea Mungu mali. Kwa hivyo, siri ya kupata utajiri ni kutoa mali kwa Mungu. Siri ya kupata usawa katika jamii ni kumtolea Mungu mali. Kadhalika,hiyo ndiyo siri ya kuepuka mivutano na matatizo yote katika jamii. Kwa maoni yetu, mafunzo hayo ya kutoa mali yametumiwa visivyo na baadhi ya wahubiri ili kuwafaa katika azma ya kujiendeleza kiuchumi. Mafunzo ya “kupanda mbegu” yanamfanya mkristo hata yule maskini kujikaza kutafuta mali ya kutoa ili angaa abarikiwe. Katika hali ambapo waumini wanadhulumiwa kiuchumi, wanaambiwa watoe mali yao ili waombewe, waondokewe na dhuluma za aina hiyo. Kwa mfano, unaweza

kusikia waumini wakiombewa waongezewe mshahara au kupandishwa madaraka katika mahali pao pa kufanyia kazi. Kwa mujibu wa imani hiyo, hawataona haja ya kupigania haki zao, wajikomboe wao wenyewe kutokana na dhuluma za kulipwa ujira duni, kama mtazamo wa u-Marx wa kirasimi unavyopendekeza. Badala yake, wataombewa na wangojee muujiza wa Mungu kufanyika ambao huenda ukaishia kuwa njozi ya uongo.

Fauka ya hayo tumekwisha kueleza, Marx alisema kwamba dini ni mpumuo wa kiumbe anayekandamizwa au dawa ya kutuliza akili (afyuni ya watu). Haya yanadhihirishwa na funzo katika kitabu cha Mathayo (5:4) linalosema: “Heri wenye huzuni; maana hao watafarijika”. Funzo hili lina uwezo wa kumtuliza muumini anayedhulumiwa kiasi cha kutokabiliana na dhuluma anazotendewa. Dhima hiyo ya dini kama kitulizo cha akili pia inapatikana katika kitabu cha Luka (6:29) kinachosema: “Akupigaye shavu moja, mgeuzie la pili, naye akunyang’anyaye joho lako, usimzuilie na kanzu”. Haya ni mafunzo yanayomdanganya muumini kwamba mambo yote ni sawa hata anaponyanyaswa. Kutokana nayo, huenda mkristo asione haja ya kuchukua hatua yoyote kujikomboa.

Kama alivyosema Marx, dini katika riwaya ya *Yasinya*, inatumiwa kuendeleza unafiki wa walio katika tabaka la juu (watawala) kwa minajili ya kuwapumbaza watawaliwa ili wavumilie ukandamizaji wanaotendewa. Hali hii inajitokeza katika mkutano wa maombi ya umma ya kitaifa ambapo viongozi wanakosa kutubu dhambi walizokuwa wametenda. Kwa maoni ya Asisi, maombi hayoyalikuwa unafiki mtupu. Unafiki huo unaonekana pale ambapo kiongozi wa maombi alikosa kutaja kwa jina kila dhambi iliyokuwa imetendwa hasa na viongozi. Kwa hivyo, baada ya maombi ya toba, nchi haikuonekana kuwa imeponywa na Mungu kutokana na dhambi za ubaguzi, utengano na udhalilishaji wa wanyonge kama kasisi alivyokuwa amesoma kwamba: “watu wangu wakitubu, hakika nitaponya nchi” (uk.29-32). Zaidi ya hayo, tunaelezwa kwamba makaziya tabaka la maskini yalikuwa na makanisa ilhali maabadi kama hayo hayakuwamo katika makazi ya tabaka la matajiri. Kama tunavyoelewa, tofauti hii inasababishwa na yale yanayoelezwa na Marx kwamba dini ni mpumuo wa kiumbe anayekandamizwa au dawa ya kutuliza akili. Kwa hivyo, waliohitaji maabadi ni maskini na wala sio matajiri. Hata hivyo, tunaona makanisha yakitumiwa na maskini kama mahali pa kunywea vileo ili kuwasahaulisha masaibu yao.Utumiaji wa makanisa na walevi haumo katika muktadha wa aliyoyasema Marx kuhusu nafasi ya dini katika mfumo wa kitabaka bali ni dhihirisho tu la hali ya kutamauka kwa tabaka la maskini.

Katika riwaya ya *Mwanasiasa*, dini inatumiwa kuficha na kuendeleza maovu ya upendeleo wa watu fulani, ufisadi na uimarishaji wa matabaka. Kwa mfano, Mwarandu aliyekuwa kiongozi wa kidini na aliyewaelekeza wanadamu katika njia ya haki, alikuwa pia msiri wa dola la Bwana Mkubwa; dola ambalo liliendeleza dhuluma si haba kwa Wanabonde. Ni wazi kwamba Mwarandu alikuwa mnafiki. Si ajabu kwamba aliacha huduma ya Mungu na kujiunga na siasa. Katika kampeni zake, Mwarandu alipata ufadhili mkubwa kutoka upande wa dola kwa sababu aliitumikia serikali iliyoongozwa na Bwana Mkubwa. Huu ni utumiaji mbaya ya mali ya umma. Mhusika huyu alipendelewa kwa sababu, sawa na Bwana Mkubwa, alitoka katika kabila la Wanyazi. Kabila hili lilipendelewa zaidi na dola katika nyanja zote za kimaisha (uk-49). Bila shaka, upendeleo huu ulichangia katika kuimarisha matabaka Bondeni. Mwarandu aliingia katika siasa kupitia ushawishi wa baadhi ya mamwinyi wa Bondeni walioegemea upande wa Bwana Mkubwa kisiasa. Yeye anawakilisha viongozi wa dini ambao kwa lengo la kujiendeleza kisiasa na kiuchumi, huunga mkono utawala unaowakandamiza watawaliwa badala ya kuukosoa. Kiini cha dosari hii ni tamaa na ubinafsi.

Kama Mwarandu, Bwana Mwakuduwa alikuwa mkuu wa kidini. Yeye ndiye aliyeanzisha hafla ya mkutano wa kisiasa wa Bwana Mkubwa katika eneo la Mkunguni kwa ibada. Kabla na baada ya maombi, Mwakuduwa alisujudia upande wa jukwaa alipokuwa ameketi Bwana Mkubwa. Katika maombi yake, Mwakuduwa alimwombea Bwana Mkubwa peke yake. Alimwombea azidi kuiongoza Bondeni milele (uk.24-25). Ni wazi kwamba mwanadini huyu hakutambua dosari iliyokuwapo katika utawala wa Bwana Mkubwa na kama aliitambua, basi alikuwa mnafiki. Udhaifu wake katika kutoukosoa utawala wa Bwana Mkubwa unampa kiongozi huyu nafasi ya kuendelea kuwadhulumu Wanabonde wachochole na hivyo basi kuzidisha pengo baina ya matabaka yaliyomo.

Katika riwaya hii (*Mwanasiasa*), tunaelezwa jinsi waliokuwa na uwezo wa kidini (sawa na waliokuwa na uwezo wa kisiasa na kiuchumi) walivyotumia nyadhifa zao kujilimbikizia mali kwa kunyakua ardhi ya maskini. Katika hali hii, dini inaonekana ikiendeleza unafiki kwa kuunga mkono ukandamizaji kama alivyosema Marx katika nadharia ya u-Marx wa kirasimi. Matokeo yake ni kupanua pengo baina ya matabaka katika jamii. Hapo awali, viongozi wa kidini Bondeni walitegemewa katika jamii kwa uadilifu na msimamo wao katika kutoa kauli ambazo hazikuwa na upendeleo. Baadaye, walianza kutahadhari walipokuwa wakitoa kauli zao kuhusu yaliyokuwa yakiendelea katika utawala wa Bwana Mkubwa. Hali hii ilisababishwa na hofu ya kuandamwa na kuadhibiwa na utawala huo. Mbali na kwamba wanadini hawa walihofu kuchukuliwa hatua

kali na utawala wa Bwana Mkubwa, kushindwa kuukosoa utawala huo kulitokana na ukweli kwamba hata wao walitumia vyeo vyao vya kidini kujilimbikizia mali kwa njia zisizo za haki. Kwa sababu hizi, viongozi wa kidini walionekana kuunga mkono utawala wa Bwana Mkubwa uliowadhulumu Wanabonde wachochole. Hawakuwa wa kutegemewa tena katika kudhibiti maadili miongoni mwa wanajamii. Kutokana na mabadiliko haya, Bwana Mkubwa alipata nafasi ya kuwadanganya Wanabonde wachochole (uk.102). Tungo za kihalisia huwa na wahusika wa kawaida walio na sifa ya kubadilika katika mitazamo, misimamo au matendo yao. Katika riwaya ya *Mwanasiasa*, msimamo unaobadilika wa viongozi wa kidini ni sifa inayoakisi mwigo wa maisha halisi katika jamii.

Kwa mujibu wa Mwarupia, ilikuwa ni unyonge wa kidini kwa Wanabonde maskini kuamini kuwa uwepo wa Mungu ungewasaidia kukabiliana na masaibu yaliyowasibu. Kwa hivyo, imani ya Mwarupia ilikuwa tofauti na ile ya Wanabonde wengine maskini na waliodhulumiwa. Yeye alishikilia kwamba Mungu hangekusaidia katika mambo yote (uk.118). Tunavyoelewa ni kwamba, kuwa na imani kama walivyoamini Wanabonde maskini, kunatilia mkazo maoni ya Marx kwamba dini huiondoa busara ya binadamu. Kadhalika, imani ya kidini inatumika kuwatia Wanabonde matumaini ya uongo. Msimulizi anatuarifu kwamba walijitokeza "manabii" kutoka Ughaibuni wakajiita "miungu". Wanabonde waliwaamini "miungu" hawa wakichukulia kwamba kwa kufanya hivyo, huenda maisha yao yangeongoka. Inaonekana kwamba kilichokuwa muhimu kwa "miungu" hawa ni sadaka walioitisha. Maisha ya Wanabonde maskini hayakuongoka bali yalibaki vile vile (uk.92). Katika hali hii, wanadini wanatumia ukata na kutamauka kwa wanajamii kujiendeleza kiuchumi. Imani za Wanabonde kwa "miungu" hawa haziwapi nafasi ya kufikiria namna ya kujinasua kutokana na madhila yaliyowakumba.

Kutokana na dhuluma zilizoendelezwa na utawala wa Bwana Mkubwa kwa Wanabonde, wanajamii hawa walianza kukusanyika mara kwa mara ili kutoa kilio chao kwa mizimu ya kale. Walijazana maabadini, wakafunga, wakaomba na kufanya matambiko katika msitu wa Nguu Tatu (uk.107-108). Hivi ni kumaanisha kwamba Wanabonde waliodhulumiwa waliamini kuwa mizimu ya kale ilikuwa na uwezo wa kuwatatulia matatizo yao. Kulingana na mojawapo ya mihimili ya nadharia inayoongoza utafiti wetu, hii ni imani potovu inayoendeleza na kudhibiti mgawanyiko wa jamii kitabaka. Ni imani iliyowakosesha wanyonge nafasi ya kupigania haki na usawa katika jamii.

### 2.3 Ubaguzi na mchakato wa kutafuta usawa katika jamii iliyogawika kitabaka

Kwa mujibu wa TUKI (2004), ubaguzi ni "hali ya kutoa vitu au huduma kwa upendeleo. Ni mfumo wa kijamii wa kutoa huduma kwa upendeleo kwa misingi ya rangi, jinsia, kabila n.k." Kutokana na maelezo hayo, ni wazi kwamba ubaguzi una nafasi kubwa ya kudhihirisha na kuendeleza matabaka katika jamii. Kwa kiwango kikubwa, tumelijadili suala hili la ubaguzi katika uchanganuzi wa maudhui ya utajiri na umaskini ambapo tumedhihirisha jinsi baadhi ya makazi ya binadamu yametengwa au kubaguliwa na viongozi kimaendeleo na hivyo basi kusababisha kuwako kwa mitaa duni kunakoishi maskini na mingine ya kifahari kunakoishi matajiri. Katika sehemu hii, hakuna haja ya kuliangazia suala hili zaidi tusije tukasababisha kosa la urudiaji.Mbali na ubaguzi uliolenga makazi ya watu, riwaya ya *Yasinya* inatueleza kuhusu ubaguzi ulioendelezwa kwenye mkutano wa maombi ya toba. Waliokaa kwenye jukwaa walikuwa watu mashuhuri. Walikuwa wakuu wa makampuni, dini, siasa na watajika wengine. Hawa waliyaegesha magari yao ndani ya uwanja huku watu wa kawaida wakiambiwa wayaegeshe yao nje ya uwanja. Kinyume na alivyotarajia Asisi, mkutano huo haukuwafanya waliouhudhuria kuonekana sawa mbele ya Mungu madhali waheshimiwa walipopewa soda, Asisi alinyimwa na hata kuamriwa asisimame karibu nao (uk.30-32). Haya yalitokea wakati Asisi alijaribu kuwakaribia waheshimiwa kutokana na njaa ya siku mbili aliyokuwa nayo. Askari wa mheshimiwa mmoja alimwamuru asonge na kumtishia kwamba angemfunga iwapo hangetii. Mheshimiwa aliyekuwa karibu na Asisi alifurahi alipoona walinzi wake wakimfukuza Asisi. Mheshimiwa huyo alilaani wachochole na wahitaji wote katika sehemu yake (uk 29-33). Yaliyompata Asisi katika mkutano huu yanaonyesha mvutano wa kitabaka unaoletwa na tofauti za kiuchumi na kisiasa baina ya watawaliwa walio katika tabaka la chini na viongozi wanaotawala.

Katika riwaya ya *Mwanasiasa*, makazi ya Bwana Mkubwa yalikuwa kasri. Msimulizi anatueleza kwamba ilikuwa nadra sana kwa Wanabonde ambao hawakuwa na hadhi kukanyaga eneo hili (uk.16). Huu ni ubaguzi unaoegemea matabaka katika jamii. Bwana Mkubwa na waliokuwa na hadhi wanawakilisha tabaka la juu, tabaka la 'wenyenchi'. Tendo linalowabagua watoto kutoka familia maskini linajitokeza katika makaribisho ya Bwana Mkubwa kwenye mkutano wa hadhara wa Mkunguni. Katika mkutano huo, Bwana Mkubwa alikaribishwa kwa kuvishwa shada la maua na mmojawapo wa watoto wa wamwinyi. Inasemekana kwamba jambo hili lilikuwa la kawaida (uk.23). Msomaji wa riwaya hii hakosi kuona kwamba kinachofanya tukio hili kuwa la kawaida ni mgawanyiko wa jamii kitabaka ambapo Bwana Mkubwa, wamwinyi na watoto wao

wamo katika tabaka la matajiri — walio mamlakani. Kutokana ubaguzi na dhuluma nyingine kwa tabaka la maskini, watu hawa wanatamauka. Kwa mujibu wa TUKI (2004), kutamauka ni "hali ya kukata tamaa au kukosa kuwa na matarajio ya kupata kitu". Katika riwaya ya *Mwanasiasa* — kabla ya mwamko — wachochole katika Bondeni ya viamboni wamo katika hali ya kutamauka. Hawatambui kuwa wao pia wamechangia katika kuunda jamii inayowakandamiza. Wanashindwa kutambua kwamba yale wanayopitia yanatokana na jinsi wanavyowaza na yale wanayotenda. Hali hii inaweza kudhihirika kupitia lugha yao — lugha ya unyonge na kukata tamaa.

Unyonge wa moyoni unadhihirisha kutamauka kwa Wanabonde wanaodhulumiwa katika kupigania usawa miongoni mwao. Hali hii ya kutamauka inajitokeza pale ambapo Mkewe Mwarupia anaingiwa na wasiwasi baada ya mumewe kumjulisha nia yake ya kutaka kujitosa siasani. Anamtahadharisha Mwarupia katika azma yake ya kujitosa siasani ili kumpinga Mwasefu, kiongozi katika utawala wa Bwana Mkubwa. Anamwambia: "Sasa huyo mtu wa kumpa Mwasefu changamoto ni wewe, mume wangu? Habari hizi zitakapofika kwa Bwana Mkubwa mume wangu si watakutia ndani?" (uk.43)

Wanasiasa wengi walijua hila za Bwana Mkubwa zilizomwezesha kuendelea kushikilia mamlaka Bondeni lakini hawakuwa na lolote la kufanya. Bwana Mkubwa aliwachezea shere maadamu alikuwa na ushawishi mwingi wa kisiasa (uk.47). Msimulizi anatuarifu kwamba Wanabonde waliona kana kwamba Bwana Mkubwa ndiye aliyehimili maisha yao. Walilalamika kila uchao, wakiuliza: "Tutaishi vipi maisha haya, jamani?"…"hata mbwa ana nafuu" (uk.47). Kutokana na kutamauka kwao, Wanabonde walipokabiliana na ugumu wa maisha, hawakwenda kwa wawakilishi wa dola au Mwasefu aliyekuwa mjumbe wao, bali walimwendea Mwarupia (uk.47). Hivi ni kwa sababu viongozi hawa hawakuwasilisha matatizo ya Wanabonde kwa Bwana Mkubwa ambaye pia hakuwa tayari kuyashughulikia. Haya yanajitokeza katika mkutano wa hadhara uliofanyika Mkunguni. Katika hotuba yake, Mwaakida anamwambia Bwana Mkubwa: "Kama unavyoona wewe mwenyewe, Hababi wetu, Wanabonde hawana shida yoyote na ni watu wanaokupenda sana. Umewafanyia mengi na ni watu wanaopenda amani" (uk.27). Akikariri maneno ya Mwaakida, Mwangome pia anamhadaa Bwana Mkubwa kuwa ni kiongozi mzuri. Anamwambia kwamba amefanya mambo mengi Bondeni. Anasema: "Tujuavyo, hakuna mwingine ambaye ametufanyia mengi hapa Bondeni kuliko muadhamu wetu" (uk.29). Umati uliohudhuria mkutano ulimuunga Mwangome mkono kwamba hakuna mtu mwingine aliyewafanyia Wanabondeni mambo mengi kuliko Bwana Mkubwa. Ni dhahiri kuwa

Mwangome alimsifu Bwana Mkubwa huku akijua kwamba mengi ya yaliyosemwa kumhusu, hususan sifa zake, hayakuwa ya ukweli. Alilimbikiziwa sifa tupu. Huku ni kumdekeza — hali ambayo ilimpa nafasi ya kuendeleza uongozi mbaya.

Wanabondeni hawakuwa na ujasiri wa kumwambia Bwana Mkubwa mahitaji yao wala makosa yake katika uongozi. Udhaifu kama huu unadhihirishwa na kinara wa walimu alipokosa kuwatetea walimu waongezewe mshahara madhali maisha yalikuwa magumu. Badala yake, alimpongeza Bwana Mkubwa kwa kuwawezesha walimu kufika mjini kwenye tamasha za kitaifa za muziki (uk.27). Alimwomba Bwana Mkubwa awawezeshe tena walimu kufika kwenye tamasha hizo katika siku za baadaye. Jambo hili linaonyesha kuwa kiongozi huyu ameshindwa kuwawakilisha walimu ipasavyo. Katika hali hii, anampa Bwana Mkubwa nafasi ya kuendelea kuwadhulumu walimu kwa kuwapa mshahara duni. Matatizo wanayopitia walimu yanachangiwa pakubwa na jiisi kiongozi wao anavyowaza na kutenda.

Mwanasiasa Mwasefu alikuwa mwakilishi wa Wanabonde katika mkutano wa hadhara wa Bwana Mkubwa. Katika mkutano huo, kinara wa vikundi vya akina mama (Bi. Mwanahela) alimkabidhi matakwa ya akina mama ayawasilishe kwa Bwana Mkubwa maadamu mwanamke hakuruhusiwa na mila za Bondeni kusimama kadamnasi na kuzungumza (uk.28). Katika mkutano huo, kina mama walikusanyika pahali pamoja, mbali kabisa na wanaume ambapo walishughulika tu katika kupiga vigelegele na chereko (uk.29). Hali hii inatuonyesha jinsi mila na tamaduni za jamii hii zinavyotumiwa kutenga, kubagua na kudunisha wanawake kijinsia na hivyo basi kuwanyima nafasi ya kujiendeleza kisiasa na kiuchumi sawasawa na jinsia ya kiume. Hali hii ina uwezo wa kuibua na kuendeleza matabaka katika jamii.

Vilevile, Mwasefu hakuwakilisha Wanabonde vizuri. Alikosa kuwasilisha kwa Bwana Mkubwa, matakwa yote ya Wanabonde yaliyokuwa kwenye orodha ya ardhilhali zao. Alifanya hivi kwa kushikilia kuwa, baadhi ya yale aliyoandikiwa kumweleza Bwana Mkubwa kwenye ardhihali zile asingetaka Bwana Mkubwa ayajue. Angeyasema baadhi tu ya yale ambayo yangemridhisha Bwana Mkubwa kutokana na imani inayodhihirisha kutamauka kwamba ‘kuambizana kupo, lakini kusikilizana hakuna’ (uk.28). Imani hii imetokana na hali ya muda mrefu ya Bwana Mkubwa kutowajibikia mahitaji ya Wanabonde huku wenye mamlaka kama Mwasefu wakitaka kumridhisha kutokana na ubinafsi wao. Kwa hivyo, matakwa ya akina mama ya kujengewa zahanati pamoja na mahitaji mengine ya Wanabonde hayakuwasilishwa kwa Bwana Mkubwa. Mwasefu alitekeleza wajibu wake kwa namna iliyoendeleza uonevu wa wanawake ambao hasa ndio waliokuwa wachochole wengi Bondeni. Kama walivyo Kinara wa walimu na Mwaakida,

Mwasefu ni mtu wa kumdekeza Bwana Mkubwa. Kupitia kwa mhusika huyu, tunaona hali kubwa ya kutowajibika kwa Bwana Mkubwa katika kuwatimizia Wanabonde mahitaji yao. Hii ndiyo sababu anaambiwa tu mambo ambayo yalionekana yangemfurahisha.

Alipokuwa akimkaribisha Bwana Mkubwa awahutubie Wanabonde katika mkutano wa hadhara, Bambua alitumia majina anuwai ya heshima kumwita Bwana Mkubwa. Alimwita Muadhama, Msharafu, Mtukufu, Bwana wetu na Hababi (uk.30-31). Kutokana na hali duni ya kiuchumi ya Wanabondeni wachochole akiwemo Bambua, majina haya ni kinaya tupu. Wamwinyi nao waliubusu mkono wa Bwana Mkubwa na kumsujudia wakati kiongozi huyo alikuwa akiwasalimia katika mkutano wa hadhara huko Mkunguni (uk.23). Walifanya hivyo, si kwa sababu ya heshima waliyokuwa nayo kwa Bwana Mkubwa bali walijifanya wema ili waendelee kunufaika kiuchumi kutokana na utawala wake. Tunavyoona ni kwamba heshima ya kiwango hiki inastahiki kupewa Mwenyezi Mungu. Si binadamu na hasa kiongozi kama Bwana Mkubwa. Mandhari katika mkutano wa hadhara pia yanaonyesha heshima kubwa (japo ya bandia) aliyopewa Bwana Mkubwa. Kiti chake hakikuwa cha kawaida. Aliwekewa arshi. Mbele ya jukwaa, alijengewa mimbari na kipazasauti chake kilikuwa mahususi (uk.31). Kutokana na utawala wake mbovu uliosheheni ahadi za uongo, ubaguzi wa Wanabondeni na dhuluma nyingi kwao, kiongozi huyu hakustahili heshima hii. Hata hivyo, mahusiano kama haya yanaweza kuthibitika katika ulimwengu halisi.

Kama ilivyo katika uhalisia, matendo ya watawaliwa maskini yanachochewa na hali waliyomo — kutamauka kutokana na utawala mbaya na hali zao duni za kiuchumi. Kabla ya kuzinduliwa, Mwarupia na Mwatua walikuwa katika hali ya kutamauka kutokanana matatizo yaliyolikumba tabaka la wachochole waliodhulumiwa. Kwa mfano, Mwatua alionyesha kutamauka kwake kwa kutupa mikono kama ishara ya kushindwa na suluhu kwa suala la kula kadhongo, na kuuliza: "tutafanyaje na utawala wetu ndio huu?" Mfano mwingine unaonekana wakati wa uchaguzi ambapo baadhi ya Wanabonde hawakuona haja ya kupiga kura. Hivi ni kwa sababu wanasiasa wale wale walichaguliwa hivi kwamba wengi wao waliona vyeo walivyokuwa navyo vilikuwa ni haki yao na wala siyo dhamana waliyopewa na watu. Hata hivyo, Mwaakida (mwakilishi wa dola, macho na masikio ya Bwana Mkubwa viamboni) alifanya msako kuwashurutisha kwenda kupiga kura. Waliopatikana walishtakiwa. Jambo hili halikuwapendeza Wanabonde ambao kutokana na umaskini wao, walihofu kwamba kushinda wakipiga kura mchana kutwa kungewafanya wakose chakula jioni (uk.67). Waliona kwamba ingekuwa bora kwenda kutarazaki. Ni uhalisia kwamba msimamo kama huu (wa kutopiga kura) umo katika jamii nyingi

zinazokumbwa na utawala kandamizi ambapo hali ya kutamauka huwa ni sababu mojawapo ya kutenda hivyo. Katika u-Marx wa kirasimi, utawala usiobadilika (kama huu wa Bwana Mkubwa) una nafasi kubwa ya kuendeleza mfumo wa ubepari. Suala la kisiasa (kama hili tulilolijadili) ni mojawapo ya masuala katika muundo wa utanzu wa riwaya ambao kwa muda mrefu umezingatia uhalisia.

Sheria ni mojawapo ya asasi za kijamii zinazohusishwa na u-Marx wa kirasimi ambapo asasi hii hutumiwa kuendeleza tabaka la matajiri (hususan walio mamlakani) huku ikizidisha unyonge wa kiuchumi wa tabaka la maskini. Katika riwaya ya *Yasinya*, Emali (mamake Asisi), anatamauka kutokana na malipo duni na yaliyocheleweshwa ya zao la mibuni hivi kwamba aliona ilikuwa bora kuikata na badala yake kuendeleza kilimo cha ndizi na viazi vikuu. Kutamauka huku kunazidishwa na sheria iliyomzuilia kuikata mibuni kwa vile alitakiwa kuwa na ruhusa ya halmashauri ya kahawa nchini (uk.76). Katika hali nyingine, Emali anadhihirisha unyonge na kutamauka kutokana na kesi ya Asisi. Askari aliyekuwa na kesi hii alitaka hongo ya sehemu ya shamba la marehemu baba yake Asisi ili amsaidie kesi yake imalizike. Asisi alikataa katakata lakini mama yake alimsihi apeane huku akidai kwamba hangekuwa wa kwanza kufanya hivyo (uk.64). Hali hii inaonyesha kukithiri kwa dhuluma na ufisadi katika mahakama. Unyonge wa Emali unamnyima nafasi ya kukabiliana na dhuluma zilizotendewa watu maskini.

Tukichunguza maisha ya Kipokeo, tunaona kwamba alikuwa ameajiriwa kazi lakini akaiacha baadaye ili kujinusuru kutokana na kutumiwa vibaya kimapenzi na mwajiri wake. Kwa sababu ya ugumu wa maisha, Kipokeo aliishia kujihusisha na ukahaba ili aishi. Anapoyaeleza haya kwa Asisi, Kipokeo anaonyesha kutamauka kwake anaposema kwamba hakuipenda kazi hiyo lakini hakuwa na lingine la kufanya (uk.22). Tukio hili linatuonyesha unyonge wa Kipokeo baada ya kutamauka ambapo alikosa moyo na ujasiri wa kupigania haki na nafasi yake katika jamii. Ni tukio lililomnyima nafasi ya kujiendeleza kiuchumi na hivyo bazi likazidi kumzamisha kwenye tabaka la wahitaji.

Katika makazi ya walalahoi, Mabonde (katika riwaya ya *Yasinya*) haikuwa imeendelea. Hali hii inasababisha kutamauka kwa Emali na wanawake alioshirikiana nao kumpeleka mama ajuza kwenye zahanati (uk.91-93). Huku akijisemea, mwanamke mmoja aliuliza iwapo Mabonde haikuwa sehemu ya watu wengine. Kutokana na umaskini, watoto waliokuwa wakiomba katika barabara za miji pia wametamauka. Tunajulishwa haya kutokana na kauli zao kwa wapitanjia ambapo waliomba kusaidiwa huku wakiongeza kuwa hata hawakuwa na pa kuishi (uk.78). Kadhalika, riwaya ya *Yasinya* inatueleza kuwa Asisi anatamauka kutokana na usemi aliousikia

shuleni kwamba vijana ndio viongozi wa kesho. Ni uhalisia kwamba usemi huu ni maarufu sana katika taasisi za elimu lakini Asisi anaishia kuona kwamba haukuwa wa kweli na kwamba mwalimu aliyesema hivyo alikuwa mwota ndoto na mbunifu wa mawazo ambayo yalilenga tu kumtia mwanafunzi matumaini bila kumpa uhalisia na hakikisho (uk.34). Hatukubaliani na Asisi kwamba Mwalimu alikuwa mwota ndoto kwani mawazo yake (Asisi) yanatokana na hali ya kutamauka kunakosababishwa na ubinafsi wa walio mamlakani. Kutamauka kwake kunaonyesha hali ambapo baadhi ya viongozi huendelea kushikilia mamlaka hata katika uzeeni wao bila kujali kuweko kwa vijana. Athari ya uhafidhina huu ni kwamba vijana hukosa mitaji na nafasi ya kujiendeleza kiuchumi hivi kwamba wanabaki maskini huku viongozi nao wakiendelea kunawiri kiuchumi.

Uwanjani palipokuwa na maombi ya umma, Asisi anatamauka kutokana na njaa iliyomkumba. Aliwatafuta na kuwakosa watu ambao wangempa msaada wa lishe. Kama Asisi, watu hao aliotafuta— mzee Juma, Betty na Griffy — walitoka katika tabaka la maskini. Tunaarifiwa kwamba alipokuwa kwake, mzee Juma alikuwa akimtilia Asisi makombo. Makombo hayo yalipatikana hasa wakati mzee Juma angetumiwa pesa kidogo na wanawe mwishoni mwa mwezi. Kwa hivyo, Asisi kutiliwa makombo na mzee Juma hakumaanishi kwamba mzee huyu alikuwa tajiri wa kula na kusaza. Wakati Betty alikuwa ameenda kwa babake kuomba karo ya Josephine, Griffy alikuwa ameenda kwa nduguye Mabo Kelfy kuazima vitabu. Hali ya kiuchumi ya Betty na Griffy katika jamii inaonekana kuwa duni kuliko ya babake Betty na Mabo Kelfy. Ni kutokana na hali ya kutamauka ambapo Asisi alimwomba Mungu alete mageuzi (uk.36). Ombi hili linaloashiria kutamauka kwa maskini linaingiliana vizuri na mtazamo wa Marx kuhusu dini kwamba ni mpumuo wa kiumbe anayekandamizwa au dawa ya kutuliza akili — afyuni ya watu.

Hali hii (ya kutamauka) inafuatwa na mchakato wa kutafuta usawa katika jamii. Mchakato huu unaanza kwa uzinduzi wa wanajamii. Katika jamii inayotawaliwa na mfumo wa ubepari, ni muhimu kuchunguza namna uzinduzi unavyoendelezwa ili kufaidi matabaka kinzani yaliyomo katika jamii husika. Kwa mujibu wa TUKI (2013), uzinduzi ni hali ya kumtoa mtu katika kutofahamu jambo au kumfanya mtu awe na habari juu ya jambo fulani. Wanapozinduliwa, wanajamii huwa wamepata mwamko. Mwamko wa jamii huwezesha kudadisi jinsi watu wa tabaka moja wanavyoungana ili kupambana na nguvu za tabaka jingine. Katika hali hiyo, harakati za tabaka linalokandamizwa hunuia kuleta mapinduzi ya kugeuza muundo wa uongozi kwa minajili ya kubadilisha mfumo wa kiuchumi. Katika riwaya ya *Yasinya*, michoro ya bin Kifuja inamzindua Asisi akaona uhalisia wa Mabonde na haja ya kupigana na hali iliyowakumba

Wanamabonde (uk.51). Hata hivyo, hatungetarajia Asisi kama kiwakilishi na mtetezi wa tabaka la wanyonge katika Mabonde kuzinduliwa na bin Kifuja maadamu bin Kifuja alitoka katika tabaka la matajiri. Si ajabu kwamba Asisi alipouona mchoro mmoja mara ya kwanza, alitamani wachoraji wengine wangepewa nafasi ya kuuchora (uk.50). Haya ni mabadiliko ambayo yana nafasi kubwa ya kuleta uongozi bora na usawa katika jamii ya sasa. Aidha, Asisi anazinduliwa na Mkutano wa ushirikiano baina ya Miji Mikuu ambapo anagundua kwamba mabanda ya Kibisuswa yaliyopatikana pale kwao ndiyo yaliyokuwa makubwa mno ulimwenguni (uk.53). Ugunduzi wa Asisi unamfanya msomi wa riwaya ya *Yasinya* kukumbuka makazi ya mabanda ya Kibera (Kibra) nchini Kenya ambayo kwa ukubwa yana nafasi nzuri katika ulimwengu mzima. Haya ni makazi halishi ya kuishi yaliyo muhimu katika kuelezea maisha ya binadamu na hasa tabaka la maskini kwa mujibu wa uhakiki wa ki-Marx. Uzinduzi alioupata Asisi unaonyesha wazi kuwa walioishi maeneo ya kwao walikuwa watu wa tabaka lenye uhitaji mkubwa.

Akiwa jela, Kijasiri aliwazindua Liwazo na Kipokeo walipokwenda kumtembelea. Akirejelea mwito wa Asisi kuhusu uhuru, Kijasiri aliona kwamba Wanamabonde waliokuwa maskini ndio waliohitaji kufunguliwa na wala sio yeye. Alisisitiza kwamba yeye alikuwa na fikra zake huru. Kauli hizi zinamaanisha kwamba waliohitaji uhuru ni waliokuwa wachochole katika jamii ya Mabonde na kwamba uhuru kamili wa mtu ni uhuru wa kimawazo. Baada ya kuzinduliwa, Liwazo anaanza kutambua kwamba nguvu za mtu ni nafsi yake, sio pesa wala ulivyonavyo. Kipokeo naye anapata ari, mwito na nguvu mpya za kupigania malengo na kuendeleza mapambano dhidi ya utawala dhalimu wa Chifu Kifuja (uk.125).Katika riwaya ya *Mwanasiasa*, Mwarupia na Mwatua wanazinduliwa na Changawa anapotoa pendekezo kwa suluhisho la matatizo yanayotokana na utawala dhalimu wa Bwana Mkubwa. Akikabiliana na hali ya kutamauka kwao, Changawa anawaambia wawili hawa kwamba kuna suluhu katika kila jambo. Aidha, alipendekeza kwamba Mwarupia ajitose katika siasa maadamu ndiye aliyefahamu shida za watawaliwa walalahoi (uk.41-42).

Katika mikutano yake ya kisiasa, Mwarupia analizindua tabaka tawaliwa kwa kulionyesha kilichosababisha tabaka hilo kunyanyaswa na tabaka tawala. Anasema kwamba tatizo kubwa la Wanabonde ni unyonge wao wa moyo: Unyonge wa kukosa imani kwamba jambo fulani linawezekana. Aliendelea kusema kwamba Wanabonde hawangeweza kupata usawa katika hali yao ya unyonge. Kulingana na Mwarupia, unyonge wa Wanabonde ulitokana na imani ya kidini kwamba Mungu yupo na angewasaidia. Mwarupia aliamini kwamba Mungu hawezi kukusaidia katika kila jambo na kwamba atakupa kidonda iwapo utamtupia kila mzigo akusaidie (uk.118)

Aina ya unyonge mwingine aliouzungumzia Mwarupia ni unyonge wa umaskini. Tabaka tawaliwa la waliokuwa wengi katika jamii ya Bondeni lilikubwa na ukata si haba. Hata hivyo, Mwarupia aliwazindua wanajamii waamini kwamba wangeweza kufaulu katika kupigania unyonge huu na hatimaye usawa kupitia umoja wao, nguvu na akili zao za kuzaliwa. Aliwaambia wanabonde kwamba usawa hauombwi bali hupiganiwa (uk.118).

Kutokana na ukandamizaji unaoendelezwa na tabaka tawala kwa tabaka tawaliwa, Wanabonde wanajawa na mwamko wa kutaka kujikomboa. Mwamko huu unazua makabiliano baina ya matabaka. Makabiliano haya yanatokana na juhudi za tabaka tawaliwa zinazolenga kujikomboa huku tabaka tawala likipinga juhudi hizo hasa kupitia asasi za kiutawala — polisi, magereza na majeshi. Katika mfumo wa kiuchumi wa ubepari, asasi hizi hutumiwa kudumisha jamii za kitabaka kwa kukandamiza tabaka tawaliwa ili litii tabaka tawala. Kwa kurejelea riwaya ya *Yasinya*, tunamwona Asisi (mtetezi wa wanyonge) akifungwa jela kwa tuhuma ya kumuua mhadhiri wa chuo kikuu pamoja na kumtishia Deni (mwanafunzi wa kike) kwa kumwita muuaji (uk.57). Aidha, Asisi anafungwa jela baada ya yeye na Kijasiri kuandaa maandamano kupinga ukiritimba ambapo mtu binafsi (Kifuja) anapewa fursa ya kubeba abiria katika jiji huku wengine wakizuiliwa (uk.64). Anao naye, japo anatoka tabaka la matajiri, anaunga mkono tabaka linalodhulumiwa. Yeye anatiwa mbaroni na kufunguliwa mashtaka kwa sababu ya kupinga njama za Kifuja, Mayowe na babaye kuendesha biashara za mbao pamoja na kutozwa kodi kwa wanajamii bila kupewa huduma muhimu kama umeme, maji ya mabomba na barabara nzuri (uk.82).Kwa vile Asisi alikuwa kiongozi wa kundi lililotetea haki ya wadhulumiwa wa Mabonde, yeye alikwenda kufuatilia kesi ya Anao. Katika tukio hilo, alikamatwa pamoja na wengine kama vile Kipokeo na wakashtakiwa kwa makosa ya kuvamia korti na kuhatarisha usalama wa wananchi wanaoitwa waaminifu na ambao walikuwa wakihudhuria kesi za wapendwa wao. Vilevile, walishtakiwa kwa kosa la kudharau mahakama (uk.83-84).

Katika riwaya ya *Mwanasiasa*, asasi ya polisi inatumiwa kumtia Mwarupia (mtetezi wa wanyonge) mbaroni ili kumdhibiti asiendelee kulichochea tabaka tawaliwa likose kutii utawala wa Bwana Mkubwa. Hata hivyo, waliomkamata walichelewesha kumfungulia mashtaka (uk.114). Akiwa kizuizini, Mwarupia alipitia mateso mengi. Baadhi ya mateso hayo ni kuchomwa mwilini kwa sigara yenye moto, kuvutwa sehemu zake za siri kwa kutumia mpira wa kuvutika, kufungiwa kwenye kichumba kidogo kilichokuwa na giza totoro na punde kupofuliwa kwa mwangaza mkali, kuwekwa kwenye kijichumba finyu chenye maji baridi ambapo alilala na kwenda haja, kupelekwa kwenye msitu mkubwa wakati wa usiku na kuning’inizwa

kichwangomba akiwa uchi wa mnyama huku akiachwa hapo hadi karibu usiku kucha. Aidha, Mwarupia alicharazwa mijeledi, akazabwa makofi na hata kunyimwa chakula kwa siku kadha (uk.115). Katika maandamano ya watawaliwa wanyonge yaliyolenga kumng'oa Bwana Mkubwa mamlakani, askari walitumia bakora, fimbo na hata bunduki kukabiliana na maandamano hayo (uk.121). Tukichunguza mataifa mengi, tunaona uhalisia huu ambapo walio mamlakani wanatumia asasi hizi za utawala ili wazidi kubaki mamlakani. Wapingao serikali tawala wamekuwa wakitishwa, kuteswa na hata wakati mwingine kuuawa.

Isitoshe, Bwana Mkubwa alitumia vyombo vya habari ili kudhibiti utawala wake mbaya na hivyo basi kudumisha matabaka katika jamii. Alifanya hivvo kwa kuhakikisha kwamba taarifa zilizosomwa na kuandikwa kwenye vyombo vya habari ambavyo vilikuwa chini ya himaya yake, vingetangaza na kuandika yaliyokuwa mazuri kumhusu yeye.Waliokwenda kinyume na matakwa au msimamo wa Bwana Mkubwa hawangesikizwa. Vichwa vyote vya taarifa kuu vilianza na Bwana Mkubwa na picha ya mbele katika magazeti kila mara ilikuwa yake akisalimiana na "watu wake" au akifanya chochote kwa Wanabonde. Mamwinyi waliotabasamu walimzingira. Bwana Mkubwa alitumia vyombo vya habari kuhakikisha kuwa Wanabonde wamemjua na kumtambua yeye tu ili kujenga taswira yake akilini mwao (uk.45).

Masuala ya kiuchumi na kisiasa ni miongoni mwa masuala yanayoangaziwa katika nadharia ya u-Marx wa kirasimi na tungo za kihalisia. Hatukosi kuona kwamba harakati za kujikomboa kwa Wanabonde watawaliwa na wanaodhulumiwa ni za kisiasa na pia kiuchumi. Katika harakati hizi, Mwarupia na wafuasi wake wanaukosoa na kuupinga utawala wa Bwana Mkubwa huku Mwarupia akitafuta kuungwa mkono katika kumng'oa Mwasefu (Mjumbe wa Wanabonde) mamlakani. Dhuluma kwa Wanabonde wachochole zinapozidi kiasi cha kutovumilika, wanajamii hawa wanaanza kutumia mbinu nyinginezo — ikiwemo ya kuhujumu uchumi wa nchi — kwa lengo la kuuporomosha utawala dhalimu wa Bwana Mkubwa. Tunaiona mbinu hii ikiwa muhimu katika kuwasilisha uhalisia wa maudhui. Hujuma hii hasa ililenga biashara zilizolinufaisha tabaka tawala. Ni uhalisia kwamba kuna mataifa mengi ambayo yamejikomboa kutoka uongozi dhalimu kwa kutumia mbinu hii. Si nia yetu kutoa mifano lakini baada ya uchaguzi wa kitaifa wa mwaka wa 2017 (uliokumbwa na utata) nchini Kenya, wapinzani wa serikali iliyokuwa mamlakani waliitaja hii kama mbinu mojawapo ambayo kwayo wangeishurutisha serikali kukubali matakwa yao.

Katika tungo za kiuhalisia, wahusika hutenda mambo kutokana na jinsi wanavyochochewa na hali waliyomo. Hali ya tabaka tawaliwa kutovumilia masaibu ya umaskini na ukandamizwaji

ndiyo inayosukuma tabaka hili lifikie kuamua kuuhujumu uchumi wa nchi ili viongozi wabaya waone ugumu kuitawala nchi na hatimaye wakubali kurekebisha maovu katika utawala wao, wang'atuke au waondolewe mamlakani kwa nguvu. Katika riwaya ya *Mwanasiasa*, hujuma ya kiuchumi inaendelezwa wakati watawaliwa wanasusia kununua bidhaa kutoka kwenye maduka ya tabaka la matajiri walioishi Mwananyamala. Kwa mfano, wanasusia kununua sukari — kiungo muhimu cha chai — kutoka kwenye maduka hayo na kuamua kunywa togwa. Aidha, wanaamua kusaga nafaka zao kwa kutumia kisago badala ya kuzipeleka kwenye vinu vya kusagia. Wanakata mifereji iliyopeleka maji kwa mabwanyenye huku pia wakiziba mabomba ya majitaka na kusababisha majitaka hayo kufurika na kutoa uvundo. Licha ya hayo, wanawashawishi walinzi wanaolinda majumba ya kifahari ya mabwanyenye ili watoe taarifa za ujasusi za waajiri wao ambazo zinawezesha kutekeleza matendo ya kijambazi katika majumba hayo (uk. 111).

Ukombozi wa Wanabonde maskini haungepatikana pasipo umoja wao. Umoja wa wadhulumiwa hawa unaonekana pale ambapo waliomuunga mkono Mwarupia walimsaidia kuepuka njama ya utawala wa Bwana Mkubwa iliyolenga kumkamata. Walipopata fununu ya lengo hili, ujumbe ulitumwa kwa Mwarupia asikaribie nyumbani ili aepuke kutiwa mbaroni na makachero waliokuwa wakipiga doria karibu na nyumba yake (uk.114). Aidha, umoja huu unaonekana katika maandamano yao wakipinga utawala wa Bwana Mkubwa. Msimulizi anatuarifu kwamba hakuna mkaazi wa viamboni aliyetaka kuachwa nyuma (uk.120). Katika azma ya kupindua utawala wa Bwana Mkubwa, waandamanaji hawa walifululiza hadi katika eneo la Ngomeni kulikokuwa na kasri la Bwana Mkubwa. Tunaona umoja wao wanapokabiliana na askari waliokuwa wamejihami wakilinda kasri hili. Katika makabiliano yaliyosababisha umwagikaji wa damu na vifo, baadhi ya askari waliona kwamba mashambulizi ya askari kwa bunduki yakilenga walioandamana hakikuwa kitendo cha haki. Kwa sababu hii, walikataa kutii amri ya kamanda wao na wakajiunga na Wanabonde wengine kuzuia kukamatwa au kuuawa kwa Mwarupia, aliyekuwa kiongozi wa waandamanaji (uk.121). Katika hali hii, tunaona utawala ukijiharibu wenyewe. Hatimaye, waandamanaji walifaulu kuupindua utawala dhalimu wa Bwana Mkubwa ambapo Mwarupia alichukua usukani wa kuitawala Bondeni katika utawala uliozingatia usawa wa Wanabonde wote (uk.120-125).

Katika riwaya ya *Yasinya*, juhudi za wanajamii wanyonge za kupinga utawala unaowakandamiza ni hafifu na hazijitokezi waziwazi. Hata hivyo, msomi Alua anapendekeza sheria za Mabonde zibadilishwe kwa kuwa ni za zamani sana. Kwa kiwango kikubwa, juhudi zinazoonekana katika

riwaya hii zinalenga kuzima mbinu ambazo kwazo baadhi ya wanajamii hususan waliokuwa mamlakani wanavyojinufaisha kwa njia zisizo za haki. Kama u-Marx wa kirasimi unavyoeleza, mbinu za aina hii hujitokeza sana katika mfumo wa ubepari huku zikiimarisha tofauti za matabaka. Mbinu hizi ni kama vile ukiritimba na ubinafsi, uendeshaji wa biashara haramu, utozwaji kodi kwa biashara ndogo, utozwaji kodi bila kutoa huduma muhimu, unyakuzi wa ardhi, ulaghai, ajira za watoto kutoka tabaka la maskini miongoni mwa nyingine. Walio katika mstari wa mbele kupinga maovu ya kujiendeleza kupitia njia zisizo za haki ni Asisi, Kijasiri na Sifichi kupitia mashirika ya kibinadamu. Utawala wa Chifu Kifuja unakabiliana na wapinzani wake lakini hatimaye, mabadiliko ya haraka yanatarajiwa kutokea katika utawala wa Mabonde baada ya kifo cha ghafla cha Chifu Kifuja.

### 2.4 Hitimisho

Katika sura hii, lengo ambalo limeongoza utafiti wetu ni kuhakiki maudhui, kutathmini uhalisia wake na kuonyesha kiasi cha kuhusiana kwa maudhui hayo na suala la mgawanyiko wa jamii kitabaka katika riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa*. Masuala mengi na yanayolingana katika riwaya zote mbili yameshughulikiwa. Tumechambua maudhui matatu. Maudhui haya ni umaskini na utajiri, ubaguzi na mchakato wa kutafuta usawa katika jamii iliyogawika kitabaka pamoja na nafasi ya dini katika mfumo wa kitabaka. Miongoni mwa masuala muhimu ambayo tumejadili katika uchanganuzi wa maudhui haya ni usawiri wa makazi ya matabaka yaliyomo katika jamii, umilisi wa rasilimali muhimu za kuzalisha mali, kujinufaisha kwa baadhi ya wanajamii kwa njia zisizo za haki, mchango wa asasi za kiutawala katika kudumisha matabaka, kutamauka kwa tabaka la wachochole, uzinduzi, umoja wa matabaka, maandamano ya wanyonge na mapinduzi. Katika riwaya hizi, maudhui makuu ya mgawanyiko wa jamii kitabaka ni umaskini na utajiri. Kwa mujibu wa tungo tulizozihakiki, haya ndiyo maudhui yanayochukua nafasi kubwa katika historia ya binadamu ambayo Marx alisema hutawaliwa na migongano na mivutano ya kitabaka inayoletwa na hali ya kiuchumi na kisiasa. Katika kiwango cha wastani ni maudhui ya ubaguzi na mchakato wa kutafuta usawa katika jamii iliyogawika kitabaka. Maudhui yanayoonekana kuchukua kiwango cha chini katika uchanganuzi wetu ni yale yanayohusu nafasi ya dini katika mfumo wa kitabaka. Matokeo haya ni bayana kutokana na kiasi cha mifano na maelezo yaliyotolewa kuyahusu maudhui hayo. Maudhui makuu yametolewa mifano mingi na maelezo mapana huku maudhui madogo yakitolewa mifano michache na maelezo finyu.

Kwa kiwango kikubwa, maudhui katika riwaya hizi yanahusiana. Kwa mfano, maudhui yaliyoshughulikiwa katika riwaya hizi yametokana na hali zinazohusiana za kisiasa na kiuchumi

za wanajamii zilizojikita katika historia ya jamii husika. Japo yanahusiana, kuna masuala ambayo yametiliwa mkazo katika riwaya moja kuliko riwaya nyingine. Hivi si kumaanisha kwamba mwandishi fulani ana udhaifu bali ni hali inayosababishwa na yale aliyokusudia kutilia mkazo. Kwa mfano, tofauti na riwaya ya *Mwanasiasa*, riwaya ya *Yasinya* haikuweka mkazo katika suala la uzinduzi wa jamii, maandamano na mapinduzi kama ambavyo ingetarajiwa katika uhakiki uliojikita kwenye nadharia ya u-Marx wa kirasimi. Kutokana na hali hii, harakati za kujikomboa kwa jamii zinaonekana kuwa finyu. Japo mwandishi wa *Yasinya* ametuchorea picha inayofichua maovu katika jamii, hatuoni picha kamili inayojumuisha jamii nzima katika harakati za kurekebisha maovu hayo. Vilevile, suala linalohusu makazi limeelezwa kwa kina kubainisha matabaka katika riwaya ya *Mwanasiasa* kuliko katika riwaya ya *Yasinya.* Maudhui ambayo hayajashughulikiwa kwa undani bado yana umuhimu katika kusawiri hali ya kugawika kwa jamii kitabaka.

Mintarafu ya fasili ya dhana 'tabaka' na 'bwanyenye' katika sura ya kwanza, ni muhimu kueleza iwapo matabaka yaliyobainishwa na nadharia ya u-Marx wa kirasimi ndiyo yanayoakisi muundo wa jamii pana ya kisasa inayowakilishwa katika riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa.* Kama tulivyoeleza, Marx alitambua kuweko kwa matabaka aina sita katika jamii ya kibepari: La wafanyakazi, la matajiri (mabwanyenye), la kati, la waliotengwa, makabaila na wakulima. Alisema kwamba kati ya matabaka haya, tabaka la mabwanyenye na wafanyakazi (maskini na wauza nguvukazi) ndiyo yaliyokuwa matabaka makuu katika jamii ya kibepari. Kwa mujibu wa utabiri wake, maskini na matajiri ndiyo yangebaki matabaka mawili makuu na kinzani baada ya maendeleo ya jamii (Marx na Engels 1998).

Tukirejelea fasili ya dhana ya 'bwanyenye' tunaona kwamba japo jamii imegawika kitabaka katika riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa* hatubainishiwi waziwazi matabaka mawili makuu kama yale yaliyozungumziwa na Marx katika enzi za kuibuka kwa ubepari. Ingawa kuna matabaka ya matajiri na maskini na ndiyo makuu katika jamii inayowakilishwa na riwaya teule, tabaka la matajiri linajumuisha walio mamlakani, ukoo wao na washirika wao. Kwa upande mwingine, watawaliwa ndio wanaounda tabaka la maskini. Hali hii ni tofauti na ilivyokuwa Ulaya wakati wa kuibuka kwa ubepari ambapo matabaka mawili makuu yaliwahusu mabwanyenye walioanzisha ubepari na kuendelea kuudhibiti kisiasa na kiuchumi kwa kumiliki njia kuu za uzalishaji mali huku tabaka la wafanyakazi likiwahusisha walioajiriwa na mabwanyenye hao. Kutokana na maelezo hayo, tungetaka kusema kwamba maana inayorejelewa na dhana za 'bwanyenye' na 'mwinyi' kama zilivyotumikakatika riwaya teule nitajiri. Ijapokuwa

utajiri unafungamana na maana ya dhana hizi katika enzi za kuibuka kwa ubepari huko Ulaya, hatuoni usawa wa kimaana unaotokana na matumizi ya dhana hizo kwa sasa na katika karne ya 18.

Zaidi ya utelezi wa kimaana (tulioeleza) wa dhana muhimu zinazohusiana na u-Marx wa kirasimi, tungetarajia tungo zetu teule, kwa misingi ya nadharia husika, kushughulikia kwa kina mgogoro wa kitabaka baina ya waajiri matajiri na wafanyikazi wauzao nguvukazi zao. Katika jamii zinazotawaliwa na mfumo wa kibepari, chanzo cha mgogoro wa aina hii hasa huwa ni malalamiko kutokana na mishahara duni inayolipwa wafanyakazi huku waajiri wakikataa kuiongeza. Kinyume na matarajio yetu, mgogoro mkuu ulioendelezwa katika riwaya tulizozihakiki (hususan *Mwanasiasa*) ni baina ya tabaka tawala na tabaka tawaliwa. Mgogoro huu unaletwa na uongozi mbaya — uongozi ambao kwa jumla, umesababisha kuzorota kwa maendeleo na hatimaye umaskini mwingi kwa watawaliwa huku wenye mamlaka wakinawiri kiuchumi. Kwa hivyo, kilio cha wanajamii maskini kwa jumla hakitokani na mishahara duni na kutoongezwa kwake bali ni utawala mbaya. Kwa mfano, katika riwaya ya *Yasinya*, Kipokeo analalamika kwamba viwanda vimefungwa kutokana na gharama ya juu ya uzalishaji iliyosababishwa na barabara mbovu (uk.21). Kwa sababu hii, mhusika huyu anajitetea kutokana na maisha yake ya ukahaba. Anadokeza kwamba ukosefu wa ajira ndio umemwingiza katika mkondo huo wa maisha. Hata pale ambapo suala la uajiri limetajwa, hatuoni kisababishi cha mivutano baina ya mwajiri na mwajiriwa kikiwa kutaka kuongezwa mshahara. Kwa mfano, tunaelezwa katika riwaya ya *Yasinya* (uk.19) kwamba kuna wakati Asisi aliacha kazi kwa sababu ya ujira duni lakini hakukuibuka mvutano baina yake na mwajiri wake huku Asisi akitaka kuongezewa mshahara naye mwajiri akikataa kufanya hivyo.

Badala yake, Asisi alilalamika tu baada ya kuacha kazi na bila kuwepo kwa mwajiri wake. Kipokeo naye (riwaya hiyo hiyo) hakuacha kazi kutokana na ujira duni bali ni kwa sababu ya kutumiwa vibaya kimapenzi hasa na mwajiri wake (uk.22). Aidha, riwaya ya *Yasinya* (uk.79), inaeleza kwamba babake Kipokeo alimfanyia Abdul kazi kwa miaka mingi bila kupata mshahara mzuri. Hatuelezwi iwapo malipo hayo duni yaliwahi kuzua mvutano wowote baina ya babake Kipokeo na mwajiri wake. Vilevile, riwaya ya *Mwanasiasa* (uk.14) inatueleza kuhusu maskini wa Bondeni ya viamboni ambao waliwafanyia kazi matajiri walioishi Bondeni mpya huku wakilipwa mshahara duni na kudharauliwa lakini japo mshahara huu pia haukulipwa kwa urahisi, hatuoni wakichukua hatua yoyote ya kupinga hali hiyo kama tunavyotarajia kwa mujibu wa nadharia ya u-Marx wa kirasimi. Badala yake, walijituliza mioyo kwa imani ya kweli

kwamba mtaka cha mvunguni sharti ainame. Ni kwa sababu hizi ambapo tunasema kwamba usawiri wa matabaka makuu na hata mgogoro katika jamii ya sasa ni tofauti na jinsi Marx alivyoeleza katika enzi za kuibuka kwa ubepari. Kwa mujibu wa utafiti huu, hatuna budi pia kusema kwamba matabaka aliyoyazungumzia Marx hayana nafasi ya kuzua mivutano ya kuwezesha jamii kuendelea ili kufikia ukamilifu wa kinjozi kupitia ngazi za kiuchumi: ujima, utumwa, umwinyi, ubepari, ujamaa na kisha ukomunisti.

Ingawa mgogoro mkuu katika riwaya teule ni tofauti na uliokuwako wakati wa kuibuka kwa ubepari huko Ulaya, hivi si kumaanisha kwamba hakuna ubepari unaoendelezwa katika riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa*. Hata hivyo, mfumo wa kiuchumi uliopo katika jamii zinazowakilishwa na riwaya hizi unaonekana kuwa ubepari uchwara. Mtazamo huu ni bayana kutokana na mifano mingi tuliyoitoa katika uchambuzi wa maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka. Kwa mfano, tabaka la wachache, hasa matajiri walio mamlakani ukoo wao na washirika wao, linaonekana likimiliki njia kuu za kuzalisha mali. Matabaka yale mengine yaliyotajwa na Marx yana wawakilishi wao lakini kutokana na ufinyu wa maendelezo yake na uchache wa wahusika waliotajwa, hayabainiki kama makundi ya watu walio na sifa sawa za kiuchumi zinazowatambulisha. Kwa mfano, tunaona Mwarupia (katika riwaya ya *Mwanasiasa*) kama mwakilishi wa tabaka la kati huku kahaba Aisha na watoto ombaomba katika *Yasinya* wakiwakilisha tabaka la waliotengwa katika jamii. Tabaka la wakulima halidhihiriki pengine kwa sababu watu wengi wamebaki maskwota baada ya kunyang’anywa mashamba na matajiri au wenye uwezo wa kisiasa. Kutokana na dhuluma hizi, huenda pia ikawa tabaka hili limejiunga na tabaka la wafanyikazi wanaouza nguvukazi kama hatima yao ilivyotabiriwa na Marx. Kwa hivyo, hatuwezi kusema kwamba matajiri wanaomiliki mashamba makubwa ndio wanaounda tabaka la wakulima kwa sababu tabaka hili kwa mujibu wa Marx na Engels huwa ni la watu waliotapakaa na wasio na uwezo wa kupanga na kuleta mabadiliko ya kijamii na kiuchumi. Vilevile, tabaka la makabaila halijabainishwa kupitia umilisi wa rasilimali za kupangisha. Ingawa kuna majumba ya kifahari yaliyojengwa katika eneo la Bondeni Mpya (riwaya ya *Mwanasiasa*) hatujulishwi kuhusu shughuli za kuzalisha mali zinazohusiana na majumba hayo na tabaka hili.

Kwa kiwango kikubwa, uhalisia wa maudhui umejitokeza kwa kuwa masuala yaliyomo yanapatikana katika jamii ya sasa. Kwa mfano, uhalisia huu unadhihirika wazi katika maelezo yanayohusu makazi halisi ya matabaka yaliyomo katika jamii. Kwa mujibu wa maelezo katika tungo ambazo tumehakiki, haya ni mazingira yanayoonekana. Kwa kiwango kikubwa, mandhari

ya mahali yaliyoteuliwa katika riwaya teule yanaakisi maisha halisi ya jamii pamoja na mgawanyiko wa jamii katika matabaka ya matajiri na maskini. Matukio katika kazi hizi yamekitwa katika wakati na mahali halisi. Mandhari ya kiwakati yanayoelezea vipindi vya kihistoria ambapo misingi ya utabaka katika jamii iliwekwa na kuendelezwa yamefafanuliwa japo si kwa namna inayoakisi wakati maalum. Suala la kujiendeleza kwa baadhi ya wanajamii kwa njia zisizo za haki linaakisi uhalisia maadamu kutokana na hali, mitazamo na matendo ya waliomo katika tabaka la matajiri, tunadhihirishiwa mwonoulimwengu wao uliojikita katika ubinafsi, ubiashara na usokidini kama ilivyokuwa baada ya kutoweka kwa fasihi ya kiramsia.

Changamoto zinazoelezwa katika jamii zinazowakilishwa na riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa* zimo katika mataifa tunayoweza kujitambulisha nayo moja kwa moja. Anwani za riwaya hizi zinadokeza masuala yanayohusiana na utafiti wetu na ambayo yamefungamanishwa vilivyo na anwani hizo. Ingawa majina ya mataifa yanayowakilishwa katika riwaya hizi hayakuwekwa wazi, riwaya ya *Yasinya* inataja mandhari halisi ya mahali nchini Kenya kama Kajiado, uliokuwa Mkoa wa Mashariki, Mlolongo, Nzoia, Namanga *Road* na daraja la Athi *River* katika tukio lililosababisha kufa kwa Chifu Kifuja. Aidha, kisa cha mhusika MA kinaeleza kuhusu marehemu binti yake wa kwanza aitwaye Nyanke. Tunajulishwa kwamba malengo ya binti huyu yalikuwa kuondoa ujinga, umaskini na kupigana na maradhi kupitia mwito wa tuvute pamoja (uk.11). Malengo ya binti huyu ndiyo yaliyosemwa kuwa malengo ya nchi ya Kenya baada ya kujinyakulia uhuru kutoka kwa wakoloni. Mwito wa tuvute pamoja unarejelea mwito wa *harambee*ambao umekuwa maarufu sana nchini Kenya. Kwa maoni yetu, binti anayetajwa, labda ni nchi ya Kenya mara tu baada ya kupata uhuru. Kwa hivyo, mandhari ya riwaya hii yanaweza kuwa ni nchi ya Kenya au eneo fulani katika nchi hiyo. Kwa upande mwingine, mandhari ya riwaya ya *Mwanasiasa* yanarejelea jamii inayoishi pwani, karibu na pwani au kisiwa kilichoko katika nchi za Uarabuni. Hivi ni kwa sababu, msimulizi anataja utawala wa zamani ulioongozwa na sultani ambaye alikuwa kiongozi hususan Uarabuni (uk.12-13). Katika kutoroka kwa Bwana Mkubwa (baada ya mapinduzi), tunaarifiwa kwamba alipanda punda hadi pwani ambako alitumia kihori cha uvuvi kutorokea kwa majirani (uk.122). Aidha, msimulizi anataja makazi ya Maweni katika Bondeni mpya yaliyojengwa kwa mawe ya pwani. Kadhalika, kazi ambayo Semkopi aliwafanyia wenye minazi — ya kuangua nazi na kugema ni shughuli inayohusishwa na mandhari ya pwani hasa pwani ya nchi za Kenya na Tanzania.

Ijapokuwa riwaya teule zina wahusika walio katika harakati za kutatua matatizo yao na ya jamii yao kama inavyopaswa kuwa katika tungo za kihalisia, kuna wahusika ambao wamebuniwa na

kupewa majina ya kimajazi kwa mujibu wa sifa zinazowatambulisha — hali ambayo haiwajengi vizuri kihalisia. Akichangia suala la kutokwenda pamoja kwa majazi na uhalisia, Mbatiah(2016:111) anasema kwamba mbinu ya majazi huwapokonya wahusika upekee unaoakisi majina ya binadamu halisi hivi kwamba majina ya wahusika huishia kuwa viwakilishi vya tabia, mienendo au dhana badala ya vitambulishi vya watu binafsi. Wahusika waliopewa majina ya kimajazi ni kama vile Bwana Mkubwa na Bambua katika riwaya ya *Mwanasiasa*, Kijasiri, Kikwasi na MA katika riwaya ya *Yasinya*.

Kama jina lake lilivyo, Bwana Mkubwa alikuwa kiongozi na ameumbwa kwa kupewa sifa zilizotiwa chumvi kiasi kwamba inaonekana kana kwamba baadhi ya wanajamii walimwabudu kabla ya kuzinduka. Hivi ni kinyume na uhalisia unaoangazia mambo katika ukawaida wake na wala sio kuyatia chumvi (Wamitila 2002:115). Haumtukuzi au kumkweza mtu binafsi na matakwa yake katika ngazi za kijamii kama Bwana Mkubwa anavyofanywa. Hata hivyo, sifa alizopewa Bwana Mkubwa (za kutiwa chumvi) zinaweza kuakisi uhalisia kutokana na unafiki wa watu wanaojitakia makuu kutoka kwa kiongozi huyu hasa kupitia kujiendeleza kwa njia zisizo za haki bila kuchukuliwa hatua yoyote ya kisheria. Mahusiano kama hayo ya kinafiki na kwa sababu zizo hizo yanaweza kuthibitika katika tawala nyingi za ulimwengu wa sasa.

Bambua ni mhusika bapa kielelezo kwa wema wake katika kuwatumikia wanajamii — hususan katika kupiga mbiu. Kihalisia, utumishi wake (upigaji mbiu) unaweza kuhusishwa na utamaduni wa jamii mahususi. Bambua ni kiwakilishi cha tabaka la watu maskini. Iwapo hakuwa na akili punguani, wema wake umekithiri na kuonekana ukikiuka ukawaida wa binadamu. Kwa mfano, japo Bambua angealikwa na kuhusishwa katika kupika vyakula kwenye sherehe, kukosa kula chakula hicho hakukuwa hoja kwake na angeridhika hata alipoambulia ukoko au utandu (uk.3). Tunapoisoma riwaya ya *Mwanasiasa,* tunahisi kwamba huo si uhalisia.

Kikwasi ni jina linalotokana na umilisi wa mali nyingi (ukwasi) na linarejelea mtu aliyekuwa wa tabaka la juu kiuchumi. Kwa upande mwingine, mhusika Kijasiri amepewa jina hili kutokana na sifa yake ya ujasiri hasa katika kukabiliana na dhuluma zinazoendelezwa na tabaka tawala kwa tabaka tawaliwa. Mhusika MA katika *Yasinya,* ambaye ni muhimu katika kuelezea historia ya jamii katika muktadha wa kujengeka kitabaka, anajitokeza kama mhusika asiye halisi. Kwa mujibu wa kisasili katika fasihi simulizi ya jamii ya Mabonde, MA ni nchi au ardhi ya Mabonde. Ni mtu aliyegeuka ardhi baada ya miaka mingi. Ni mhusika asiye halisi anayewakilisha ardhi ya Wanamabonde kama mama wa jamii hasa ya Waafrika (uk.37). Hata hivyo, athari yake kwa

wahusika kama Asisi inaibua matendo na kujenga maudhui ya kisiasa na kiuchumi yanayoonekana kuwa halisi katika jamii ya sasa.

Uwasilishaji wa uhalisia katika hali yake ya kimaendeleo na kimapinduzi umejitokeza wazi zaidi katika riwaya ya *Mwanasiasa* kuliko*Yasinya*. Tofauti ya uwasilishaji wa uhalisia pia imetokana na uteuzi wa mandhari ya mahali, wahusika na matendo yao kama inavyobainika katika riwaya zinazohusika. Kwa ufupi, kiwango cha uhalisia katika riwaya ya *Mwanasiasa* kimepiku kile cha riwaya ya *Yasinya*. Hata hivyo, hatuna budi kusema kwamba riwaya moja ni mwangwi wa nyingine katika kuisawiri jamii ya sasa kitabaka na kihalisia. Aidha, tungo hizi ni mwangwi wa maoni ya wahakiki wengi kwamba uhalisia ndio mkondo tawala katika utanzu wa riwaya. Chembechembe za uramsia katika riwaya hizi hasa kutokana na matumizi ya majazi ni kawaida katika utunzi wa fasihi ambapo aghalabu, masuala ya uhalisia na uramsia huingiliana (Mbatiah 2016:96).

## SURA YA TATU

## FANI NA UWASILISHAJI WA MAUDHUI YA MGAWANYIKO WA JAMII KITABAKA KATIKA RIWAYA ZA *YASINYA* NA *MWANASIASA*.

### 3.0 Utangulizi

Katika sura hii, tunabainisha jinsi fani (kwa jumla) ilivyotumiwa kuwasilisha maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka katika riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa*. Kulingana na Shaw (1905:165), fani hurejelea "namna sehemu za utungo zilivyopangwa — ni mpangilio wa kimuundo wa kazi ya kisanaa". Vinginevyo, fani ni "ujumuishi mzima wa kimuundo wa mawazo na kujieleza". Shaw anaendelea kusema kwamba, "fani katika riwaya hurejelea mpangilio wa matukio na vitushi katika sura au katika mgao wa aina nyingine wa kazi ya kisanaa" (tafsiri yetu). Kwa upande mwingine, Oriedo (2007:18) anasema kwamba fani ni "ufundi ambao msanii hutumia kujenga kazi za sanaa zinazotumia lugha kisanii". Ufundi huo huonekana katika msuko, namna ya kutumia lugha, uteuzi wa mandhari na ukuzaji wa wahusika. Kwa ufupi na katika hali inayoonekana kujumuisha yanayosemwa na Shaw na Oriedo, Said (1995:11) anaeleza fani kama "mbinu ambazo zinatumiwa katika lugha kuyaeleza maudhui". Japo hatupingi maoni ya Shaw kuhusu fani, maelezo yake yameegemea sana muundo — kipengee kimojawapo cha fani huku vipengee vingine vikipuuzwa. Hata hivyo, mitazamo ya hao watatu (Shaw, Said na Oriedo) ni muhimu katika yale tunayochunguza kuhusu fani.

Kama u-Marx unavyotilia mkazo, watafiti wengi walioongozwa na mawazo ya ki-Marx wamejikita katika uchambuzi wa maudhui pekee. Hata hivyo, sisi tunatambua kwamba u-Marx wa kirasimi unaruhusu uchunguzi wa fani, japo kwa ujumla, kutokana na sifa ya nadharia hii kufungamanisha au kukamatanisha masuala mengi kwa pamoja huku ikitilia mkazo kwamba maisha ya binadamu huelezewa zaidi kihalisia na hasa kupitia uhalisiaunaoonekana. Suala hili limetajwa na Wamitila (2002:182) anaposema kwamba u-Marx una sifa ya kijumla ya kuligusia kila eneo na kuwa na la kusema kuhusu takribani kila kitu. Wazo hili pia limechangiwa na Lukac's (1972:4-5) anaposema kwamba mwongozo wa u-Marx huchanganua na kuwazia binadamu na historia ya maendeleo yake kwa ujumla huku ukijishughulisha na matatizo yote maishani (tafsiri yetu). Ni muhimu kuongeza kwamba, kama wanavyosisitiza wasomi wengi, vipengee vya fani na maudhui haviwezi kutenganishwa.

Mchango wa Marx na Engels kuhusu fani unaonekana katika mawazo ambayo yaliishia kuwa sehemu ya uhalisia wa kirasimi katika u-Marx wa kirasimi. Huu ni wakati ambapo

walizungumzia mhusika kifano katika tungo za kihalisia. Kwa mfano, Engels katika (Marx na Engels 1976:90) alieleza uhalisia kama uwasilishi kwa ukweli wa wahusika kifano katika mazingira kifano (tafsiri yetu). Uwasilishi wa uhalisia kikweli umesisitizwa katika mihimili ya nadharia ya u-marx wa kirasimi.Fasili ya Engels kuhusu dhana ya uhalisia na msisitizo wa dhana hiyo katika nadharia husika ni msingi wa uhakiki wa fani katika sura hii.

**3.1 Uchambuzi wa fani kwa jumla**

Tutaanza na wahusika katika jamii iliyogawika kitabaka. Kwa kurejelea Waititu na wenzake (2003:64), wahusika ni "viumbe wanaoumbwa na msanii kimawazo ili kuwakilisha jamii au watu katika kazi ya fasihi. Viumbe hao wanaweza kuwa watu, wanyama, wadudu, miti, mimea au vitu vingine visivyo na uhai lakini hupewa sifa na tabia za watu katika jamii". Waandishi hawa wanaendelea kusema kwamba, "msanii hutumia wahusika katika kazi ya fasihi kuwa viwakilishi vya hali halisi ya maisha ya watu katika jamii anayoizungumzia". Wahusika ndio wanaotumiwa na mwandishi kuwasilisha ujumbe au maudhui kwa hadhira. Akichangia dhana hii (ya wahusika), Msokile (1993:32-33), anasema kwamba "wahusika wanaweza kuwa watu, wanyama, wadudu, mashetani, miungu au vitu katika kazi ya sanaa ya kifasihi. Wao huwakilisha tabia maalumu katika jamii. Tabia hii inaweza kudhihirisha wema au ubaya katika maisha ya watu". Katika fasihi, wahusika huwa wa aina tofauti kutokana na jinsi walivyoumbwa na kukuzwa. Maelezo ya Msokile na yale ya Waititu na wenzake yanalingana kwa vile waandishi hawa wanazungumzia viumbe wanaobuniwa na mwandishi katika kazi ya kifasihi. Hata hivyo, maelezo ya Waititu na wenzake yametufaa zaidi ya mawazo ya Msokile madhali yamefafanua mhusika katika muktadha wa uhalisia ambao ndio mwelekeo wa utafiti wetu. Mintarafu ya kazi hii, ni muhimu kutaja kwamba ubunifu wa wahusika kama wanyama, wadudu, mashetani, miungu na vitu si usawiri wa jamii kiuhalisia.

Mhusika kifano aliyezungumziwa katika u-Marx wa kirasimi ni mhusika anayewakilisha tabaka maalum katika mazingira kifano. Mathalani, anaweza kuwakilisha itikadi ya tabaka hilo. Aidha, mhusika huyu huwakilisha ubinafsi na sifa zake katika mazingira yayo hayo. Riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa* zina wahusika wengi na waliokuzwa kwa namna tofauti. Tutawachunguza wahusika kadha wa kadha ili angaa kubaini uumbaji wao kama wahusika kifano. Tutaanza na Asisi katika riwaya ya *Yasinya*. Mhusika huyu ameendelezwa kutoka mwanzoni mwa riwaya hadi mwisho. Anazungukwa na matendo mengi ya msingi katika riwaya husika. Kiuhalisia, mawazo na matendo yake yanasukumwa na changamoto za kiuchumi zinazosababishwa na

utawala mbaya katika Mabonde. Anasema kwamba motisha yake kuu ni kupigana na njaa, maradhi na umaskini (uk.58).

Kama mhusika kifano, Asisi ni kijana anayeliwakilisha tabaka la maskini hususan watawaliwa. Tunajulishwa kuhusu ufukara wa familia yake kwa kuelezwa kwamba makazi yao yalikuwa katika mtaa duni wa Kibisuswa (uk.53). Ufukara huu ulimpa Asisi changamoto nyingi katika masomo. Kuna wakati alisomeshwa na pesa zilizotokana na kazi duni ya mamake ya kuuza chang'aa (uk.34). Aidha, Asisi alilipa karo ya shahada ya uanasheria kutokana na malipo ya kufanya vibarua (uk.101). Baada ya kuiacha kazi ya kuuza chang'aa, mamake Asisi alianza kuuza mboga na matunda (uk.34). Kwa upande wa vyakula, kuna wakati njaa ilimfanya mama huyu awapikie wanawe maembe na ndizi ambazo kwa kawaida hazikuwa zinapikwa (uk.34). Kukithiri kwa umaskini katika familia ya mhusika huyu kunasisitizwa na hali ya njaa kali iliyompata Asisi alipokuwa uwanjani palipokuwa na maombi ya umma. Tunajulishwa kwamba hakuwa amekula vizuri kwa siku mbili jambo ambalo lilimfanya kuwafikiria masahibu wake ambao walimuauni wakati mwingine alipokuwa na njaa (uk.31-36). Uchochole wa familia yake unaelezewa pia na hali ambapo mamake (Emali) hangeweza kumlipia dhamana au kumtafutia wakili baada ya yeye (Asisi) kukamatwa na kufunguliwa mashtaka (uk.58).

Uwakilishi wa Asisi wa tabaka la maskini pia unaonekana kupitia maelezo yanayoonyesha mtazamo wake kuhusu utabaka. Maelezo hayo yanasema kwamba Asisi hakupendezwa na mfumo ya jamii yake uliojengwa kwa msingi wa kitabaka (uk.23).Kadhalika, Asisi amekuzwa kama mtetezi wa wanajamii waliodhulumiwa na utawala mbaya katika Mabonde. Anapozinduka, mhusika huyu anaishia kuwa kiongozi jasiri wa kundi linalotetea haki ya wadhulumiwa wa Mabonde (uk.83). Aidha, Asisi (pamoja na Kijasiri) wana mradi wa kupigania afya na makazi bora katika jamii ya Mabonde (uk.82). Uendelezi wa mradi huu kwa pamoja unaonyesha sifa ya ushirikiano wa Asisi na watu waliokuwa na maono sawa na yake — maono ya kubadilisha maisha ya watu maskini. Kwa mujibu wa u-Marx wa kirasimi, umoja na ushirikiano huwa muhimu katika kupigania maslahi ya kila tabaka. Hata hivyo, mtazamo wa Marx kuhusu namna ya kuibadilisha jamii na ulimwengu kwa jumla haukulenga uendelezi wa miradi ya kusaidia maskini bali ulilenga kupigania maslahi ya tabaka la maskini hususan wafanyikazi au tuseme wauza nguvu-kazi kutokana na dhuluma walizotendewa na waajiri wao.Katika harakati za kuwatetea maskini wa Mabonde, Asisi alikabiliwa na nguvu kinzani za utawala wa Mabonde. Kwa mfano, alifungwa kwa kuandaa maandamano kupinga ukiritimba — uovu uliomhusisha Chifu Kifuja aliyeiongoza Mabonde (uk.64). Mbinu za kumnyamazisha pia ziliendelezwa kwa

kufungwa jela baada ya kutuhumiwa kumuua mhadhiri wa chuo kikuu pamoja na kumtishia usalama mwanafunzi fulani wa kike kwa kumwita muuaji (uk.57).

Sifa nyingine ya Asisi ni uadilifu. Tunaiona sifa hii baada ya yeye kufichua kashfa katika kiwanda alichokifanyia kazi ambapo bosi fulani alishirikiana na mtu wa nje kufuja mali ya kiwanda hicho. Kutokana na ufichuzi huu, Asisi alifutwa kazi (uk.24). Kadhalika, uadilifu wake unaonekana wakati ambapo alikataa kutoa kwa askari, sehemu ya shamba la marehemu baba yake kama hongo ili askari huyo amsaidie kesi yake imalizike (uk.64). Hii ni hulka nzuri ya mtetezi wa wanyonge katika kukabiliana na uovu wa kujinufaisha kwa njia zisizo za haki katika jamii inayotawaliwa na mfumo wa kibepari. Kwa ufupi, mtu hawezi kupigania maadili iwapo yeye mwenyewe si mwadilifu.

Asisi alikuwa msomi mwerevu na mwenye bidii. Kama kiongozi wa wanyonge, sifa hizi ni muhimu katika kushughulikia matatizo yake binafsi na ya jamii nzima. Ni kutokana na sifa hizi ambapo Asisi (akishirikiana na Kijasiri) aliweza kuanzisha na kuendesha mradi wa kupigania afya na makazi bora hasa ya maskini wa Mabonde (uk.82). Hata hivyo, ushauri wa MA kwa Asisi hauipi elimu nafasi ya kuikomboa jamii. Katika ushauri huu, Asisi aliambiwa kwamba kupata uhuru hakuhitaji mtu kutumia nguvu za ujana na hekima ya dunia kwa kuwa uhuru ni kujituma au kujinyima ili wengine wafaidi (uk.86). Kinyume na ushauri huu, tunaelezwa kwamba ilimbidi Asisi kuvuta hekima yote na elimu ya saikolojia ili kumjibu Chifu Kifuja walipokutana katika eneo lililokuwa na makaburi (uk.89). Sifa za werevu na bidii ni sifa za kibinadamu na ni muhimu pia katika kumsawiri mhusika huyu kiuhalisia. Tunajulishwa sifa hizi kutokana na maelezo kwamba Asisi alizoa alama karibu zote katika mtihani wa kitaifa wa shule za msingi (uk.28). Alisomea shahada mbili: moja ya fasihi na historia na nyingine ya uanasheria (uk.55). Asisi pia alikuwa na lengo la baadaye la kusoma historia na sayansi ya uongozi na utawala (uk.101). Mbali na kuwa na elimu ya chuo kikuu, Asisi alikuwa mwandishi. Kutokana na werevu wake uliotokana hasa na usomi wa fasihi, aliandika riwaya yenye anwani "Kilio Penye Kicheko" (uk.53).Anwani hii inadokeza kuwa kuna masuala ya kijamii yaliyomkera Asisi na ambayo yalikuwa muhimu katika kuyajenga maudhui ya riwaya yake. Mambo hayo ndiyo kiini cha mapambano ya tabaka lake. Kwa maoni yetu, kilio kinachorejelewa na anwani hii ni cha Wanamabonde maskini na wanaodhulumiwa na utawala wa Kifuja huku kicheko kikitoka vinywani vya matajiri wa Mabonde. Bila shaka, riwaya ya Asisi ni muhimu katika kuizindua jamii.

Sifa inayomuumbua mhusika huyu kwa mujibu wa nadharia ya u-Marx wa kirasimi ni kwamba, Asisi hajaiwezesha jamii kufikia maendeleo ya kiuchumi kupitia maandamano na mapinduzi. Kile ambacho ameshughulikia akiwa pamoja na wengine walio na maono sawa na yake ni kuizindua jamii na kuboresha maisha ya maskini kwa kuunda miradi mbalimbali. Kwa hivyo, hatuoni umuhimu wa elimu yake katika kuendeleza jamii kiuchumi kwa namna inayozingatia mtazamo wa u-Marx wa kirasimi. Harakati zake hazijaiwezesha jamii kupata mabadiliko ya kiuchumi. Asisi alikuwa mpenda amani hivi kwamba hakupendelea jamaa ikitumbukia katika ghasia (uk.75). Sifa hii ni bayana kutokana na mtazamo wake kuhusu Kifuja, Mayowe na wengine walioifilisi Mabonde kwa pupa ya mali. Pamoja na Kijasiri, Asisi anasisitiza umoja na maridhiano ya Wanamabonde kupitia wito wa kusameheana madhali hakuna insi aliye mkamilifu (uk.158). Tunahisi kwamba ni kwa sababu hii ambapo hakuna makabiliano ya kufana baina ya tabaka tawala na tabaka tawaliwa. Mtazamo wa u-Marx wa kirasimi kuhusu suala hili ni kwamba wahusika walio na uwezo wa kuleta mabadiliko chanya ya kiuchumi katika jamii ni wale wanaoegemea mitazamo ya kimapinduzi. Hivi ni kutokana na msisitizo wa nadharia husika kuwasilisha uhalisia wa maisha ya binadamu katika hali yake ya kimaendeleo na kimapinduzi (Njogu 1997:13). Asisi hajaumbika kikamilifu kama mhusika wa aina hii. Aidha, kuna wakati anaonekana akiwakilisha nafsi ya vijana badala ya maskini wote kwa jumla. Uwakilishi huu unatokea pale ambapo analalamikia ukosefu wa ajira kwa vijana huku wakisemwa kuwa ndio viongozi wa kesho (uk.34).

U-Marx wa kirasimi unatambua matabaka mawili makuu: mabwanyenye wanaomiliki njia kuu za uzalishaji mali kama vile viwanda na ardhi na wafanyikazi wanaoajiriwa kuwafanyia matajiri kazi hususan katika viwanda. Tuonavyo ni kwamba Asisi hajaumbika kama mwakilishi wa tabaka la maskini waliouza nguvukazi zao ili waishi. Isitoshe, nadharia inayoongoza utafiti wetu hushikilia kwamba tabaka linalodhulumiwa linapaswa kupigania haki zake kwa kuwa tabaka tawala haliko tayari kuleta usawa wa kiuchumi katika jamii bali kuendeleza maslahi yake tu huku likihakikisha kuwa jamii inabakia vilevile — bila kubadilika. Juhudi za kutimiza lengo hili ni hafifu mno katika riwaya ya *Yasinya*. Ijapokuwa mhusika huyu (Asisi) alitoka katika mtaa wa maskini wa Kibisuswa, tunaona kwamba hajakuzwa kikamilifu katika mazingira kifano.

Mhusika aliye na dhima inayoonekana kuwa karibu sawa na ya Asisi katika riwaya ya *Mwanasiasa* ni Mwarupia. Kama Asisi, mhusika huyu amekuzwa kutoka mwanzo wa hadithi hadi mwisho na matukio mengi ya kimsingi yanamzunguka yeye. Kama mhusika kifano, Mwarupia anawakilisha tabaka la maskini. Alifahamu na kusumbuliwa na matatizo ya wanajamii

hususan maskini wa Bondeni ya viamboni. Hata hivyo, mhusika huyu alikuwa ametamauka kabla ya kuzinduliwa na Changawa. Kutamauka kwake kulimnyima uwezo wa kuona suluhu kwa matatizo ya Bondeni. Hiyo ni hali ya kawaida kabla ya mwamko katika jamii iliyogawika kitabaka kutokana na mfumo wa kibepari unaoitawala. Ufahamu wa Mwarupia kuhusu matatizo ya jamii na usumbufu uliotokana na matatizo hayo unaelezwa kupitia maneno ya Changawa anaposema kwamba Mwarupia aliumwa moyoni kwa sababu ya wanyonge kuonewa na wachache wenye nguvu (uk.42). Ni kutokana na athari hii ambapo mhusika huyu (Mwarupia) anaendeleza harakati za ukombozi wa jamii ya Wanabonde inayodhulumiwa na uongozi mbaya. Vinginevyo, tunaweza kusema kwamba, matendo ya Mwarupia yanalingana na yale ya wahusika halisi ambao hutenda kutokana na jinsi wavyochochewa na hali waliyomo (Wamitila 2002:115). Mwarupia alikuwa jasiri. Hii ni sifa muhimu kwa mtetezi wa maslahi ya mtu binafsi na ya tabaka la wanyonge kwa jumla. Tunaiona sifa hii kutokana na jinsi alivyokabiliana na utawala uliojaribu kumnyamazisha hasa kupitia maandamano. Juhudi zake za kuikomboa jamii kutoka utawala dhalimu wa Bwana Mkubwa zilikumbana na upinzani mkali. Kwa mfano, Mwarupia aliteswa sana baada ya kukamatwa na kuwekwa kizuizini. Baada ya kuachiliwa, yeye hakufa moyo bali aliendelea kupigania haki za wadhulumiwa wa Bondeni.

Mwarupia aliyakidhi mahitaji yake ya kimsingi kwa kufanya biashara japo ya kiwango cha chini. Aliuza bidhaa kwa rejareja katika mtaa wa Tuwa Tugawe — mojawapo ya mitaa duni katika Bondeni ya viamboni kulikoishi maskini. Tunaelezwa kwamba aliuza bidhaa zake kwenye kijiduka (uk.40). Uwezo wake wa chini kiuchumi unaonekana pia alipojiunga na siasa ambapo alifanya kampeni zake kwa miguu au kwa baiskeli yake (uk. 48). Hata hivyo, tunaelezwa kwamba mhusika huyu alikuwa katika hali bora kiuchumi kuliko wakazi wengine wa Bondeni ya viamboni.

Kama alivyokuwa Asisi katika riwaya ya *Yasinya*, Mwarupia alikuwa mwerevu hivi kwamba alifanya maamuzi baada ya kufikiria kwa kina. Kwa mfano, tunaelezwa kuwa aliwaza na kuwazua kuhusu kuingia katika siasa (uk.42-44). Kadhalika, alitumia hekima kuwaeleza Wanabonde walionyanyaswa kwamba iwapo wangemchagua, angemaliza udhalimu kutokana na utawala wa Bwana Mkubwa (uk.47-48). Mhusika huyu alikuwa mwenye utu. Hii ni sifa inayomwezesha mja kutambua na kuyakemea maonevu ya binadamu wengine hasa katika jamii iliyogawika kitabaka.Vinginevyo, utu humwezesha binadamu kuwa na maadili—suala mojawapo la kijamii linalohusishwa na nadharia ya u-Marx wa kirasimi. Utu wa Mwarupia ulionekana kupitia moyo wake wa huruma, ukarimu na upendo kwa watu (uk.40-42).

Tunayaelewa haya kutokana na uhusiano wake na wateja wake. Alipotoka gulioni, Wanabonde walijitolea kuzikokota bidhaa zake hadi kijidukani mwake halafu wakaipakua mizigo. Mwarupia aliwajali wateja wake katika biashara huku akiwauzia bidhaa kwa vipimo vya kibaba na mara nyingine kwa bei ya kutupa (uk.40). Mbali na hayo, aliwakopesha watu bidhaa na pesa. Inashangaza kwamba Mwarupia hakuvunjika moyo baada ya baadhi ya watu aliowakopesha kukosa kumlipa (uk.40). Ni kutokana na sifa hizi ambapo msimulizi anasema kuwa kila mtu aliyekutana naye alimwahidi kumuunga Mwarupia mkono katika siasa kwani hakuna akiba nzuri kama wema wa mtu (uk.48).

Kama mhusika kifano anayepaswa kuwa na sifa ya kuendeleza maudhui na uhalisia katika hali ya kimaendeleo na kimapinduzi, tunaona kwamba Mwarupia alipenda maendeleo ya jamii ambapo aliahidi kuijenga upya Bondeni ili kuhakikisha kwamba kulikuwa na usawa miongoni mwa watu ambapo kila mtu alikula jasho lake. Aliitoa ahadi hii baada ya mapinduzi ya uongozi wa Bwana Mkubwa. Tukio hili ni hatua muhimu inayowapa maskini tumaini la kuing'oa mizizi ya unyonyaji na unyanyasaji katika jamii iliyogawika kitabaka. Kama u-Marx wa kirasimi ulivyo, ni tukio linalomsawiri binadamu kama mwenye urazini unaoifanya dunia itengenee na kuwa mahali bora pa kuishi. (Wafula na Njogu (2013: 67).

Sifa zinazomuumbua Mwarupia kama mhusika kifano ni kwamba ingawa anawakilisha tabaka la maskini, tunaona mkinzano katika uwakilishi huu kutokana na maelezo yanayomsawiri kama mtu aliyekuwa na uwezo mkubwa wa kiuchumi kuliko Wanabonde wengi (uk.41). Kupitia kwake, hatuyatambui matabaka mawili makuu yaliyozungumziwa na Marx. Yaani, (kama Asisi katika *Yasinya*) hatumuoni Mwarupia akiwa mtetezi wa tabaka la wafanyikazi ambalo hunyanyaswa na waajiri wao katika mfumo wa kibepari. Kadhalika, lengo la kufanya biashara, kwa kawaida, huwa ni kupata faida. Kwa sababu hii, hatuoni uhalisia tunapoelezwa kwamba Mwarupia aliuza vitu vyake kwa bei ya kutupa huku pia akikosa kuathiriwa na wale ambao hawakumlipa pesa alizowakopesha. Japo msimulizi anachukulia sifa hii kuwa chanya, tunaona kwamba huenda Mwarupia aliyatenda mema haya akiwa na lengo la kuwashawishi watu wamuunge mkono katika siasa. Vinginevyo, tunaona kama mwandishi anajaribu kumuumba kiumbe aliyekamilika kupitia kwa wema wake. Hivi ni kinyume na wanauhalisia wasiotilia mkazo kwenye uzuri na ukamilifu wa kibinadamu kama walivyo wafuasi wa ulimbwende (Wamitila 2003:289).

Mbali na Mwarupia, tunaelezwa kuhusu mhusika aitwaye Semkopi. Mhusika huyu anatajwa tu mwanzoni mwa riwaya halafu anatoweka. Kwa kiwango cha chini, yeye ni mhusika kifano

anayewakilisha tabaka la maskini. Katika mazingira yake kifano (viamboni), mhusika huyu hakuwa na shamba la minazi. Alikuwa mlevi aliyepata riziki yake kwa kuwafanyia watu kazi ya kuangua nazi na kugema tembo. Kutokana na hatari ya kuangua nazi, alijiliwaza kwa kuimba akiwa vileleni vya minazi. Wimbo wake mmoja unaeleza kuhusu kukonda kwake ambako anasema kulisababishwa na mja asiye fadhili (uk.7-8). Ni wazi kwamba kazi ya mhusika huyu na uimbaji wake ni mambo yanayochochewa na hali aliyomo. Shughuli za Semkopi, kukonda kwake na uimbaji ni sifa za binadamu halisi. Aidha, tunaona uhalisia wa mhusika huyu akiwa mlevi ambapo anayumbayumba na kutumia lugha ya kumlazimisha mkewe afungue mlango wakati wa usiku. Ukosefu wa fadhila za waja anaozungumzia Semkopi ni maonevu halisi, hasa kwa maskini, katika jamii iliyogawika kitabaka. Hivi ni kumaanisha kwamba Semkopi alikuwa akidhulumiwa na watu hata alipowatendea mema. Udhaifu wa Semkopi kama mhusika kifano ni kwamba hajakuzwa kwa vyovyote vile kama mtetezi wa wanyonge wengi wanaodhulumiwa katika jamii. Uwakilishi wa nafsi yake na itikadi za tabaka la wanyonge ni finyu mno.

Tukichunguza watoto waliokuwa wakicheza katika mazingira kifano ya viamboni kwa maskini (riwaya ya *Mwanasiasa*), tunaona kwamba watoto hawa wanawakilisha tabaka la maskini. Hata hivyo, wao wanatajwa tu na kutoweka katika usimulizi. Kama tunavyoelezwa, kucheza kwao hakukuwa kwa kawaida. Hakukuchangiwa na raha maishani bali ni kutokana na masaibu waliyopitia. Kama wahusika halisi, kucheza kwao kulichochewa na hali waliyomo. Walicheza ili wajiliwaze kutokana na masaibu yaliyowapata wao wenyewe na pia wavyele wao. Tabia yao ya kuoga kwenye vidibwi vya maji machafu na sifa wanazopewa kama vile kuwa na pua zilizotoka kamasi, matumbo yaliyovimba kutokana na safura au utapiamlo, nywele zilizonyonyoka ovyo, nywele zilizogeuka rangi na kuwa nyekundu, ni sifa za binadamu halisi na watoto katika hali yao ya umaskini (uk.9-10).

Tukimgeukia mhusika Bambua katika riwaya iyo hiyo (*Mwanasiasa*), tunaona kwamba, lau si kile kinaonekana kama kutiliwa chumvi kwa sifa za kibinadamu za utu wake na kutumiwa na utawala uliowanyanyasa wanyonge, mhusika huyu angekuwa mwakilishi mzuri wa tabaka la maskini kupitia kwa mazingira kifano ya kuishi na yanayoonekana. Aidha, Bambua ameendelezwa tu mwanzoni mwa riwaya na hakupewa nafasi yoyote ya kutetea maslahi yake na ya tabaka lake. Kama maskini wa Bondeni ya viamboni, Bambua aliishi kwenye chumba cha msonge kilichokandikwa kwa udongo na kuezekwa nyasi. Tunaelezwa kwamba mlango wa chumba hiki — uliokosa tumbuu — ulikuwa wa kumba za makuti ya mnazi (uk.54). Kitanda chake kilikuwa mkeka. Makazi ya mhusika huyu hayakuwa na choo hivi kwamba alijisaidia

kichakani. Mswaki aliotumia kusugua meno ulikuwa wa mti, nao uliwekwa kwenye mwanya wa ukuta wa chumba chake (uk.56).

Baada ya kuchunguza wahusika waliowakilisha tabaka la maskini, ni muhimu sasa kuwachunguza wahusika waliowakilisha tabaka la matajiri. Katika riwaya ya *Yasinya*, tunakutana na Kifuja aliyekuwa chifu wa jamii ya Mabonde. Mhusika huyu amekuzwa kutoka mwanzo hadi mwisho na usimulizi wa hadithi unamzunguka yeye pakubwa. Kifuja ndiye aliyeongoza Mabonde baada ya chifu aliyeitwa Chebaskwony. Kabla ya kuwa chifu, Kifuja alikuwa mdogo wake Chebaskwony. Ingawa amepewa jina la kimajazi linaloashiria jinsi alivyofuja mali ya umma, yeye ni mhusika kifano anayewakilisha tabaka la matajiri. Uumbaji wake kama mhusika halisi unaonekana kupitia sifa bainishi za binadamu alizopewa. Tunaambiwa kwamba alikuwa na shingo nene, kipaji kipana na upara uliomeremeta. Mikono yake ilionekana kuwa mifupi kwa sababu ya unene wake. Aliifungia suruali yake juu ya tumbo. Isitoshe, alikuwa mchoyo hivi kwamba ilikuwa muhali kuwanunulia walinzi na dereva wake chakula. Kusisitiza uchoyo huu, tunajulishwa kwamba mhusika huyu alielekezwa na mambo mawili tu: tumbo lako na mfuko wako (uk.33).Chifu Kifuja analiwakilisha tabaka lakekupitia utajiri wake katika mazingira kifano ya jamii iliyogawika kitabaka na inayotawaliwa na mfumo wa ubepari uchwara. Mazingira haya yanaonekana yakiwadhulumu walio wengi huku yakiwafaidi wachache hususan wale walio mamlakani. Tunaona utajiri wa Kifuja katika umilisi wake wa njia kuu za kuzalisha mali kama vile, mashamba makubwa. Pia, Kifuja alikuwa mmoja wa wamilisi wa Shirika la Maba ambalo ndilo lililokuwa shirika kubwa sana la bima katika Mabonde (uk.96).

Mhusika Kifuja anaiwakilisha nafsi yake kupitia tamaa nyingi ya mali hivi kwamba mashamba yake mengi yalipatikana kwa njia zisizo za haki. Aliishia hata kunyakua ardhi ya makaburini ili ajenge hoteli (uk.89). Isitoshe, Kifuja alikuwa tapeli. Kwa kushirikiana na Mayowe, waliendesha matbaa bandia ya uchapishaji waliyoitumia kuwatapeli watu (uk.120). Aidha, kiongozi huyu alikuwa mlanguzi wa dawa za kulevya. Sifa hii inadokezwa hata katika tamthilia yake iliyoitwa "Nikiwa Rais" (uk.156-157). Mbali na hayo, tamthilia hiyo inaeleza kwamba iwapo angepata nafasi ya kuwa rais, Kifuja angeiendeleza jamii kwa misingi ya kitabaka. Yanayoeleza hivyo katika tamthilia yake ni picha za wanafunzi waliovuta bangi, vijana wakijiuza katika barabara za mijini, Mayowe akiwa waziri mkuu tajiri sana huku wakulima wakija kukopa kwake pesa za mbolea, mbegu na dawa ya kuua kwekwe (uk157). Kutokana na maelezo hayo, ni dhahiri kwamba Kifuja alikuwa katili. Ukatili wake uaonekana pia wakati ambapo mama mmoja ajuza

alikuwa akipelekwa hospitali kwa baiskeli. Ajuza huyo alitoka katika tabaka la maskini na hakukuwa na namna bora ya kumsafirisha hadi hospitali. Ijapokuwa alikuwa mgonjwa sana, Kifuja hakumwonea huruma akamkimbiza hospitalini kwa gari lake. Alimpuuza, akaingia kwa gari lake na kwenda zake (uk.91). Mbali na hayo, Kifuja alimwona Asisi kama mpinzani wake wa kisiasa, jambo ambalo lilisababishakufungwa jela kwa Asisi (uk.43).

Mhusika anayeweza kulinganishwa na Kifuja katika riwaya ya *Mwanasiasa* ni Bwana Mkubwa. Sawa na Kifuja (katika *Yasinya*), Bwana Mkubwa amekuzwa kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi. Jina hili (Bwana Mkubwa) ni la kimajazi na linadokeza nafasi ya mhusika huyu katika jamii kama mtawala wa jamii ya Bondeni (uk.18). Japo amepewa jina la kimajazi (ili pengine atambulike kwa urahisi), yeye ni mhusika kifano anayewakilisha tabaka la matajiri na wamilisi wa nguvu za kisiasa katika jamii ya Bondeni. Kiuhalisia, ameumbwa kwa kupewa sifa bainishi za binadamu. Kwa mfano, tunaelezwa kwamba alikuwa na umbo la wastani hivi kwamba hakuwa mrefu wala mfupi. Aidha, alikuwa na kitambi cha wastani. Msimulizi anasema kwamba huenda kitambi hiki kilitokana na umbo lake au mali aliyokuwa nayo (uk.24). Mavazi yake yanayotajwa kama vile kofia nyeusi ya tarbushi ilitumika kuficha mvi kichwani ambao aghalabu ni ishara bainishi ya umri mkubwa wa binadamu. Mavazi yake ya kanzu nyeupe ya hariri na joho ni mavazi yanayotumiwa na binadamu. Mikono yake (ambayo ni viungo vya binadamu halisi) ilitumika kushikilia mgwisho na bakora (uk.23). Kama inavyopaswa kuwa katika tungo za kihalisia, uumbaji wa mhusika huyu unajenga taswira yake katika akili ya msomaji.

Bwana Mkubwa analiwakilisha tabaka lake katika hali yenye mgogoro wa kisiasa na kiuchumi unaosababishwa na utawala wake mbaya. Hali hiyo imejaa joto la kisiasa kutokana na juhudi za kujikomboa za watawaliwa wanaolalamikia viongozi waliopuuza majukumu yao. Kama tulivyoeleza katika sura ya pili, mazingira kifano ya mhusika huyu yanaonekana kupitia makazi yake ya kifahari. Utawala wa Bwana Mkubwa ulibagua baadhi ya wanajamii hivyo basi kuchangia katika kuendeleza mfumo wa kitabaka. Kiongozi huyu alikuwa na ushawishi mkubwa wa kisiasa na kiuchumi Bondeni hivi kwamba Wanabonde walimwogopa. Utawala wake ulikuwa wa ki-imla. Tunajulishwa haya baada ya Mwarupia kukosa kutoa mchango wa pesa kwa matayarisho ya mkutano wa Bwana Mkubwa ambapo Mwaakida anamwambia: “Hii ni amri kutoka kwa Bwana Mkubwa na hakuna anayestahili kuikiuka hata kidogo” (uk.38).

Mtawala huyu (Bwana Mkubwa) anawakilisha nafsi yake hasa kupitia hila nyingi za kisiasa alizotumia ili kuendelea kushikilia mamlaka Bondeni (uk.45-47). Kwa mfano, alitumia vitisho kuwanyamazisha wapinzani wake. Akiwa katika mkutano, Bwana Mkubwa alisema:

"...atakayetuchezea na kujaribu kuivuruga amani yetu, tutampondaponda kiasi cha kutoweza kusimama" (uk.80). Kwa mujibu wa u-Marx wa kirasimi, hila za aina hiyo ni kawaida katika jamii iliyogawika kitabaka ambapo tabaka la walio mamlakani hung'ang'ania kushikilia mamlaka kwa vyovyote vile ili kuendelea kuudhibiti mfumo wa kitabaka.

Mbali na wahusika, tunachunguza usimulizi na msuko katika riwaya za kihalisia**.** Usimulizi ni dhana inayorejelea jinsi matukio yanavyoelezewa katika hadithi. Kuna aina nyingi za usimulizi. Aidha, kunaweza kuwa na mwingiliano wa aina mbalimbali za usimulizi katika kazi ya kifasihi. Usimulizi uliopo katika riwaya tunazohakiki ni wa nafsi ya tatu, nao ndio umezoeleka sana katika uandishi wa fasihi. Mbali na usimulizi huu, kunao pia matumizi ya nafsi ya kwanza hasa katika mazungumzo ya moja kwa moja baina ya wahusika. Katika usimulizi wa nafsi ya tatu, anayesimulia hadithi huelezea matukio au mambo yanayomhusu mtu mwingine. Kwa kawaida, usimulizi wa nafsi ya tatu katika tungo za kihalisia huendelezwa na msimulizi maizi ambaye kwa mujibu wa *Cambridge Academic Content Dictionary*, ni sauti ambayo kwayo hadithi imeandikwa hivi kwamba sauti hiyo iko nje ya hadithi na inajua kila kitu kuhusu wahusika na matukio katika hadithi (tafsiri yetu). Inavyosema kamusi hii ni kuwa sauti hiyo si ya mhusika na kwamba msimulizi huyu (aliyeteuliwa na mwandishi) ana uwezo wa 'kupenya' katika akili na mioyo ya wahusika huku akiyafichua mambo yote yanayowahusu. Kwa ufupi, msimulizi huyu hujikita katika kile kinachoitwa usimulizi maizi. Kutokana na nduni hii (ya usimulizi maizi), tungo za kihalisia huwa na usimulizi wa kina wa matukio na uhusika.

Zaidi ya usimulizi maizi, tungo za kihalisia huegemea usimulizi wa kimuhakati. Hivyo ndivyo wanavyodokeza Harriet na Adelaida (2003:81) wanaposema kwamba, wafikiriapo kuhusu uhalisia katika bunilizi, jambo linalowajia akilini kwanza ni dhana ya mimesia (muhakati) ambayo kwa maoni yao ni mwigo wa maisha. Kuhusu mwigo huu, wasomi hawa wanaendelea kusema kwamba "kuna kitu kilichoko nje ya akili ya mwandishi ambacho yeye anajaribu kuiga" (tafsiri yetu). Kwa maoni yetu, dhana ya kitu kama inavyotajwa hapa ni pana na wala hairejelei kifaa tu. Kwa mfano, inaweza pia kurejelea jambo au hali fulani katika maisha. Hivi ni kumaanisha kwamba tungo za kihalisia hazifai kujikita kwenye usimulizi unaohusu mambo, hali, watu na vitu dhahania bali zinafaa kusimuliwa kwa namna inayoiga maisha halisi ya jamii. Mawazo haya yanalingana na msingi wa nadharia ya u-Marx wa kirasimi ulio hali yakinifu katika maisha ya binadamu au uhalisi unaoonekana. Akichangia wazo hili, Wamitila (2002:115-116) anaeleza usimulizi wa kimuhakati kama ule unaosimulia matukio kama yanavyotokea katika ulimwengu halisi au kwa namna inayokaribiana na hali iliyoko katika jamii. Ni usimulizi

unaofaa kuwasilisha maisha ya wahusika, matendo yao na mazingira waliyomo kwa usahihi na uaminifu (kihalisia) huku pia ukidhihirisha maisha ya jamii katika ngazi za kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa.

Sifa nyingine ya tungo za kihalisia ni kwamba muundo wa sentensi wa kazi hizo pamoja na uteuzi wa msamiati huwa sahili. Mbali na hayo, usimulizi unaoegemea uhalisia unapaswa kusuta maovu ya kijamii (Wafula na Njogu 2013:64). Kwa maoni yetu riwaya zetu teule zina sifa hizi lakini kwa viwango tofauti. Kwa mfano, masimulizi yaliyomo katika riwaya teule yamekitwa katika maisha ya jamii. Kuna ufafanuzi wa mandhari ya mahali maalum yanayoangaza makazi ya matabaka mawili makuu hasa katika riwaya ya *Mwanasiasa*. Matukio hayajapangwa kikronolojia lakini kiuhalisia, usimulizi unaorejelea mandhari ya wakati maalum pia umehusishwa katika riwaya hii. Tunaweza kutoa mfano wa siku ya jumatano asubuhi na mapema ambapo maandamano ya kumng'oa Bwana Mkubwa uongozini yalipofanyika (uk.119).

Kimsingi, usimulizi katika tungo teule unaakisi hali halisi za kiuchumi na kisiasa katika nchi nyingi, hasa katika bara la Afrika muda mrefu baada ya kupata uhuru kutoka kwa wakoloni. Ngazi ya kiuchumi katika jamii inayowakilishwa katika riwaya teule inadhihirishwa na mfumo wa ubepari uchwara huku siasa inayoibuka ikitokana na mfumo huo. Hivi ni kwa sababu kitegemezi cha mabadiliko ya jamii — kama u-Marx wa kirasimi unavyoeleza — ni cha kiuchumi pekee (Wafula na Njogu 2013:69). Katika ngazi ya kisiasa, usimulizi wa riwaya ya *Mwanasiasa* unazungukia usawiri wa maovu yanayotokana na uongozi mbaya pamoja na harakati za kuirekebisha hali hiyo kimapinduzi. Tunaona usimulizi sawa na huo katika riwaya ya *Yasinya* lakini mwelekeo unaoonekana kujaribu kuirekebisha hali hiyo si wa kimapinduzi kama u-Marx wa kirasimi unavyopendekeza bali ni wa kuyapinga maovu, kuanzisha miradi ya kuwasaidia wanyonge, kuelimisha jamii iadilike kwa kuthaminiana kama inavyosemwa na mhadhiri aitwaye Gwiji (uk.135) pamoja na pendekezo la kubadili sheria za nchi. Pendekezo hili (kubadilisha sheria za nchi) na wakati mwingine kutekelezwa kwake ni suala halisi la kisiasa ambalo limeshuhudiwa hasa katika mataifa mengi yaliyorithi sheria kandamizi kutoka kwa tawala za kikoloni. Tunapozisoma riwaya teule, tunahisi kwamba tumeathiriwa na maovu ya utawala mbaya yanayoangaziwa katika tungo hizo.

Tukigeukia usimulizi maizi, mfano unajitokeza katika *Yasinya* (uk.32), pale ambapo msimulizi 'anapenya' katika mawazo ya mheshimiwa aliyekuwa katika mkutano wa maombi ya umma na kueleza jinsi alivyoanza kuwaza juu ya mashamba yake ya chai na mibuni. Usimulizi wa aina hii pia unapatikana katika riwaya ya *Mwanasiasa* (uk.36) pale ambapo msimulizi maizi 'anaingia'

katika akili ya Mwarupia na kutujulisha maswali ambayo mhusika huyu alikuwa akijiuliza kuhusu picha iliyokuwa imetundikwa ukutani kwenye ofisi ya mwaakida. Huu ni wakati ambao Mwarupia alikuwa ameitwa katika ofisi hiyo akaeleze sababu za kukataa kutoa mchango wa kufadhili mkutano wa Bwana Mkubwa.

Katika usimulizi wa kimuhakati, tumekutana na wahusika kama Asisi (katika *Yasinya*) na Mwarupia (katika *Mwanasiasa*) waliopewa dhima ya kudadisi, kufichua na kusuta maovu yanayoendelezwa na tawala mbaya. Usimulizi unaonyesha jinsi wahusika wanaotafuta kuchaguliwa kama viongozi katika riwaya ya *Mwanasiasa* wanavyotumia lugha. Usimulizi huu unaiga uhalisia madhali matumizi hayo ya lugha yanashabihiana na ya wanasiasa katika jamii tunazofahamu. Kwa kawaida, wao hutumia lugha kwa namna inayodhihirisha kujisifu na kutoa ahadi za uongo. Kwa mfano, Bwana Mkubwa aliambia umati uliohudhuria mkutano wake kwamba alikuwa amewafanyia watu mambo mengi. Huku akiomba kuchaguliwa tena kama kiongozi wa Bondeni, mhusika huyu aliahidi kukamilisha miradi yote ya maendeleo (uk.31-32). Kiuhalisia, matumizi yake ya lugha yanachochewa na azma ya kutaka kuchaguliwa tena. Katika *Yasinya* (uk.106), usimulizi unaoonyesha matumizi ya lugha kulingana na umri au hali inayomkumba mtu unadhihirisha mwigo wa hali halisi kupitia kwa dada mdogo wa Huni. Alipokuwa ametumwa na nyanyake kwa Yusi wakapokee hongo ili wamwachilie Huni huru, msichana huyu alizungumza kwa hali ya kusitasita. Alipoulizwa na Yusi kile alichokuwa ametumwa na nyanya, dadake Huni alisema: “Ati...ati...amesema...m...m...” Kwa maoni yetu, kusitasita huku kulisababishwa na woga na pia umri mdogo wa msichana huyo. Kwa upande mwingine, lugha iliyotumiwa (muundo sahili wa sentensi na msamiati) inachangia uelewekaji wa riwaya teule hivi kwamba haitubidi kufanya urejelezi wa kamusi mara kwa mara. Hatuna budi kusema kwamba lengo hasa la usimulizi sahili uliopo ni kufikia hadhira maalum kwa urahisi ili kuielimisha na kuizindua ipate mwamko wa kutatua matatizo yanayoikabili. Hivi ndivyo inavyopasa kuwa katika sanaa amilifu kama riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa*.

Kwa lengo la kusisitiza mawazo fulani na kuakisi hisia za ndani za mhusika kutokana na hali yake halisi, usimulizi umehusisha mbinu ya anafora. Kwa mujibu wa Shaw (1905:20), hii ni mbinu ya kiusemi inayohusu “urudiaji wa neno au kundi la maneno mwanzoni mwa mishororo miwili au zaidi inayofuatana katika sentensi, kishazi au kifungu” (tafsiri yetu). Akihutubia mkutano katika kumbukumbu ya mhadhiri Gwiji, Asisi (katika *Yasinya*) anaeleza umuhimu wa kuheshimu mchango wa Gwiji katika ustawi wa Mabonde. Katika maneno yake yanayodhihirisha matumizi ya mbinu ya anafora, Asisi anasema: “Basi, ili kuheshimu mchango

wake huo, tunastahili kujenga jamii mpya. Ni kwa ajili hii ndugu zetu ndipo tunawasihi kujenga jamii mpya. Ni kwa ajili hii ndugu zetu ndipo tunawasihi kaeni, ishini na changamaneni kama Wanamabonde" (uk.158). Tazama jinsi makundi ya maneno kama 'ni kwa ajili hii ndugu zetu ndipo tunawasihi', na 'jamii mpya' yalivyorudiwa. Mfano mwingine katika riwaya ya *Yasinya* unapatikana katika malalamiko ya Kipokeo kuhusu uongozi mbaya ulioleta umaskini katika Mabonde na hatimaye kumfanyayeye kuwa malaya. Katika malalamiko haya, Kipokeo anauliza: "Nani hajui hakuna ajira? Nani hajui?" (uk.21). Matumizi ya mbinu ya anafora yanadhihirishwa na urudiaji wa maneno "nani hajui?" Katika riwaya ya *Mwanasiasa*, mfano wa usimulizi wa aina hii upo katika kueleza yaliyosemwa na Mwarupia alipokuwa akiwazindua Wanajamii kupigania usawa. Anasema: "Wanabonde lazima tuungane tuwe kitu kimoja. Lazima tuwe na umoja. Lazima tuzungumze kwa sauti moja". Urudiaji wa neno 'lazima' unaakisi matumizi ya mbinu ya anafora.

Mwandishi wa kazi ya kiuhalisia huandika ili azungumze na msomaji kwa namna ya kujenga taswira au picha wazi zinazomwathiri kihisia kwa sababu ya usanii uliotumiwa. Picha hizi huwezesha kueleweka kwa kazi inayohusika. Tunaona usanii wa aina hii ukijitokeza katika usimulizi unaohusisha tashbihi. Kwa mujibu wa Mwakio (2016), tashbihi ni"mbinu ya lugha ya kufananisha kitu kimoja na kingine kwa kutumia viungio kama vile 'mithili ya', 'kama', 'sawa na', 'mfano wa', na 'ja". Viungio vingine vinavyotambulisha tashbihi ni 'kiasi cha', 'utadhani ni' na 'utafikiri ni'. Kwa mujibu wa nadharia ya u-Marx wa kirasimi, makazi huwa muhimu katika kuelezea uhalisia.Katika riwaya ya *Yasinya*, msimulizi ametumia tashbihi kuiakisi picha halisi ya makao ya Kibisuswa kwa tabaka la wachochole. Kama tunavyoelezwa, picha hii ilimshangaza Asisi. Kwa mfano tunaambiwa: "Njia ya kufikia makazi ya watu ilikuwa nyembamba kama iliyopita panya*"* (uk.53). Tashbihi hii inaonyesha jinsi eneo hili lilivyobaguliwa katika maendeleo ya Mabonde. Usambazaji wa mali ya Mabonde haukufanywa kwa usawa hivyo basi kuzorotesha maisha ya wakazi wa Kibisuswa. Mbali na hayo, tashbihi hii inaonyesha kuzinduka na kuathirika kwa Asisi akaona umuhimu wa kuendelea kupigania usawa wa jamii ya Wanamabonde waliotengwa kimaendeleo. Katika riwaya ya *Mwanasiasa*, Mwandishi ametumia tashbihi kuwasilisha maudhui ya kutamauka kwa tabaka la maskini linalojumuisha watawaliwa. Aidha, kutamauka kwa wanyonge kunaonekana baada ya ardhi yao kuchukuliwa na matajiri. Tunajulishwa kwamba matajiri walinyakua ardhi, wakawafurusha wachochole, wakabomoa nyumba zao na kuwafanya kuwa maskwota. Kwa kutumia tashbihi, msimulizi anaeleza kwamba wachochole walijaribu kupinga maovu haya lakini: "Juhudi zao

zilikuwa kama kilio cha samaki; machozi kwenda na maji" (uk.103). Usimulizi kwa kutumia tashbihi katika riwaya teule ni mpana. Hapa tumetoa mifano tu.

Katika riwaya ya *Yasinya*, tunaona usimulizi unaochanganya msimbo. Usimulizi wa aina hii huwa na nafasi ya kudhihirisha uhalisia. Akichangia hoja hii, (Mbatiah 2016:268) anasema kwamba kuchanganya msimbo huakisi hali halisi ya matumizi ya lugha katika mazingira ya lugha nyingi. Kadhalika, ni mbinu ya kutumia lugha inayosawiri mandhari ya kimahali na kiutamaduni. Mfano mzuri upo katika matumizi ya maneno *managu* na *terere* (uk.34) na *nduma* (uk.142) kutoka baadhi ya lugha za kiasili za kibantu — yaliyotumiwa kurejelea chakula kilichotumiwa na tabaka la maskini. Usimulizi wa aina hii katika riwaya ya *Yasinya* unatokea pia katika muktadha unaoeleza kukerwa kwa Kipokeo kutokana na jinsi Kifuja alivyowateua wanachama katika bodi ya usimamizi wa hazina ya ustawishaji maeneo ya pale kwao. Kutokana na hali hii, utingo aliyetaka kumbeba Kipokeo kwa gari lake alimkuta akiwa anajizungumzia hivi kwamba aliona kama alikuwa na wazimu. Kwa kutumia lugha ya sheng, utingo anasema, "mbao! unaenda?...huyu haendi dere. Alikuwa anabonga solo" (uk.45). Tofauti na riwaya ya *Yasinya*, usimulizi katika riwaya ya *Mwanasiasa* umejikita pakubwa katika lugha sanifu ya Kiswahili — jambo ambalo ni ukwepaji wa uhalisia wa matumizi ya lugha katika mazingira ya lugha nyingi.

Kwa sababu ya viwango tofauti vya uhalisia katika riwaya teule, usimulizi katika riwaya ya *Mwanasiasa* unaifanya simulizi hiyo kusomeka haraka na hivyo basi kwenda kasi kuliko riwaya ya *Yasinya*. Tunaweza kutetea mtazamo huu kwa kutoa mfano wa mwanzo wa riwaya hizo ambapo riwaya ya *Yasinya* inajikita katika usimulizi unaomzunguka mhusika MA, ambaye anaonekana kukiuka uhalisia kwa kuwa anajitokeza katika mawazo ya Kijasiri na Asisi. Kwa ufupi, usimulizi unaonyesha kwamba uhusika wa MA ni wa kinjozi kinyume na ipasavyo kuwa katika tungo za kiuhalisia. Kwa hivyo, usomekaji na kisha uelewekaji wa riwaya hii katika sehemu hiyo ya mwanzoni hauendi kwa kasi sawa na ule wa mwanzo wa riwaya ya *Mwanasiasa*. Athari sawa na hiyo inapatikana katika masimulizi yanayomhusu Asisi akigombana na kukemeana na Kifuja katika ndoto (uk.65-66). Mazungumzo ya aina hii yanakwenda kinyume na mtazamo wa nadharia ya u-Marx wa kirasimi isiyoweka msisitizo mkubwa kwenye mawazo au mambo dhahania katika maisha ya binadamu. Ijapokuwa juhudi kubwa zimefanywa kusimulia hadithi katika riwaya teule kiuhalisia, ukuzaji wa baadhi ya wahusika na utumiaji wa majazi kurejelea baadhi ya makazi katika riwaya teule ni mambo yanayoonekana kukiuka uhalisia. Tulieleza jinsi utumiaji wa majazi unavyokiuka uhalisia katika sura ya pili na hakuna mantiki ya kuliangazia suala hili zaidi.

Said (1995:64) anaeleza msuko kama "majilio ya matukio mbalimbali katika kazi ya sanaa kama yalivyopangwa kutokana na visababisho na matokeo". Riwaya ya *Mwanasiasa* ina msuko msago (sahili) ambao ni mpangilio wa matukio katika fasihi kwa namna ya moja kwa moja au mfuatano bila kuhusisha matumizi ya mbinu rejeshi. Katika msuko huu, hadithi huanza, hukua na kufikia upeo au kilele chake na kisha tamati. Kwa upande mwingine, riwaya ya *Yasinya* ina msuko kioo. Katika msuko wa aina hii, matukio katika kazi ya kifasihi hutupwa nyuma na mbele na hayaendi sambamba na wakati (Oriedo 2007:52). Kutupwa nyuma na mbele kwa matukio kunarejelea matumizi ya mbinu rejeshi na kiangazambele mtawalia.

Katika riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa*, hadithi zinaanza kwa masimulizi yanayoonyesha kiini cha matatizo ya jamii husika. Katika hali ambayo inaafikiana na nadharia ya u-Marx wa kirasimi, msingi wa matatizo hayo umekitwa katika historia ya jamii. Haya tunayapata kupitia kwa Kijasiri katika riwaya ya *Yasinya* katika masimulizi ya kisa cha mhusika MA anayelalamika kwamba wananchi wa sasa katika Mabonde wameshindwa kukumbuka mambo yaliyopita kutokana na ubinafsi, uchoyo na ulafi wao (uk.7-17). Hadithi hii inapoendelea, maovu katika jamii yanaangaziwa. Haya ni maovu ambayo chanzo chake hasa ni uongozi mbaya wa Chifu Kifuja. Maovu haya yanapozidi, tunakutana na wahusika kama Asisi na Kijasiri ambao wanajaribu kukabiliana nayo kwa kukosoa utawala mbaya wa Kifuja na kuunda mashirika ya kibinadamu ya kuwasaidia wanajamii. Shughuli za Asisi na washirika wake zinazua mvutano baina yake na utawala uliopo. Hadithi inaisha kwa vifo vya wengi waliojinufaisha kwa njia zisizo za haki akiwemo mtawala wa Mabonde — Chifu Kifuja.

Katika riwaya ya *Mwanasiasa*, hadithi inaanza kwa masimulizi kuhusu mhusika aitwaye Bambua. Masimulizi haya yanaeleza dhima yake katika jamii na kisha kuunganisha utendakazi wake na usawiri wa mji wa Bondeni uliogawika katika matabaka mawili ambayo mwandishi anayaita tabaka la wananchi na la wenyenchi kurejelea tabaka la maskini na matajiri mtawalia. Kupitia mbinu ya uwekaji sambamba na ulinganishi, tunaelezwa tofauti za kimaendeleo katika sehemu mbili za mji wa Bondeni, yaani Bondeni ya viamboni na Bondeni mpya. Ni katika maelezo hayo ambapo tunajulishwa chanzo cha kihistoria cha matatizo ya jamii ya mji wa Bondeni. Hadithi inapoendelea, tunaelezwa kuhusu mikutano ya kisiasa kwa maandalizi ya uchaguzi. Baadaye, tunasawiriwa madhara ya utawala mbaya kwa watawaliwa na kisha harakati za kujikomboa kwa wanajamii. Harakati hizo ndizo zinazojenga kilele cha hadithi kupitia mivutano inayokosoa utawala dhalimu, maandamano na kisha mapinduzi. Kama ambavyo tumedhihirisha, riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa*zinatamatika kwa namna tofauti.Riwaya ya

*Mwanasiasa* inahitimishwa kwa kuakisi maendeleo chanya ya jamii kupitia mapinduzi ya utawala mbaya na kuchukuliwa kwa mamlaka na kiongozi anayezingatia usawa na haki. Kama inavyopaswa kuwa katika u-Marx wa kirasimi, mapinduzi katika riwaya ya *Mwanasiasa* yametanguliwa na maandamano ya wanajamii wanaodhulumiwa. Hata hivyo, waandamanaji hawa si wa tabaka la wafanyakazi eti wakitaka ujira bora kama inavyopaswa kuwa kwa mujibu wa nadharia inayoongoza utafiti wetu bali ni watawaliwa maskini kwa jumla. Kwa upande mwingine, riwaya ya *Yasinya* imehitimishwa kwa namna ambayo haionyeshi maandamano na mapinduzi yanayoendelezwa na wadhulumiwa kwa jumla. Kwa sababu hii, tunaona kwamba msuko katika riwaya ya *Mwanasiasa* umesukumwa mbele na motisha wazi ya kuleta mabadiliko katika jamii kupitia utawala bora unaozingatia usawa wa wanajamii huku msuko katika riwaya ya *Yasinya* ukikosa motisha sawa na hio maadamu hatuoni maandamano ya kufana na yenye uwezo wa kuondoa ubinafsi, ulafi na udhalimu kwa watawaliwa wa Mabonde. Aidha, mabadiliko yanayoashiriwa na amri ya chifu mpya iliyowezesha kuachiliwa kwa Kijasiri katika *Yasinya* hayatokani na motisha ya wanaodhulumiwa kutafuta usawa wa wanajamii kupitia mapinduzi bali ni zao la kufa maji kwa Chifu Kifuja. Hakuna maelezo yanayoonyesha kwamba chifu aliyeshika hatamu baada ya Kifuja ana sifa za kuibadilisha Mabonde kwa namna ambayo ingehakikisha kwamba hakuna upaliliaji wa maovu na mfumo wa ubepari katika jamii. Aidha, hakuna ithibati inayoonyesha kwamba sheria za nchi zimebadilishwa kwa sababu ya ukale wake kama alivyopendekeza mhadhiri aitwaye Alua (uk.67).

Suala la itikadi ni mojawapo ya masuala ya kijamii yanayohusishwa na nadharia ya u-Marx wa kirasimi. Kwa sababu hii, tunachunguza pia usawiri wa itikadi, dhima zake katika msuko na uwasilishaji wa maudhui. Kwa mujibu wa Williams (1977:55-56), ‘itikadi, ni istilahi iliyoundwa mwishoni mwa karne ya 18 na mwanafalsafa wa Ufaransa, Destutt de Tracy, ikiwa na maana ya kifalsafa ya “sayansi ya mawazo” (tafsiri yetu). Kama wasomi wengi, Williams anasema kwamba ufafanuzi wa maana ya istilahi hii ni telezi. Kulingana na Mbatiah (2016:231) itikadi ni “mkabala au msimamo maalum wa kimawazo. Pia humaanisha mawazo au imani inayotawala kikundi cha watu au mtu binafsi”. Kwa kiwango kikubwa, maelezo haya yanafanana na mtazamo wa kirasimi wa Marx na Engels kuhusu istilahi hii wanaposema kwamba itikadi ni “mawazo yanayotawala katika kipindi au wakati mahususi”. Mtazamowa Marx na Engels (kuhusu itikadi) pia ni mkarara wa mawazo ya Teun (1998:10) katika kitabu kiitwacho *Ideology: A Multidisciplinary Approach*. Aidha, mwandishi huyu (Teun) anasema kwamba matumizi ya kila siku ya dhana ya itikadi yanarejelea mfumo wa imani za uongo au potovu zinazohusishwa na wapinzani wa kijamii na kisiasa. Mintarafu ya uchumi wa kisiasa wa nyakati za Marx na Engels,

mawazo yaliyotawala yalihusishwa na yale ya tabaka tawala, yalikuwa sehemu ya kikorombwezo na yalidhibitiwa na msingi wa kiuchumi wa jamii (tafsiri yetu). Basi kwa muhtasari, tunaweza kusema kwamba itikadi ni imani, hasa potovu, zinazotawala kikundi cha watu au mtu binafsi katika kipindi mahususi cha wakati. Hata hivyo, baadhi ya wasomi hushikilia kwamba mtu binafsi hawezi kusemwa kuwa na itikadi. Mtazamo huu hauwezi kuathiri utafiti wetu kwani mhusika kifano anaweza kuwakilisha mawazo ya jamii nzima.

Tukirejelea tungo zetu teule, tunaona kwamba katika riwaya ya *Yasinya*, ushauri wa Mayowe kwa kizazi kinachowakilishwa na Kifuja ni itikadi. Kupitia kwa Kijasiri, kisa cha mhusika MA kinasema kwamba Mayowe na watu wengine walimshauri Kifuja kwamba "mpanda ngazi na mshuka ngazi hawapatani" (uk.15). Hii ni imani potovu iliyo na misingi yake katika pupa ya mali na ubinafsi wa matajiri walio wachache. Dhima yake ni kuendeleza maslahi ya tabaka tawala (tabaka la matajiri). Maana ya itikadi hii ni kwamba si rahisi kuwasawazisha maskini na matajiri kiuchumi. Yaani, maskini ataendelea kuwa maskini huku tajiri akiendelea kutajirika na hivyo basi matabaka ya kiuchumi katika jamii yatadumu. Vinginevyo, Chifu Kifuja alikuwa anaambiwa kwamba hakukuwa na haja ya kung'ang'ania kuboresha maisha ya maskini wa Mabonde. Ni kutokana na kuongozwa na itikadi hii ambapo utawala wake ulishindwa kuleta usawa katika maendeleo ya kiuchumi ya jamii. Kuna sehemu za Mabonde zilizokuwa zimeendelea huku zingine zikiwa zimepuuzwa. Aidha, inaonekana kwamba itikadi hii ilichochea maovu ambayo kwayo baadhi ya wanajamii (hususan waliokuwa na ushawishi wa kisiasa na kiuchumi) walijiendeleza kiuchumi kwa njia ambazo hazikuwa za haki.

Mayowe na wenzake waliendelea kushauri utawala wa Chifu Kifuja kwamba "duniani kuna wana wakondevu na wana wanene wenye maumbo ya majitu wanaoghaniwa katika ngano za mazimwi". Bila kutilia maanani ngano za mazimwi ambazo ni za kifantasia, tunaona kwamba kwa kawaida, binadamu hawatoshani kimaumbo. Kwa hivyo, huo ndio uhalisia wa maumbile ya waja. Itikadi hii inalenga kuhalalisha kuweko kwa matabaka katika jamii kwa kuyaweka mbele maslahi ya tabaka la matajiri. Kutokana na imani hii, MA analalamika kwamba utawala wa Chifu Kifuja ulikosa kutekeleza wajibu wa kusawazisha umoja, udugu na utangamano wa watu ambao kwa siku nyingi waliishi kwa ubaguzi na chuki (uk.15).

Kauli "mume na nguvuze" ni itikadi nyingine inayopatikana katika riwaya ya *Yasinya* (uk.31). Hii ni imani inayowakosesha utu Wanamabonde wengi hasa walio na nguvu za kisiasa na kiuchumi (tabaka tawala). Athari ya imani hii ni kwamba ulafi na ubinafsi wa kumiliki mali ulitawala na kuongoza nafsi za viongozi na kugeuza Mabonde kuwa uwaja wa fujo ya

kung'ang'ania kutwaa mali nyingi kadri ya uwezo wa mtu. Inasemekana kwamba fujo hii iliendelea bila yeyote kujali kujenga barabara, mabwawa, makazi ya bei nafuu, viwanda au kuendesha kilimo. Athari za itikadi "mume na nguvuze" ni wazi katika jamii tunamoishi ambapo mara kwa mara tunasikia kashfa za ufisadi zikitangazwa katika vyombo vya habari. Akiwakilisha tabaka la waliotengwa katika jamii, Kipokeo (katika riwaya ya *Yasinya*) analalamikia hali yake ya umaskini. Anasema kwamba umaskini — zao la uongozi mbaya — ndio umemfanya kuwa kahaba. Ili kujitia nguvu za kuendeleza uozo huu, Kipokeo anasema kwamba shilingi hainuki (uk.21). Kwa maoni yetu, mtazamo huu unadhihirisha itikadi yake iliyosukuma mbele tendo la kwanza katika historia ya binadamu ambalo ni kukidhi mahitaji ya kimsingi. Tunaona kiwango cha juu cha kuathiriwa kwake na imani hii anaposisitiza kwamba angeichukua shilingi hata kama ingetoka kwa maiti (k.h.j).

Itikadi za jamii zinaweza kuelezewa na miko na desturi zake. Katika jamii ya Wanamabonde (riwaya ya *Yasinya*), elimu ya mabango ilisheheni miko na desturi zilizoongoza historia ya kizazi cha MA tangu jadi. Ijapokuwa hatuelezwi miko na desturi hizi zilikuwa zipi, itikadi katika jamii zinaakisiwa kupitia elimu hii ambayo tunaambiwa ilitia tumbo mbele huku ulimi ukichomoka kuramba kila aina ya utamu nao nyuki wakihimizwa kujitahidi zaidi kutengeneza asali (uk.16). Kwa maoni yetu, matajiri walafi na wanyonyaji wa maskini ndio wanaorejelewa na tumbo lililotiwa mbele na ulimi uliochomoka kuramba kila aina ya utamu huku nyuki wanaohimizwa kujitahidi zaidi kutengeneza asali wakirejelea wafanyikazi wanaohimizwa kutia bidii kazini. Elimu hii inaonyesha kwamba wafanyikazi hawakufaidika na nguvukazi zao. Ni elimu iliyoendeleza na kuhalalisha unyanyasaji wa wafanyikazi na hivyo basi kusababisha mgawanyiko wa jamii kitabaka.

Matumizi ya lugha katika riwaya teule yanadhihirisha itikadi za wanajamii. Tukirejelea riwaya ya *Mwanasiasa*, methali "njaa haijui miiko" inakuza maudhui ya umaskini na kuonyesha imani inayohalalisha matakwa ya walalahoi katika mazingira ambamo miiko inawafunga kutenda mambo fulani ili kukidhi haja ya njaa. Kauli hii, inayodhihirisha msukumo wa tendo la kwanza katika historia ya binadamu (kutafuta namna ya kukidhi mahitaji ya kimsingi),inamaanisha kwamba, aonaye njaa, huwa hawezi kuzingatia sana miiko. Kwa hivyo, mhitaji anaweza kutumia kila aina ya maarifa kutosheleza haja yake. Mara nyingine, mbinu anazotumia hukiuka matarajio ya watu lakini mwenye haja hajali ili apate msaada anaotafuta. Kwa sababu ya msukumo wa njaa, imani hii inaendeleza maslahi ya maskini kwa kuvunja sheria na miiko iliyoulinda msitu wa Nguu Tatu na kuuvamia ili kuchuma matunda ya mwituni, wakaendeleza usasi na ulishaji wa

mifugo (uk.108). Kadhalika, imani hii inarejelea hali ambapo walalahoi wa viamboni vya Tuwa Tugawe walizikopa bidhaa katika kijiduka cha Mwarupia. Mwarupia aliwakopesha maadamu alielewa fika kwamba "mwenye njaa hana miiko" (uk.40). Ni imani inayoonekana kuijenga sifa ya Mwarupia kama mtu mwenye huruma kwa maskini na hivyo basi kumweka katika nafasi nzuri ya kuwa mwakilishi wao katika dola la Bwana Mkubwa.

Kauli nyingine na ambayo inadhihirisha njia za kiyakinifu za kijumla za uzalishaji wa mawazo, imani na tathmini katika maisha ya jamii iliyogawika kitabaka ni kwamba "mnyonge kupata haki ni mwenye nguvu kupenda". Hii ni itikadi inayoendeleza maudhui ya utajiri na umaskini pamoja na kupalilia matendo ya kujinufaisha kwa njia zisizo za haki. Maana yake ni kwamba kufanikiwa kwa mtu maskini hutokea endapo mtu aliye na uwezo amemwachia fukara huyo nafasi. Ni itikadi inayotumiwa kuwaliwaza wale wanaolalamikia kunyanyaswa na matajiri. Katika riwaya ya *Mwanasiasa*, methali hii inarejelea hali ambapo matajiri wa Bondeni mpya walifanyiwa kazi na wachochole wa Bondeni ya viamboni kwa malipo yasiyofaa (uk.82). Kadhalika, inarejelea hali ambapo walalahoi hao waliitwa katika ofisi ya Mwaakida kuthibitisha uhalali wa umilisi wa ardhi yao ambayo walidai ilkuwa imenyakuliwa na tajiri. Tunaarifiwa kuwa wito huo haukuwa na umuhimu wowote kwa walalahoi kwa sababu uamuzi ulikuwa tayari umechukuliwa kati ya Mwaakida na tajiri aliyetaka kunyakua ardhi aliyoipenda. Kujitetea kwa walalahoi hao hakukuwafaa kitu kwani waliishia kusomewa vifungu vya sheria za ardhi ambavyo hawakuvielewa. Waliikosa haki yao na kubaki kuwa maskwota (uk.104). Fauka ya hayo, kauli hii imetumiwa kukuza maudhui ya mchango wa asasi za kiutawala katika kudumisha matabaka Bondeni. Katika riwaya ya *Mwanasiasa*, haya yanadhihirika wakati Wanabonde walipoandamana kupinga kuwepo kwa tabaka la watu wachache waliofaidika kwa jasho la waliokuwa wengi. Katika kukabiliana na maandamano hayo, dola la Bwana Mkubwa lilitumia askari waliojihami kuwatawanya waandamanaji. Msimulizi anasema kwamba askari walitumia nguvu bila huruma maadamu, "mnyonge kupata ni mwenye nguvu kupenda" (uk.97). Vilevile, imani hii inarejelea uchaguzi uliofanyika Bondeni. Uchaguzi huo haukuwa huru na wa haki. Kutokana na ushawishi wa kisiasa na kiuchumi, baadhi ya waliotafuta kuchaguliwa walivipata vyeo kwa kutumia udanganyifu. Kwa mfano, kulikuwa na visa vya kupimwa kwa taa za kandili wakati wa usiku uchaguzi ulipokuwa ukiendelea. Uovu huu ulifanywa na watu ambao walidhaniwa kutumwa na mwanasiasa fulani kuvuruga uchaguzi hasa baada ya kuhisi kuwa angekosa kuchaguliwa. Wakati mwingine, mratibu wa uchaguzi angetishiwa na wanasiasa waliokuwa na ushawishi mkubwa, jambo ambalo lingemfanya atangaze matokeo yenye upendeleo. Ni katika hali hii ambapo Bwana Mkubwa alichaguliwa tena kama kiongozi wa

Bondeni. Msimulizi anasema kwamba kuchaguliwa kwa Bwana Mkubwa hakukuwa jambo la ajabu madhali "mnyonge kupata haki ni mwenye nguvu kupenda" (uk.70). Walioshindwa na Bwana Mkubwa kiudanganyifu hawakuwa na uwezo wa kupinga matokeo ya uchaguzi kutokana na nafasi zao duni (kisiasa na kiuchumi) katika jamii. Urejelezi wa methali katika miktadha mbalimbali ni dhihirisho la kiwango cha kuenea kwa imani inayoakisiwa nayo katika jamii iliyogawika kitabaka.

Kwa namna inayoakisi imani iliyo karibu sawa na "mnyonge kupata haki ni mwenye nguvu kupenda," tunakutana na kauli inayoendeleza ukuzaji na uhalalishaji wa matamanio ya tabaka fulani dhidi ya matamanio ya tabaka kinzani katika jamii. Hii ni kauli isemayo kwamba "mwenye nguvu mpishe". Msemo huu hutumiwa kumshauri mtu kumwacha apite, yule aliye na nguvu kumshinda. Yaani, mtu asiwe na tabia ya kujitia ushujaa wa kupigana na yule anayemshinda nguvu. Katika riwaya ya *Mwanasiasa*, methali hii inarejelea hali ambapo wafanyibiashara matajiri na wanasiasa walinunua bidhaa mbalimbali kutoka kwa wakulima wa Bondeni kwa bei ya chini na baadaye kuziuza bidhaa zizo hizo kwa bei ghali hivi kwamba Wanabonde wachochole walishindwa kuzinunua. Tunaarifiwa kwamba dhuluma hii iliendelezwa Bondeni huku utawala wa Bwana Mkubwa ukijua pasi na waliohusika kuchukuliwa hatua yoyote. Uovu huu uliifanya Bondeni kuwa ya "mwenye nguvu mpishe" ambapo vigogo wa biashara walishindana na vigogo wa siasa katika umilisi wa mali (uk.83). Huku ni kujiendeleza kwa njia zisizo za haki. Kutokana na unyonge wao wa kisiasa na kiuchumi, Wanabonde wa Viamboni hawakuwa na nguvu za kupinga maovu yaliyoendelezwa na matajiri.

Jamii katika riwaya ya *Mwanasiasa* pia inatawaliwa na imani potovu kwamba "mkono mtupu haulambwi". Tunaichukulia hii kuwa imani potovu kutokana na kutumiwa kwake katika kujiendeleza kwa njia zisizo za haki. Kwa mfano, ni katika kampeni za Mwarandu ambapo msimulizi anasema kwamba kwa kuwa "mkono mtupu haulambwi", Mwarandu angewapa wahitaji chochote kile kuwaridhisha huku naye akijihisi amewatendea fadhila kubwa watu hao (uk.51). "Chochote" kinachorejelewa hapa kinaashiria hongo ili Mwarandu apate kuchaguliwa. Huu ni ufisadi ambao umeshuhudiwa katika mataifa mengi wakati wa uchaguzi — hali inayowanyima maskini nafasi ya kuchagua viongozi wanaofaa. Uovu huu una nafasi kubwa ya kuchangia hali ambapo Wanabonde waliwachagua viongozi wasiofaa kila msimu wa uchaguzi. Ni uovu halisi katika jamii madhali hata serikali nyingi zimeweka sheria ya kukabiliana nao.

Katika riwaya ya *Yasinya*, imani kwamba "kelele za chura hazimzuii ng'ombe kunywa maji" inatumiwa kuhalalisha matamanio ya tabaka tawala kwa upotoshaji. Kimsingi, imani hii

inahalalisha maslahi ya tabaka la matajiri ya kujiendeleza kwa njia zisizo za haki. Katika muktadha wa riwaya husika, 'chura' wanaorejelewa ni Wanamabonde wanaodhulumiwa huku 'ng'ombe' wakiwa watu wenye uwezo mkubwa (kisiasa na kiuchumi) na wanyanyasaji kama vile Chifu Kifuja. 'Kelele' nazo, ni sauti za Wanamabonde wakipinga dhuluma wanazofanyiwa na wenye nguvu. Kauli hii inamaanisha kwamba mtu anapoendelea na kazi yake, hafai kuwajali wanaomwambia mambo ya kumvuta nyuma au kuiwekea shughuli yake kikwazo bali anafaa kuwapuuza. Huu ndio msimamo ulioshikiliwa na Kifuja na washirika wake katika bodi ya usimamizi wa hazina ya ustawishaji maeneo ya Mabonde. Tuonavyo ni kwamba imani hii inahalalisha dhuluma zinazofanyiwa tabaka tawaliwa kwa kuchukulia kwamba sauti zao zinazopinga ukandamizwaji hazina umuhimu wowote kwa tabaka linalowadhulumu. Ni imani inayorejelea hali ambapo Chifu Kifuja alihakikisha kwamba waliochukua nyadhifa katika bodi iliyotajwa awali ni waliokuwa na uhusiano wa karibu naye. Bodi hii ilitekeleza majukumu yake kwa upendeleo. Kwa mfano, tunaelezwa kwamba visima vinne vya maji vilichimbwa katika mashamba ya watu binafsi — wote waliokuwa na uhusiano na Chifu Kifuja. Msimulizi anasema kwamba tukio hili liliwafanya watu watete bali kuteta kwao hakukuwa na umuhimu wowote madhali "kelele za chura hazimzuii ng'ombe kunywa maji" (uk.48). Katika riwaya iyo hiyo (*Yasinya*), imani potovu kwamba "maskini kupata ni tajiri kupenda" imetumiwa kuashiria mazingira na uzoefu wa maisha halisi katika jamii iliyogawika kitabaka. Imani hii inaonyesha kwamba mtu maskini hufanikiwa tu anapoachiwa nafasi na mwenye uwezo hasa tajiri. Kauli hii inaendeleza maudhui ya kujinufaisha kwa njia zisizo za haki. Matumizi yake yanatokana na uamuzi wenye utata, wa kesi katika mahakama za Mabonde. Ni uamuzi unaofanya msimulizi kurejelea mwanasayansi mchanga wa Mabonde aliyesema kuwa hakuna jambo ambalo halingewezekana katika Mabonde kwani ilitegemea uzito wa mkono wa mwasilishaji au mwasilishiwa. Kwa hivyo, "maskini kupata ni tajiri kupenda" (uk.102). Uzito wa mkono unaotajwa hapa ni nguvu za kiuchumi au kisiasa za anayehusika katika kesi fulani. Japo kesi iliyomfanya mwanasayansi huyo kutamka haya haikuwahusu watu kutoka matabaka mawili tofauti, bali iliwahusu mume na mke, kauli aliyoitoa ilikuwa ya kijumla na ya kudhihirisha jinsi kesi zilivyoamuliwa katika mahakama za Mabonde. Imani hii inaonyesha wazi kuweko kwa matabaka mawili katika jamii — watawaliwa walio maskini na wanaotawala walio matajiri. Aidha, inaonyesha jinsi haki ilivyokosekana kwa maskini katika maamuzi ya kesi katika mahakama za Mabonde. Huu ni uhalisia katika jamii ambapo mfumo wa ubepari unaendelezwa. Hivi ndivyo sheria inavyotumiwa katika mfumo huo. Yaani, sheria hutumiwa kuwadhulumu wanyonge huku ikipendelea na kulinda mali ya tabaka lenye nguvu.

Isitoshe, maudhui ya kujiendeleza kwa njia zisizo za haki pamoja na kutamauka kwa wanyonge yanaendelezwa kupitia kwa imani kwamba “mkono mtupu haulambwi”. Kwa mujibu wa utafiti wetu, hii ni imani potovu inayohalalisha matamanio ya tabaka tawala. Katika riwaya ya *Yasinya*, kauli hii imetumiwa kurejelea muktadha ambapo malipo ya mumewe Kijasiri yalicheleweshwa na shirika la bima liitwalo Maba. Mintarafu ya tukio hili, Kijasiri alikosa matumaini ya kuyapata malipo hayo. Jambo hili lilisababishwa na kutoendelea kwa kesi iliyohusu malipo hayo. Katika kesi hiyo, Kijasiri alikumbana na kuongezewa bei na wakili wake wa kwanza huku kesi ikiwa haiendelei. Wakili wa pili alimkwepa Kijasiri na kuahirisha kesi mara kwa mara. Angusha naye alimtaka Kijasiri awe mpenziwe ili amsaidie katika kesi hii. Alipomwacha wakili wa kwanza na kukataa ushawishi wa Angusha, Kijasiri alijiuliza: “Kesi za wangapi hazisuluhishiki maana wangu mtupu haulambwi?” (uk.98). Maneno “wangu mtupu haulambwi” ni kifupisho cha methali inayosema “mkono mtupu haulambwi”. Matumizi yake yanaonyesha kwamba mbali na Kijasiri, kuna watu wengi ambao hawakuwa na uwezo wa kugharamia kesi zao. Hawa walitoka katika tabaka la maskini. Mikono yao ni mitupu. Kutokana na umaskini uliowakumba, ilikuwa vigumu kupata haki katika jamii ya Mabonde. Masaibu yaliyomsibu Kijasiri katika shirika la Maba yanaonyesha njama ya kumnyima haki yake — malipo ya mumewe. Katika tukio sawa na hilo, mhazili wa kampuni ya bima alimtaka Asisi atoe hongo ili Kijasiri apate malipo ya marehemu mumewe. Huu ni wakati Asisi alikuwa ameandamana na Kijasiri katika afisi ya bima ili kufuatilia malipo hayo. Mhazili alimwambia Asisi: “Wangu mtupu haulambwi, wewe bwana unajua ilivyo. Jikune unapoweza” (uk.110). Utoaji na upokeaji hongo ni mbinu mojawapo ambayo kwayo baadhi ya watu (hasa wenye uwezo wa kiuchumi na kisiasa) katika Mabonde wanaendelea kujinufaisha kwa njia zisizo za haki.

Ingawa Asisi alinyanyaswa katika harakati za kukabiliana na maovu yaliyotendewa Wanamabonde, yeye aliendelea kuwatetea watu kwa ujasiri unaoelezwa na imani yake kwamba “penye mawimbi ndipo penye mlango” (uk.76). Imani hii inatumiwa kuwahimiza watu katika malengo yao ili wasife moyo matatizo yanapozidi kwani mwisho wa matatizo hayo huwa karibu. Katika riwaya ya *Yasinya*, mawimbi yanayorejelewa yanatokana na juhudi za tabaka tawala kutaka kudumisha uongozi uliowaletea Wanamabonde wengi dhuluma na umaskini mkubwa. Mlango unaotajwa ni ufanisi wa Asisi katika kufanya Mabonde mahali pema pa kuishi. Tukichunguza mtazamo wa Asisi, tunaona uhalisia katika harakati za kuwakomboa wadhulumiwa wa Mabonde kwa kuwa harakati za aina hii aghalabu hukumbana na upinzani mkubwa. Baada ya kuzinduka kwa Asisi, kauli hii inaonyesha mwamko na ukakamavu wake katika kukabiliana na dhuluma katika jamii ya Mabonde. Huku pia ikitumiwa kuwasilisha

maudhui ya ukombozi wa jamii, kauli inayojenga imani hii imekitwa katika muktadha wa mazingira halisi ya uchukuzi wa majini. Mbali na hayo, Kijasiri anatueleza kuhusu sifa ya ujasiri wa Asisi anaposema kwamba Asisi alitenda lililowezekana siku hiyo hiyo bila kuingoja kesho (uk.100).

Katika riwaya ya *Mwanasiasa,* imani kwamba "binadamu si kamili" imetumiwa kuhalalisha matamanio ya tabaka la matajiri. Imani hii inashikilia kwamba kila mtu ana udhaifu wake na huingia majaribuni. Kwa hivyo, hatufai kuwadharau wenzetu wanapotenda mabaya kwa kuwa maovu ya binadamu duniani yanatokana na udhaifu wake. Ijapokuwa ni kweli kwamba binadamu si kamili, imani hii inapotosha maadamu inachangia katika kujinufaisha kwa njia zisizo za haki. Katika riwaya husika, tunaelezwa kwamba Mwarandu aliyekuwa kiongozi wa dini aliiasi huduma ya Mungu na kujitosa kwenye siasa. Katika kampeni za kutaka kupigiwa kura, mhusika huyu alitoa hongo. Kudhihirisha uovu huu, msimulizi anaeleza jinsi Mwarandu "alivyotoa kilemba" kote alikopitia ili kuwapa vinara pesa za kutumia kwenye kampeni za kumpigia debe. Kwa kuwa binadamu si kamili, vinara hao hawakutoa chauchau yote waliyopewa bali walifaidisha nafsi zao kwanza na kuwapunja waliokusudiwa (uk.51). Kutokamilika kwaokibinadamu kulitokana na ubinafsi pamoja na msukumo wa tendo la kwanza la historia ya binadamu ambalo, kama tulivyoeleza katika sura ya kwanza, ni kutafuta namna ya kutosheleza mahitaji ya kimsingi. Imani hii pia imetumiwa kudhihirisha nafasi ya dini katika mfumo wa kitabaka ambapo kimsingi, inaonyesha jinsi unafiki unavyoendelezwa na wanadini katika mfumo wa kibepari. Dhima nyingine ya imani hii ni kuakisi uhalisia kupitia matendo yanayotokana na hali halisi ya binadamu. Ni uhalisia kwamba binadamu si kamili. Kama mhusika Mwarandu alivyo, binadamu hubadilika na huingia majaribuni kutokana na hali halisi anayokumbana nayo.

Imani nyingine inayoongoza jamii katika riwaya ya *Mwanasiasa* ni kwamba "sikio halishindani na kichwa". Katika muktadha wa riwaya husika, imani hii inaashiria mazingira na uzoefu wa maisha ya tabaka la maskini. Ni imani inayoendeleza maudhui ya kutamauka kwa wanyonge (maskini watawaliwa) katika riwaya teule. Usemi huu unaambiwa mtu aliye chini ya mamlaka ya mtu mwingine kisha akawa anajidai kuwa na uwezo mkubwa. 'Sikio' linalotajwa linarejelea Mwarupia huku 'kichwa' kikirejelea Bwana Mkubwa (kiongozi wa Bondeni). Wahusika hawa wanawakilisha matabaka mawili tofauti katika jamii ya Bondeni: maskini na matajiri mtawalia. Maneno haya yalitumiwa wakati Mwarupia alikamatwa. Kukamatwa kwake kulizidisha dhuluma kwa Wanabonde kwa vile hakukuwa na mtu mwingine wa kukemea maovu hayo. Wakosoaji wa Mwarupia walikuwa na maoni tofauti kuhusu harakati zake za kuupinga utawala wa Bwana

Mkubwa. Walimtaja kwa husuda maadamu hawakuona uwezekano wa kumng'oa Bwana Mkubwa kutoka mamlakani. Katika hali inayodhihirisha ukosefu wa matumaini ya kupata ukombozi, wanasema: "Tulimwambia sisi, sikio halishindani na kichwa" (uk.114). Aidha, maudhui yayo hayo (kutamauka) yanawasilishwa katika riwaya ya *Yasinya* kupitia kwa imani kwamba "gangaganga ya mganga humwacha mgonjwa na tumaini" (uk.93). Kwa upande mwingine, imani hii inaelezea njia za kiyakinifu na kijumla za uzalishaji wa mawazo, imani na tathmini katika maisha ya jamii. Kutamauka kunakorejelewa hapa ni kwa maskini walioishi katika maeneo yaliyobaguliwa kimaendeleo na uongozi wa Chifu Kifuja. Kauli hii ilitumiwa katika harakati za kumtafutia ajuza fulani matibabu. Baada ya ajuza huyo (aliyepelekwa hospitali kwa bodaboda) kukosa matibabu, mgonjwa alifanyiwa ukunga na Emali kwa kutumia dawa iliyotokana na umajimaji wa matawi yaliyochumwa msituni. Tunaelezwa kuwa tiba ya Emali ilimpa bikizee huyo afueni hivi kwamba aliitisha chakula. Ni kutokana na ukunga huo ambapo msimulizi anatumia maneno hayo. Gangaganga ya mganga humpa mgonjwa matarajio au matumaini ambayo aghalabu hayadumu. Huku ikiwasilisha maudhui ya kutamauka, imani hii inaakisi uhalisia kwa kuwa imetumika katika muktadha unaoonyesha jinsi maskini wanavyotumia mazingira halisi wanamoishi kujaribu kutatua matatizo yao ya kiafya hasa kupitia dawa za kienyeji.

"Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu" aidha ni imani inayoongoza jamii katika riwaya ya *Mwanasiasa*. Hii ni imani ya kweli inayotumiwa kusisitiza umuhimu wa ushirikiano wa watu katika kushughulikia mambo yanayowahusu. Tunakutana na maneno hayo katika hotuba ya Mwarupia (mtetezi wa wanyonge) ambapo aliwahimiza Wanabonde wawe na umoja katika kushinda udhalimu waliotendewa na utawala wa Bwana Mkubwa. Katika hotuba hiyo, Mwarupia anadhihirisha imani yake kuhusu hatima ya jamii kwa kuwaambia Wanabonde wenzake kwamba hakuna malaika angetoka mbinguni kuwasaidia — ilibidi wajisaidie wao wenyewe. Tunauona mtazamo huu (wa Mwarupia) kama mkarara wa mawazo ya Wafula na Njogu (2013: 67) wanaposema kwamba u-Marx humwabudu binadamu kama mwenye urazini wa kuibadilisha dunia iwe mahali bora pa kuishi. Mhusika huyu aliwataka Wanabonde waungane mikono ili waweze kushinda udhalimu waliotendewa kwa kuwa "umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu" (uk.99). Maneno haya yamekuwa muhimu katika kuwasilisha maudhui ya uzinduzi wa tabaka la wanyonge — tabaka tawaliwa. Vilevile, ni maneno yanayotumika kuwasilisha maudhui hayo kiuhalisia kwa kuwa tunasikia yakitumiwa mara kwa mara na viongozi wakitaka watu waungane kwa sababu umoja wao huwa muhimu katika kuyatatua matatizo yanayowakabili.Aidha, maudhui ya uzinduzi katika riwaya hiyo (*Mwanasiasa*)

yanaendelezwa kupitia kwa imani kwamba "amani haiji ila kwa ncha ya upanga". Hivi ni kumaanisha kwamba maneno peke yake hayawezi kutegemewa kuleta suluhu katika kila jambo. Akionyesha kukithiri kwa dhuluma zilizofanyiwa Wanabonde watawaliwa na utawala wa Bwana Mkubwa, msimulizi anaeleza jinsi kikundi cha akina Mwarupia kilivyopanga mikakati ya kupambana ana kwa ana na uongozi wa Bwana Mkubwa kwani "amani haiji ila kwa ncha ya upanga" (uk.111). Pia, msemo huu umetumiwa na Changawa kusudi awatie moyo Mwarupia na Mwatua walioonekana kuwa katika hali ya kutamauka kutokana na dhuluma za tabaka tawala kwa tabaka tawaliwa. Maneno ya Changawa yalimfanya Mwarupia ajitose kwenye siasa. Yalimzindua akaanza kuona kwamba hakuna jambo ambalo lisingewezekana — likiwemo kuwang'oa viongozi wasiofaa mamlakani. Baada ya kuzinduliwa, Mwarupia naye anatumia maneno yayo hayo anapowahimiza Wanabonde wapiganie usawa. Anawaambia kwamba usawa hauombwi bali hupiganiwa (uk.118). Zaidi ya uzinduzi, maudhui ya mapinduzi na ukombozi wa Wanabonde hususan wachochole wa Bondeni ya viamboni yanaendelezwa. Kama tulivyosema hapo awali, urudiaji wa methali fulani kimatumizi (kama ilivyofanyika hapa) ni dhihirisho la kiasi cha kukita mizizi na kuenea kwa itikadi inayoakisiwa katika jamii. Kutokana na imani inayoelezewa na methali husika, tunaona uhalisia wa maudhui yanayowasilishwa kwa kuwa tangu jadi, vita vya kupigania usawa vimekuwako katika historia ya maendeleo ya jamii.

### 3.2 Hitimisho

Katika sura hii, tumebainisha jinsi fani kwa jumla ilivyotumiwa kuwasilisha maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka katika riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa*. Masuala ya fani ambayo tumechunguza ni wahusika na jinsi wanavyojitokeza kama wahusika kifano, matumizi ya lugha na jinsi yanavyoakisi itikadi katika jamii, usimulizi na msuko. Aidha, tumetaja mandhari japo kwa ufinyu mno ili kuepukana na urudiaji wa yale tuliyochambua katika sura ya pili.

Kwa mujibu wa maelezo yetu, kuna wahusika wanaowakilisha matabaka mawili makuu katika jamii pamoja na nafsi zao wenyewe. Hata hivyo, tunahisi kwamba uumbaji wa wahusika kifano kwa jumla haukufanyika kikamilifu. Kwa mfano, ukuzaji wa Kifuja na Bwana Mkubwa kwa namna ya kuwasawiri wakiwakilisha nafsi zao ndio umetiliwa mkazo badala ya uwakilishi wa maslahi ya tabaka lao. Kupania kushikilia mamlaka na kujiendeleza kwa njia sizizo za haki kwa viongozi hawa si kwa maslahi ya tabaka lao bali ni kwa manufaa yao binafsi. Kwa kulinganisha, Mwarupia amejitokeza kama mwakilishi bora wa tabaka lake kuliko Asisi. Hivi ni kutokana na

motisha yake imara na wazi ambayo imewezesha kuikomboa jamii kutoka utawala mbaya wa Bwana Mkubwa.

Kuhusu usimulizi, tumeeleza jinsi usimulizi maizi na wa kimuhakati unavyojitokeza katika riwaya teule. Kadhalika, tumedadisi msuko katika kila mojawapo ya riwaya teule na kuonyesha mchango wake katika usomekaji wa riwaya husika hasa kupitia sifa bainifu za kila msuko na uwiano wa matukio katika mfululizo wake. Kwa upande mwingine, tumegundua kwamba itikadi ambazo zimejikita katika jamii zimewezesha kukuza maudhui, kuakisi ushabihikweli na kukunjuka kasi kwa msuko. Kwa kiwango kikubwa, itikadi hizo zimeakisiwa kupitia kwa methali. Ugunduzi huu unalingana na mawazo ya Matei (2011:61-70) kwamba methali huambatana sio tu na itikadi bali pia na mazingira ya jamii iliyozizaa, hulka, tamaduni na tajiriba zake. Haya ni baadhi ya masuala ya kijamii yanayohusishwa na nadharia ya u-Marx wa kirasimi na yanayoonyesha nafasi ya methali kuelezea uhalisia.

Ingawa — kwa viwango tofauti katika riwaya teule — kuna masuala ambayo yameonekana kuegemea uramsia, tunaona kwamba kiwango cha uwasilishaji wa maudhui kihalisia na kwa usahihi kupitia kwa fani ni cha kuridhisha. Kulingana na utafiti wetu, uwasilishi wa maudhui kwa namna hii umezingatia uchunguzi wa uumbaji wa wahusika kifano, uwakilishi wa matabaka yao na nafsi zao, uakisi wa uhalisia katika usimulizi na msuko, dhima za itikadi pamoja na uwiano wa fani na maudhui kwa misingi kwamba vipengee hivi haviwezi kutenganishwa.

## SURA YA NNE

## HITIMISHO

### 4.0 Utangulizi

Malengo ambayo yameongoza utafiti wetu ni mawili. Lengo la kwanza limekuwa kuhakiki maudhui, kutathmini uhalisia wake na kuonyesha kiasi cha kuhusiana kwa maudhui hayo na suala la mgawanyiko wa jamii kitabaka katika riwaya zinazohusika. Lengo hili ndilo tumeshughulikia katika sura ya pili.Lengo la pili limehusu kubainisha jinsi fani kwa jumla ilivyotumiwa kusawiri hali ya jamii kugawika kitabaka katika riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa*. Lengo hili nalo limetuongoza katika sura ya tatu. Baada ya kuyashughulikia malengo yetu kwa kina, yafuatayo ndiyo matokeo ya utafiti wetu.

### 4.1 Maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka katika *Yasinya* na *Mwanasiasa*

Katika sura ya pili, masuala mengi na yanayolingana katika riwaya zote mbili yameshughulikiwa. Tumechambua maudhui matatu. Maudhui haya ni umaskini na utajiri, ubaguzi na mchakato wa kutafuta usawa katika jamii iliyogawika kitabaka pamoja na nafasi ya dini katika mfumo wa kitabaka. Miongoni mwa masuala muhimu ambayo tumejadili katika uchanganuzi wa maudhui haya ni usawiri wa makazi ya matabaka yaliyomo katika jamii, umilisi wa rasilimali muhimu za kuzalisha mali, kujinufaisha kwa baadhi ya wanajamii kwa njia zisizo za haki, mchango wa asasi za kiutawala katika kudumisha matabaka, kutamauka kwa tabaka la wachochole, uzinduzi, umoja wa matabaka, maandamano ya wanyonge na mapinduzi. Katika riwaya hizi, maudhui makuu ya mgawanyiko wa jamii kitabaka ni umaskini na utajiri. Kwa mujibu wa tungo tulizozihakiki, haya ndiyo maudhui yanayochukua nafasi kubwa katika historia ya binadamu ambayo Marx alisema hutawaliwa na migongano na mivutano ya kitabaka inayoletwa na hali ya kiuchumi na kisiasa. Katika kiwango cha wastani ni maudhui ya ubaguzi na mchakato wa kutafuta usawa katika jamii iliyogawika kitabaka. Maudhui yanayoonekana kuchukua kiwango cha chini katika uchanganuzi wetu ni yale yanayohusu nafasi ya dini katika mfumo wa kitabaka. Matokeo haya ni bayana kutokana na kiasi cha mifano na maelezo yaliyotolewa kuyahusu maudhui hayo. Maudhui makuu yametolewa mifano mingi na maelezo mapana huku maudhui madogo yakitolewa mifano michache na maelezo finyu.

Kwa kiwango kikubwa, maudhui katika riwaya hizi yanahusiana. Kwa mfano, maudhui yaliyoshughulikiwa katika riwaya hizi yametokana na hali zinazohusiana za kisiasa na kiuchumi

za wanajamii zilizojikita katika historia ya jamii husika. Japo yanahusiana, kuna masuala ambayo yametiliwa mkazo katika riwaya moja kuliko nyingine. Hivi si kumaanisha kwamba mwandishi fulani ana udhaifu bali ni hali inayosababishwa na yale aliyokusudia kutilia mkazo.

Mintarafu ya fasili ya dhana 'tabaka' na 'bwanyenye' katika sura ya kwanza, ni muhimu kueleza iwapo matabaka yaliyobainishwa na nadharia ya u-Marx wa kirasimi ndiyo yanayoakisi muundo wa jamii pana ya kisasa inayowakilishwa katika riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa*. Kama tulivyoeleza, Marx alitambua kuweko kwa matabaka aina sita katika jamii ya kibepari: la wafanyakazi, la matajiri, la kati, la waliotengwa, makabaila na wakulima. Alisema kwamba kati ya matabaka haya, tabaka la mabwanyenye na wafanyakazi (maskini na wauza nguvukazi) ndiyo yaliyokuwa matabaka makuu katika jamii ya kibepari. Kwa mujibu wa utabiri wake, maskini na matajiri ndiyo yangebaki matabaka mawili makuu na kinzani baada ya maendeleo ya jamii (Marx na Engels 1998).

Tukirejelea fasili ya dhana ya 'bwanyenye' tunaona kwamba japo jamii imegawika kitabaka katika riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa* hatubainishiwi waziwazi matabaka mawili makuu kama yale yaliyozungumziwa na Marx katika enzi za kuibuka kwa ubepari. Ingawa kuna matabaka ya matajiri na maskini na ndiyo makuu katika jamii inayowakilishwa na riwaya teule, tabaka la matajiri linajumuisha walio mamlakani, ukoo wao na washirika wao. Kwa upande mwingine, watawaliwa ndio wanaounda tabaka la maskini. Hali hii ni tofauti na ilivyokuwa Ulaya wakati wa kuibuka kwa ubepari ambapo matabaka mawili makuu yaliwahusu mabwanyenye walioanzisha ubepari na kuendelea kuudhibiti kisiasa na kiuchumi kwa kumiliki njia kuu za uzalishaji mali, huku tabaka la wafanyikazi likiwahusisha walioajiriwa na mabwanyenye hao.

Kwa misingi ya nadharia tunayotumia, tungetarajia tungo zetu teule kushughulikia kwa kina mgogoro wa kitabaka baina ya waajiri matajiri na wafanyikazi wauzao nguvukazi zao. Katika jamii zinazotawaliwa na mfumo wa kibepari, chanzo cha mgogoro wa aina hii hasa huwa ni malalamiko kutokana na mishahara duni inayolipwa wafanyikazi huku waajiri wakikataa kuiongeza. Kinyume na matarajio yetu, mgogoro mkuu ulioendelezwa katika riwaya tulizozihakiki (hususan *Mwanasiasa*) ni baina ya tabaka tawala na tabaka tawaliwa. Mgogoro huu unaletwa na uongozi mbaya — uongozi ambao kwa jumla, umesababisha kuzorota kwa maendeleo na hatimaye umaskini mwingi kwa watawaliwa huku wenye mamlaka wakinawiri kiuchumi. Kwa hivyo, kilio cha wanajamii maskini kwa jumla hakitokani na mishahara duni na kutoongezwa kwake bali ni utawala mbaya. Kwa mfano, katika riwaya ya *Yasinya*, Kipokeo

analalamika kwamba viwanda vimefungwa kutokana na gharama ya juu ya uzalishaji iliyosababishwa na barabara mbovu (uk.21). Kwa sababu hii, mhusika huyu anajitetea kutokana na maisha yake ya ukahaba. Anadokeza kwamba ukosefu wa ajira ndio umemwingiza katika mkondo huo wa maisha. Hata pale ambapo suala la uajiri limetajwa, hatuoni kisababishi cha mivutano baina ya mwajiri na mwajiriwa kikiwa kutaka kuongezwa mshahara. Kwa mfano, tunaelezewa katika riwaya ya *Yasinya* (uk.19) kwamba kuna wakati Asisi aliacha kazi kwa sababu ya ujira duni lakini hakukuibuka mvutano baina yake na mwajiri wake huku Asisi akitaka kuongezewa mshahara naye mwajiri akikataa kufanya hivyo. Badala yake, Asisi alilalamika tu baada ya kuacha kazi na bila kuwepo kwa mwajiri wake. Kipokeo naye (riwaya hiyo hiyo) hakuacha kazi kutokana na ujira duni bali ni kwa sababu ya kutumiwa vibaya kimapenzi hasa na mwajiri wake (uk.22). Aidha, riwaya ya *Yasinya* (uk.79), inaeleza kwamba babake Kipokeo alimfanyia Abdul kazi kwa miaka mingi bila kupata mshahara mzuri. Hatuelezwi iwapo malipo hayo duni yaliwahi kuzua mvutano wowote baina ya babake Kipokeo na mwajiri wake.

Tukichunguza riwaya ya *Mwanasiasa* (uk.14) tunaelezwa kuhusu maskini wa Bondeni ya viamboni ambao waliwafanyia kazi matajiri walioishi Bondeni mpya huku wakilipwa mshahara duni na kudharauliwa lakini japo mshahara huo pia haukulipwa kwa urahisi, hatuoni wakichukua hatua yoyote ya kupinga hali hizo kama tunavyotarajia kwa mujibu wa u-Marx wa kirasimi. Badala yake, walijituliza mioyo kwa imani ya kweli kwamba mtaka cha mvunguni sharti ainame. Ni kwa sababu hizi ambapo tunasema kwamba matabaka makuu katika jamii ya sasa hayakusawiriwa kama Marx alivyoyaeleza. Yamebadilika na sio kama yeye (Marx) alivyotabiri. Kwa hivyo, hatuna budi kusema kwamba matabaka aliyoyazungumzia Marx hayana nafasi (katika riwaya teule) ya kuzua mivutano na kuwezesha jamii kuendelea ili kufikia ukamilifu wa kinjozi kupitia ngazi za kiuchumi: ujima, utumwa, umwinyi, ubepari, ujamaa na kisha ukomunisti. Hivi si kumaanisha kwamba hakuna ubepari unaoendelezwa katika riwaya hizo. Hata hivyo, mfumo wa kiuchumi uliopo katika jamii zinazowakilishwa na riwaya husika unaonekana kuwa ubepari uchwara. Mtazamo huu ni bayana kutokana na mifano mingi tuliyoitoa katika uchambuzi wa maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka. Kwa mfano, tabaka la wachache, hasa matajiri walio mamlakani ukoo wao na washirika wao, linaonekana likimiliki njia kuu za kuzalisha mali. Matabaka yale mengine yaliyotajwa na Marx yana wawakilishi wao lakini kutokana na ufinyu wa maendelezo yake na uchache wa wahusika waliotajwa, hayabainiki kama makundi ya watu walio na sifa sawa za kiuchumi zinazowatambulisha.

Ijapokuwa Mwarupia (katika riwaya ya *Mwanasiasa*) hakuwa ameajiriwa kazi na kwamba ndiye anayetetea Wanabonde wachochole, yeye anaonekana kama mwakilishi wa tabaka la kati. Hivi ni kutokana na hali yake ya kiuchumi inayoonekana kuwa nzuri kuliko ya Wanabonde wenzake ambao walikwenda kumkopa kwenye kijiduka chake. Tunaarifiwa pia kwamba, Mwarupia alinyenyekea na kuishi maisha ya kawaida japo alikuwa na uwezo wa kula mchuzi mzito wa samaki (uk.41). Kwa upande mwingine, kahaba Aisha na watoto ombaomba katika *Yasinya* wanawakilisha tabaka la waliotengwa katika jamii. Tabaka la wakulima halidhihiriki pengine kwa sababu watu wengi wamebaki maskwota baada ya kunyang'anywa mashamba na matajiri au wenye uwezo wa kisiasa. Kutokana na dhuluma hizi, huenda pia ikawa tabaka hili limejiunga na tabaka la wafanyakazi wanaouza nguvukazi kama hatima yao ilivyotabiriwa na Marx. Kwa hivyo, hatuwezi kusema kwamba matajiri wanaomiliki mashamba makubwa ndio wanaounda tabaka la wakulima kwa sababu tabaka hili kwa mujibu wa Marx na Engels huwa ni la watu waliotapakaa na wasio na uwezo wa kupanga na kuleta mabadiliko ya kijamii na kiuchumi. Vilevile, tabaka la makabaila halijabainishwa kupitia umilisi wa rasilimali za kupangisha. Ingawa kuna majumba ya kifahari yaliyojengwa katika eneo la Bondeni Mpya (riwaya ya *Mwanasiasa*) hatujulishwi kuhusu shughuli za kuzalisha mali zinazohusiana na majumba hayo na tabaka hili.

Kwa kiwango kikubwa, uhalisia wa maudhui umejitokeza kwa kuwa masuala yaliyomo yanapatikana katika jamii ya sasa. Kwa mfano, uhalisia huu unadhihirika kupitia usawiri wa makazi ya matabaka yaliyomo katika jamii. Kwa mujibu wa maelezo katika tungo ambazo tumehakiki, haya ni mazingira yaliyomo katika nchi nyingi hasa barani Afrika. Ingawa majina ya kweli yanayorejelea nchi mahususi zinazowakilishwa katika riwaya teule na makazi ya wanajamii yamebanwa hasa kupitia matumizi ya majazi, tunaona kwamba kwa kiwango kikubwa, mandhari ya mahali (hususan makazi) yaliyoteuliwa katika kuendeleza maudhui tuliyochunguza ni mwigo wa maisha halisi yanayodhihirisha kugawika kwa jamii katika matabaka ya matajiri na maskini. Mandhari ya kiwakati yanayoelezea vipindi vya kihistoria ambapo misingi ya utabaka katika jamii iliwekwa na kuendelezwa yamefafanuliwa japo si kwa namna inayoakisi wakati maalum. Kutokana na ugunduzi huu, ni muhimu kusema kwamba ingawa uwasilishi wa maudhui una jaribio la kuiga maisha halisi ya jamii, mandhari ya kijiografia na kihistoria katika tungo teule si ya kweli. Tukichunguza kujiendeleza kwa baadhi ya wanajamii kwa njia zisizo za haki, tunaona kwamba suala hili linaakisi uhalisia maadamu kutokana na hali, mitazamo na matendo ya waliomo katika tabaka la matajiri, tunadhihirishiwa mwonoulimwengu wao uliojikita katika ubinafsi, ubiashara na usokidini kama ilivyokuwa baada

ya kutoweka kwa fasihi ya kiramsia. Hata hivyo, ni kinyume cha inavyopasa kuwa katika mfumo wa ubepari kwamba upatikanaji wa mali kupitia unyonyaji wa tabaka la wafanyakazi umeelezwa kwa ufinyu mno katika riwaya teule na hasa katika riwaya ya *Yasinya.*

Changamoto zinazoelezwa katika jamii zinazowakilishwa na riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa* zimo katika mataifa tunayoweza kujitambulisha nayo moja kwa moja. Anwani za riwaya hizi zinadokeza masuala yanayohusiana na utafiti wetu na ambayo yamefungamanishwa vilivyo na anwani hizo. Ijapokuwa majina ya mataifa yanayowakilishwa katika riwaya hizi hayakuwekwa wazi, riwaya ya *Yasinya* inataja mandhari halisi ya mahali nchini Kenya kama Kajiado, uliokuwa Mkoa wa Mashariki, Mlolongo, Nzoia, Namanga *Road* na daraja la Athi *River* katika tukio lililopelekea kufa kwa Chifu Kifuja. Aidha, kisa cha mhusika MA kinaeleza kuhusu marehemu binti yake wa kwanza aitwaye Nyanke. Tunajulishwa kwamba malengo ya binti huyu yalikuwa kuondoa ujinga, umaskini na kupigana na maradhi kupitia mwito wa tuvute pamoja (uk.11). Malengo ya binti huyu ndiyo yaliyosemwa kuwa malengo ya nchi ya Kenya baada ya kujinyakulia uhuru kutoka kwa wakoloni. Mwito wa tuvute pamoja unarejelea mwito wa *harambee* ambao umekuwa maarufu sana nchini Kenya. Kwa maoni yetu, binti anayetajwa hapa (Nyanke) anaweza kuwa nchi ya Kenya baada ya kupata uhuru. Kwa hivyo, mandhari ya riwaya hii yanaweza kuwa nchi ya Kenya au eneo fulani katika nchi hiyo. Kwa upande mwingine, mandhari ya riwaya ya *Mwanasiasa* yanarejelea jamii inayoishi pwani, karibu na pwani au kisiwa kilichoko katika nchi za Uarabuni. Hivi ni kwa sababu, msimulizi anataja utawala wa zamani ulioongozwa na sultani ambaye alikuwa kiongozi hususan Uarabuni (uk.12-13). Katika kutoroka kwa Bwana Mkubwa (baada ya mapinduzi), tunaarifiwa kwamba alipanda punda hadi pwani ambako alitumia kihori cha uvuvi kutorokea kwa majirani (uk.122). Aidha, msimulizi anataja makazi ya Maweni katika Bondeni mpya yaliyojengwa kwa mawe ya pwani. Kadhalika, kazi ambayo Semkopi aliwafanyia wenye minazi — ya kuangua nazi na kugema ni shughuli inayohusishwa na mandhari ya pwani hasa pwani ya nchi za Kenya na Tanzania.

Ingawa riwaya teule zina wahusika walio katika harakati za kutatua matatizo yao na ya jamii yao kama inavyopaswa kuwa katika tungo za kihalisia, kuna wahusika ambao wamebuniwa na kupewa majina ya kimajazi kwa mujibu wa sifa zinazowatambulisha — hali ambayo haiwajengi vizuri kihalisia. Wahusika hawa ni kama vile Bwana Mkubwa na Bambua katika riwaya ya *Mwanasiasa*, Kijasiri, Kikwasi na MA katika riwaya ya *Yasinya*. Kama jina lake lilivyo, Bwana Mkubwa alikuwa kiongozi na ameumbwa kwa kupewa sifa zilizotiwa chumvi kiasi kwamba inaonekana kana kwamba baadhi ya wanajamii walimwabudu kabla ya kuzinduka. Hivi ni

kinyume na uhalisia unaoangazia mambo katika ukawaida wake na wala sio kuyatia chumvi (Wamitila 2002:115). Haumtukuzi au kumkweza mtu binafsi na matakwa yake katika ngazi za kijamii kama Bwana Mkubwa anavyofanywa. Hata hivyo, sifa alizopewa Bwana Mkubwa (za kutiwa chumvi) zinaweza kuakisi uhalisia kutokana na unafiki wa watu wanaojitakia makuu kutoka kwa kiongozi huyu hasa kupitia kujiendeleza kwa njia zisizo za haki bila kuchukuliwa hatua yoyote ya kisheria. Mahusiano kama hayo ya kinafiki na kwa sababu zizo hizo yanaweza kuthibitika katika tawala nyingi za ulimwengu wa sasa. Bambua ni mhusika bapa kielelezo kwa wema wake katika kuwatumikia wanajamii. — hususan katika kupiga mbiu. Utumishi wake (upigaji mbiu) ni ishara ya umoja wa jamii maalum na uhalisia ulio kielelezo cha utamaduni wa jamii hiyo.

Bambua ni kiwakilishi cha tabaka la watu maskini. Iwapo hakuwa na akili punguani, wema wake umekithiri na kuonekana ukikiuka ukawaida wa binadamu. Kwa mfano, japo angealikwa na kuhusishwa katika kupika vyakula kwenye sherehe, kukosa kula chakula hicho hakukuwa hoja kwake na angeridhika hata alipoambulia ukoko au utandu (uk.3). Tunapoisoma riwaya ya *Mwanasiasa*, tunahisi kwamba huu si uhalisia. Kikwasi ni jina linalotokana na umilisi wa mali nyingi (ukwasi) na linarejelea mtu aliyekuwa wa tabaka la juu kiuchumi. Kwa upande mwingine, mhusika Kijasiri amepewa jina hili kutokana na sifa yake ya ujasiri hasa katika kukabiliana na dhuluma zinazoendelezwa na tabaka tawala kwa tabaka tawaliwa. Mhusika MA katika *Yasinya*, ambaye ni muhimu katika kuelezea historia ya jamii katika muktadha wa kujengeka kitabaka, anajitokeza kama mhusika asiye halisi. Kwa mujibu wa kisasili katika fasihi simulizi ya jamii ya Mabonde, MA ni nchi au ardhi ya Mabonde. Ni mtu aliyegeuka ardhi baada ya miaka mingi. Ni mhusika asiye halisi anayewakilisha ardhi ya Wanamabonde kama mama wa jamii hasa ya Waafrika (uk.37). Hata hivyo, athari yake kwa wahusika kama Asisi inaibua matendo na kujenga maudhui ya kisiasa na kiuchumi yanayoonekana kuwa halisi katika jamii ya sasa.

Uwasilishaji wa uhalisia katika hali yake ya kimaendeleo na kimapinduzi umejitokeza wazi zaidi katika riwaya ya *Mwanasiasa* kuliko *Yasinya*. Tofauti ya uwasilishaji wa uhalisia pia imetokana na uteuzi wa mandhari ya mahali, wahusika na matendo yao kama inavyobainika katika riwaya zinazohusika. Kwa ufupi, kiwango cha uhalisia katika riwaya ya *Mwanasiasa* kimepiku kile cha riwaya ya *Yasinya*. Hata hivyo, hatuna budi kusema kwamba riwaya moja ni mwangwi wa nyingine katika kuisawiri jamii ya sasa kitabaka na kihalisia. Aidha, tungo hizi ni mwangwi wa maoni ya wahakiki wengi kwamba uhalisia ndio mkondo tawala katika utanzu wa riwaya. Chembechembe za uramsia katika riwaya hizi hasa kutokana na matumizi ya majazi ni kawaida

katika utunzi wa fasihi ambapo aghalabu, mitindo ya uhalisia na uramsia huingiliana (Mbatiah 2016:96).

## 4.2 Fani na uwasilishaji wa maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka

Katika sura ya tatu, tumebainisha jinsi fani kwa jumla ilivyotumiwa kuwasilisha maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka katika riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa*. Masuala ya fani ambavyo tumechunguza ni wahusika na jinsi wanavyojitokeza kama wahusika kifano, matumizi ya lugha na jinsi yanavyoakisi itikadi katika jamii, usimulizi na msuko. Aidha, tumetaja mandhari japo kwa ufinyu mno ili kuepukana na urudiaji wa yale tuliyochambua katika sura ya pili.

Kwa mujibu wa maelezo yetu, kuna wahusika wanaowakilisha matabaka mawili makuu katika jamii pamoja na nafsi zao wenyewe. Kama tulivyosema, Mwarupia katika riwaya ya *Mwanasiasa* na Asisi katika riwaya ya *Yasinya* wanawakilisha tabaka la maskini. Tabaka la matajiri linawakilishwa na Kifuja na Bwana Mkubwa katika riwaya ya *Yasinya* na *Mwanasiasa* mtawalia. Huku pia kukiwa na wahusika wengine wadogo wanaoonekana kuwakilisha matabaka yao, tunahisi kwamba uumbaji wa wahusika kifano kwa jumla haukufanyika kikamilifu. Kwa mfano, mazingira kifano ya Bwana Mkubwa, (hususan yale yanayoonekana) yameelezewa tu kupitia makazi yake ya kifahari yaliyokuwa eneo la Ngomeni. Hali hii inakaribia kuwa sawa hata kwa wahusika kama Mwarupia, Asisi na Kifuja. Ukuzaji wa Kifuja na Bwana Mkubwa kwa namna ya kuwasawiri wakiwakilisha nafsi zao ndio umetiliwa mkazo badala ya uwakilishi wa maslahi ya tabaka lao. Kwa mfano, kupania kushikilia mamlaka na kujiendeleza kwa njia zisizo za haki kwa viongozi hawa si kwa maslahi ya tabaka lao bali ni kwa manufaa yao binafsi. Kwa kulinganisha, Mwarupia amejitokeza kama mwakilishi bora wa tabaka lake kuliko Asisi. Hivi ni kutokana na motisha yake imara na wazi ambayo imewezesha kuikomboa jamii kutoka utawala mbaya wa Bwana Mkubwa.

Kuhusu usimulizi, tumeeleza jinsi usimulizi maizi na wa kimuhakati unavyojitokeza katika riwaya teule. Kadhalika, tumedadisi msuko katika kila mojawapo ya riwaya teule na kuonyesha mchango wake katika usomekaji wa riwaya husika hasa kupitia sifa bainifu za kila msuko na uwiano wa matukio katika mfululizo wake. Kwa upande mwingine, tumegundua kwamba itikadi ambazo zimejikita katika jamii zimewezesha kukuza maudhui, kuakisi ushabihikweli na kukunjuka kasi kwa msuko. Kwa kiwango kikubwa, itikadi hizi zimeakisiwa kupitia kwa methali. Ugunduzi huu unalingana na mawazo ya Matei (2011:61-70) kwamba methali

huambatana sio tu na itikadi bali pia na mazingira ya jamii iliyozizaa, hulka, tamaduni na tajiriba zake. Haya ni baadhi ya masuala ya kijamii yanayohusishwa na nadharia ya u-Marx wa kirasimi na yanayoonyesha nafasi ya methali kuelezea uhalisia. Tumeshuhudia urudiaji wa baadhi ya methali katika miktadha mbalimbali, jambo ambalo kulingana nasi ni thibitisho la kiwango cha kukita mizizi kwa imani inayoakisiwa na methali husika. Kwa kiasi kikubwa, itikadi hizi zina misingi yake katika hali zinazowakumba wanajamii kama vile umaskini, utajiri, nguvu za kisiasa, kutamauka na mwamko. Kiuhalisia, hali hizo ndizo zinazoimbua na kusukuma mbele matendo ya wahusika yanayoendeleza maslahi yao binafsi na ya matabaka yao.

Ingawa — kwa viwango tofauti katika riwaya teule — kuna masuala ambayo yameonekana kuegemea uramsia, tunaona kwamba kiwango cha uwasilishaji wa maudhui kiuhalisia na kwa usahihi kupitia kwa fani (kwa jumla)ni cha kuridhisha. Kulingana na utafiti wetu, uwasilishi wa maudhui kwa namna hiyo umezingatia uchunguzi wa uumbaji wa wahusika kifano, uwakilishi wa matabaka yao na nafsi zao, uakisi wa uhalisia katika usimulizi na msuko, dhima za itikadi pamoja na uwiano wa fani na maudhui kwa misingi kwamba vipengee hivi haviwezi kutenganishwa.

**4.3 Ufaafu wa nadharia husika na changamoto za utafiti**

U-Marx wa kirasimi ni nadharia ya kijamii iliyo na sifa ya kukamatanisha masuala mengi yanayohusiana na jamii. Kwa hivyo, nadharia hii imekuwa muhimu katika kuhakiki maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka katika muktadha wa kiuhalisia. Aidha, riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa,* tulizozihakiki kwa msingi wa nadharia teule zina masuala ya kisiasa na kiuchumi yanayopewa uzito na nadharia hiyo. Kwa hivyo, nadharia ya u-Marx wa kirasimi imekuwa mwafaka katika kushughulikia mada yetu. Hata hivyo, matumizi yake yametupa changamoto kutokana na ukweli kwamba Marx aliikita nadharia hii katika ubepari wa Ulaya iliyokomaa kiuchumi katika karne ya 18 huku nasi tukichunguza hali za mfumo sawia wa kiuchumi lakini ambao umejitokeza kuwa ubepari uchwara unaotawala katika mataifa ya Kiafrika kwa sasa. Kutokana na mfumo huu (ubepari uchwara), utafiti wetu umekumbwa na changamoto zilizojikita kwenye upungufu wa riwaya teule zikipimwa katika mizani ya nadharia husika.

Kama tulivyodhihirisha katika sura ya pili na ya tatu, mojawapo ya changamoto zilizokumba utafiti wetu ni kwamba mahusiko ya dhana muhimu zinazohusiana na nadharia hii (kama vile tabaka, bwanyenye, ubidhaaishaji na uzinduzi) katika tungo teule yamekuwa telezi hivi kwamba hazijitokezi wazi kama zilivyoelezewa na Marx. Tofauti na mtazamo wa u-Marx wa kirasimi,

chanzo cha kuweko kwa matabaka katika jamii ya sasa ni uongozi mbaya, tamaa, ulafi na ufisadi hususan wa walio mamlakani, ukoo wao na washirika wao. Marx hakuwataja wezi wa mali ya umma kama watu waliounda tabaka la juu (mabwanyenye) katika jamii. Tayari, tumelishughulikia suala hili la matabaka kwa kina na hakuna haja ya kuliangazia zaidi.

Mbali na usawiri wa matabaka visivyo, riwaya zote mbili zinakosa maudhui ya kina yaliyojikita kwenye ubidhaaishaji. Kutokana pengine na hali duni ya kiuchumi ya jamii zinazowakilishwa katika riwaya teule au labda tamaa kuu ya mali na kutotosheka kwa matajiri, hatuoni mahusiko ya dhana hii (ubidhaaishaji) kupitia ununuzi na umilisi wa vitu ambavyo labda si muhimu sana kwao au hali ya kuvikinai vitu hivyo haraka. Katika kushughulikia maudhui ya uzinduzi, jamii pana katika *Yasinya* ni tuli hivi kwamba haijashirikishwa vilivyo katika harakati za kujikomboa au kupigania usawa kupitia mapinduzi. Kama tulivyosema awali, nadharia za ki-Marx zinapaswa kuhusishwa na kuandamana pamoja dhidi ya mfumo wa kibepari. Kwa hivyo, ingekuwa bora kama riwaya hii (*Yasinya*) ingeonyesha kushirikishwa kwa jamii nzima inayodhulumiwa katika maandamano ya kuung’oa mamlakani utawala dhalimu wa Chifu Kifuja. Ni upungufu wa riwaya hii kwamba badala ya maandamano na mapinduzi yanayoshuhudiwa katika riwaya ya *Mwanasiasa*, riwaya ya *Yasinya* inaipa elimu nafasi kubwa katika kuleta mabadiliko ya jamii. Suala hili ni bayana hasa kwa kutazama mawazo ya wasomi kama Amazulu, Kijasiri, Gwiji na Asisi. Kwa mfano, Akiongea katika kumbukumbu ya mhadhiri Gwiji, profesa Amazulu anasema kwamba elimu ni uhuru. Yaani, elimu huizindua jamii huku ikimwezesha mja kuwaza kwa kina na kuhakiki mambo kabla ya kuyatenda. Aidha, inaondoa kiza, kulainisha nyoyo zenye kutu na kunyoosha mawazo yaliyopinda. Manufaa haya humwezesha mtu kutafuta malengo ya uwepo wake binafsi na wa jamii yake (uk.153). Kulingana na Kijasiri, ni elimu tu ambayo ingeiwezesha jamii ya Mabonde kujikomboa kiuchumi na kijamii. Elimu anayoipendekeza ni ya uwekezaji, biashara na teknolojia katika ulimwengu unaoendelea (uk.104). Kutokana na mapuuza ya elimu ya aina hii, ndoto na tamaa ya kujikomboa kwa jamii hii kiuchumi na kijamii imegonga mwamba.

Katika riwaya ya*Yasinya*, mwito wa ‘pamoja tunaweza’ (*harambee*) hauna nafasi ya kuikomboa Mabonde kiuchumi na kijamii. Waliokuwa katika mstari wa mbele kupigania mabadiliko katika jamii (kama Asisi na Kijasiri) wameishia kuhubiri umoja na maridhiano kupitia wito wa kuzika yaliyopita na kuganga yajayo. Wanawarai Wanamabonde kusameheana — na hasa kuwasamehe Kifuja na Mayowe — kwa sababu hakuna binadamu aliye mkamilifu (uk.158). Upungufu mwingine wa riwaya ya *Yasinya* umeonekana pale ambapo Anao, Liwazo na bin Kifuja kutoka

tabaka la matajiri wamejiunga na walalahoi katika kupigania usawa wa Wanamabonde. Kadhalika, Elimika (Bibiye Chebaskwony) pia kutoka tabaka la matajiri, alipinga ubaguzi kama mwanawe Liwazo. Haya yanathibitishwa na udhamini wake wa siri alioutoa kwa shirika la Kijasiri na Asisi lililopigania afya na makazi bora katika Mabonde.

Kwa mujibu wa nadharia ya u-Marx wa kirasimi, tungetarajia Asisi na Mwarupia wapiganie mishahara bora kutokana na malipo duni ya tabaka la wafanyakazi. Badala yake, Asisi anakazana kupigania afya na makazi bora huku Mwarupia akipigania mabadiliko katika uongozi. Kinyume na inavyopaswa kuwa — kulingana na nadharia inayoongoza utafiti wetu — matendo ya Anao, Liwazo, bin Kifuja na Elimika (katika *Yasinya*) yanalenga kuendeleza maslahi ya tabaka tofauti na lao. Wao wanadhihirisha mabadiliko katika mahusiano baina ya wanajamii kutoka matabaka mawili tofauti. Matendo yao yanaweza kusababisha kutoweka kwa mkinzano unaokuwako baina ya matabaka ambao kwa mujibu wa Marx na Engels, ndio huwezesha jamii kuendelea. Kutokana na mienendo ya wahusika hawa pamoja na nafasi inayopewa elimu katika kuikomboa jamii, tunaona kwamba si lazima jamii iendelee kupitia mivutano ya kitabaka, maandamano na mapinduzi bali inaweza kuendelea kupitia kusisitiza aina fulani ya masomo katika taasisi za elimu, kuzingatia maridhiano ya wanaozozana na pia kuthamini utu wa binadamu. Kwa maoni yetu, mienendo ya Anao, Liwazo, bin Kifuja na Elimika (katika *Yasinya*) inatia tumaini kwa jamii ya sasa inayowakilishwa katika *Yasinya* ambapo kizazi cha sasa, hata kutoka tabaka la matajiri kimeanza kupinga maonevu na ubaguzi wa wanajamii ambao hatimaye huibua matabaka. Hali sawia na hiyo inaonekana katika riwaya ya *Mwanasiasa* ambapo vita vya ukombozi vinapoendelea, askari waliokuwa wakilinda kasri la Bwana Mkubwa wanakataa kutii amri ya kamanda wao na kujiunga na Wanabonde wengine kumtetea Mwarupia — kiongozi wa wanaodhulumiwa katika jamii (uk.121). Ni muhimu ieleweke kwamba askari hao hawakuamua kumtetea Mwarupia baada ya kushindwa nguvu na waandamanaji bali ni baada ya kuona kwamba haikuwa haki kuwakabili waandamanaji kwa bunduki. Kwa maoni yetu, haya ni mabadiliko makubwa yanayopingana na mtazamo wa Marx kuhusu maendeleo ya jamii kutokana na mivutano ya kitabaka.

Imani za kitamaduni katika riwaya ya *Mwanasiasa* zinaonyesha picha ya jamii inayopuuza kupinga tofauti za kijinsia zinazowanyima wanawake nafasi sawa na wanaume ya kutetea maslahi yao ya kiuchumi. Katika mkutano wa Bwana Mkubwa, wanawake hawakuruhusiwa kusimama mbele ya watu wajiwasilishie mahitaji yao ya kiuchumi kwa kiongozi wao. Walifungwa na mila zilizochukulia kwamba kufanya hivyo ilikuwa mwiko. Ni upungufu wa

riwaya hii kwamba imani kama hizi zinaonekana pia kuwa na nafasi ya kuchangia katika kuendeleza matabaka katika jamii — bali kwa misingi ya kijinsia na kinyume na mtazamo wa Marx. Kwa mujibu wa Barry (2002), hili ni suala la kifeministi ambalo huchukuliwa na nadharia hii (u-Marx wa kirasimi) kama suala linalohusiana na nguvu za kiuchumi zinazoathiri siasa (tafsiri yetu).

Kwa mujibu wa utafiti huu, tunaona kwamba Marx alikuwa amejibana sana katika mtazamo wake kuhusu mfumo wa kitabaka na maendeleo ya jamii. Hata hivyo, nadharia ya u-Marx wa kirasimi imefaulu kuongoza utafiti wetu maadamu imetimiza malengo ya utafiti. Utafiti wetu umedhihirisha maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka na jinsi maudhui hayo yalivyowasilishwa kupitia kwa fani. Aidha, tumeonyesha kwamba sifa za kikorombwezo, hususan siasa, zimetegemea uzalishaji na usambazaji wa mali (msingi) na kuzua mgogoro unaoakisi kuweko kwa matabaka katika jamii. Kwa mujibu wa nadharia yetu, hii ndiyo sababu wanajamii hasa katika riwaya ya *Mwanasiasa* wamo katika harakati za kuleta mageuzi katika muundo wa kiutawala au kisiasa ili kubadili umilisi wa mali unaoegemea ubepari uchwara unaodhibitiwa na nguvu za kisiasa.

### 4.4 Pendekezo kwa watafiti wa baadaye

Wahakiki hushikilia kwamba hakuna fasiri ya kazi ya kifasihi inayoweza kusemwa kuwa ni ya mwisho. Vivyohivyo, hakuna nadharia ya fasihi inayotosheleza kuihakiki kazi ya fasihi. Muhimu ni yale mhakiki anayolenga kudhihirisha kwa mujibu wa vigezo fulani. Kwa sababu hizi, tahakiki hii haiwezi kuwa mwisho wa kuhakiki riwaya ambazo tumejikita kwazo na kwa nadharia ambayo imeongoza utafiti wetu. Kwa hivyo, tunapendekeza kwamba watafiti wa baadaye wanaweza kuhakiki maudhui mengine kama vile usawiri wa mwanasiasa, uongozi, tamaa na mengine mengi. Kadhalika, wanaweza kuchunguza vipengee vingine vya fani katika ujumla wake. Isitoshe, wanaweza kuhusisha mikabala mingine ya u-Marx badala ya u-Marx wa kirasimi au watumie nadharia nyingine zisizohusiana na u-Marx.

### 4.5 Muhtasari wa hitimisho

Kwa kutumia nadharia ya u-Marx wa kirasimi, tumehakiki riwaya za *Yasinya* na *Mwanasiasa* ili hasa kudhihirisha maudhui ya mgawanyiko wa jamii kitabaka na jinsi fani kwa jumla ilivyotumika kuyawasilisha. Uhakiki wetu umekuwa wa kulinganisha na kulinganua yale tuliyochunguza katika riwaya husika. Tumefanya hivyo kwa kuchunguza kiasi cha kuhusiana kwa maudhui katika riwaya teule na suala la mgawanyiko wa jamii kitabaka. Tumetathmini kiasi

hicho katika viwango vitatu: kiwango cha juu zaidi kinachohusisha maudhui makuu, cha kadri au wastani kinachobeba maudhui madogo na kile cha chini kabisa kinachohusu maudhui madogo zaidi. Kilichofanikisha kutathmini viwango hivi ni idadi ya mifano iliyotolewa na kina cha maelezo cha maudhui husika. Aidha, tumeweza kubainisha kuwa maudhui hayo ni halisi kwa kiwango kikubwa na kwamba fani imetumika kwa usahihi na kihalisia kuyawasilisha. Ingawa nadharia ya u-Marx wa kirasimi imefaa katika utafiti wetu, tumebainisha changamoto za kuitumia hasa kutokana na ubepari uchwara uliomo katika jamii zinazowakilishwa na riwaya teule. Hata hivyo, tahakiki hii itawezesha uelewa wa kina wa riwaya tulizozihakiki pamoja na kufanikisha urejelezi katika mtalaa wa fasihi.

# MAREJELEO


Aswani, B., Mayaka, G. na Riro, M. (Tarehe haikutolewa) *Misingi ya Nadharia na Mbinu za Utafiti*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers.

Barry, P. (2002) *Beginning Theory*: *An Introduction to Literary and Cultural Theory*. New York: Manchester University Press.

Beard, A. na Kent, A. (2012) *AQA English Literature B*. Cheltenham: Nelson Thornes Publishers.

Bibiana, M.A. (2014) 'Masuala ya Kisiasa Katika Riwaya za Shaaban Robert: Mfano wa *Kusadikika* na *Kufikirika*'. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania: Haijachapishwa.

BSKT, (1997) *The Holy Bible in Kiswahili: Union Version*. Dodoma: The Bible Societies of Kenya and Tanzania.

CUP, (2009) *Cambridge Academic Content Dictionary*. 1$^{st}$ Edition. New York: Cambridge University Press.

Harriet, T. na Adelaida, LM. (2003) *The Cambridge Companion to the Spanish Novel From 1600 to the Present.* Cambridge: Cambridge University Press.

Kamunde, M.E. (1983) 'Kilio Cha Wanyonge Katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed'. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu Cha Nairobi: Haijachapishwa.

King'ei, K. na Ndalu, A. (2009) *Kamusi ya Methali za Kiswahili*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Leo, L.S. (2014) *Yasinya*. Nairobi: Focus Publishers.

Lomatoro, P.J. (2014) 'Viwango vya Uhalisi na Ubunifu Katika Riwaya Teule za Kiswahili'. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Kenyatta: Haijachapishwa.

Lukac's, G. (1972) *Studies in European Realism*. London: Merlin Press Publishers.

Marx, K. na Engels, F. (1976) *Marx and Engels on Literature and Art*. Moscow: Progress Publishers.

Marx, K. na Engels, F. (1998) *The Communist Manifesto*. London: Verso Publishers.

Matei, A.K. (2011) *Fani ya Fasihi Simulizi kwa Shule za Upili*. Nairobi: Oxford University Press.

Mbatiah, M. (2016) *Riwaya ya Kiswahili: Chimbuko na Maendeleo Yake*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Mdoe, S. (2014) *Mwanasiasa*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Msokile, M. (1993) *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mutea, R. (2015) *Social Research Methods*. Meru: Eureka Publishers.

Muthoni, M. (2014) 'Uhakiki wa Maudhui na Mtindo Katika Riwaya ya *Tikitimaji*". Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Mwakio, L.W. (2016) 'Matumizi ya Tashbiha, Sitiari na Taashira Katika *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine'*. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Njogu, K. (1997) *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar*. Nairobi: Nairobi University Press.

Njoroge, A.W. (2014) 'Viongozi Kama Visababishi Vya Mabadiliko Katika Riwaya za Mwenda Mbatiah'. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi:Haijachapishwa.

Nyutu, W.J. (2016) 'Mtindo Katika Kazi za Kubuni za Leonard Sanja'. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Oriedo, H.E. (2007) *Istilahi za Fasihi ya Kiswahili*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Raines, J.C. (2002) *Marx on Religion.* Philadelphia: Temple University Press.

Rono, P. (2013) 'Uhakiki wa Kimaudhui na Kifani wa *Kidagaa Kimemwozea'*. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Said, A.M. (1995) *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Shaw, H. (1905) *Dictionary of Literary Terms*. Michigan: McGraw-Hill Publishers.

Teun, A.V.D (1998) *Ideology: A Multidisciplinary Approach*. London: Sage Publications. East African Educational Publishers.

TUKI, (2013) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Wafula, R.M. na Njogu, K. (2013) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation Publishers.

Waititu, F. Ipara, I. Okaalo, B. na Vuzo, A. (2003) *Kiswahili Fasaha: Kidato cha Pili.* Nairobi: Oxford University Press.

Wamitila, K.W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers.

___________ (2003) *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publications.

Williams, R. (1977) *Marxism and Literature*. Oxford: Oxford University Press